

/// **ULINGANISHI WA KIRAI TENZI CHA KS NA EK**
KIMOFOSINTAKSIA: MTAZAMO WA
UMINIMALISTI //

NA

MARY PHELLONICAH IOICHOE

TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA
BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI WA SANAA KATIKA
CHUO KIKUU CHA NAIROBI

University of NAIROBI Library



0496784 0

AGOSTI 2005.

IKIRARI


Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kikuu kingine chochote kwa kutosheleza mahitaji ya shahada yoyote.



MARY PHELLONICAH OICHOE


(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika Chuo Kikuu Cha Nairobi.



PROF. ABDULAZIZ M.

(Msimamizi)



DKT. SCHROEDER H.

(Msimamizi)

YALIYOMO

Uk.

Mada.....	(i)
Ikirari.....	(ii)
Yaliyomo.....	(iii)
Tabaruku.....	(vii)
Shukrani.....	(ix)
Mshabaha wa konsonanti za AKIKI.....	(xi)
Mshabaha wa vokali za AKIKI.....	(xii)
Muhtasari.....	(xiii)
Orodha ya vifupisho na ishara.....	(xiv)

SURA YA KWANZA

1.0.0	Utangulizi.....	1
1.0.1	Lugha ya Ekegusii	2
1.0.2	Lugha ya Kiswahili Sanifu.....	3
1.1.0	Somo la utafiti.....	4
1.2.0	Sababu za kulichagua somo	5
1.3.0	Nadharia tete.....	6
1.4.0	Madhumuni ya utafiti.....	7
1.5.0	Upeo na mipaka.....	7
1.6.0	Udurusu wa yaliyoandikwa kuhusu somo hili	8
1.7.0	Msingi wa nadharia.....	12
1.7.1	Uminimalisti.....	13
1.7.2	Kanuni ya kukagua sifa	16
1.7.3	Nafasi ya mofolojia katika uminimalisti.....	18

1.8.0	Njia za utafiti.....	21
	Tanbihi.....	22

SURA YA PILI

2.0.0	Utangulizi.....	23
2.1.0	Mofolojia ya nomino.....	25
2.1.1.0	Uambishaji wa nomino.....	25
2.1.2.0	Ufafanuzi wa ngeli kiulinganishi.....	29
2.1.2.1	Ngeli 1 / 2.....	29
2.1.2.2	Ngeli 3 / 4.....	32
2.1.2.3	Ngeli 5 / 6	33
2.1.2.4	Ngeli 7 / 8.....	36
2.1.2.5	Ngeli 9 / 10.....	37
2.1.2.6	Ngeli 11/ 10a/ 6a/ 11a.....	39
2.1.2.7	Ngeli 12/ 8a.....	40
2.1.2.8	Ngeli 14.....	41
2.1.2.9	Ngeli 15.....	42
2.1.2.10	Ngeli 16 /17 / 18.....	43
2.2.0	Unyambuaji wa nomino.....	45
2.3.0	Uainishaji wa ngeli kisintaksia.....	47
2.2.1	Kundi la ngeli 1 / 2.....	48
2.2.2	Kundi la ngeli 3 / 4	50
2.2.3	Kundi la ngeli 5 / 6.....	51
2.2.4	Kundi la ngeli 7/ 8.....	52
2.2.5	Kundi la ngeli 9 / 10.....	52
2.2.6	Kundi la ngeli 11/10a/6a/11/6a.....	53
2.2.7	Kundi la ngeli 12 / 8a	54
2.2.8	Kundi la ngeli 14	55
2.2.9	Kundi la ngeli 15.....	56
2.2.10	Kundi la ngeli 16 / 17/ 18.....	56

2.3.0	Ulinganishaji wa KN cha Ks na Ek.....	57
2.3.1.0	Vivumishi katika lugha ya Ks na Ek.....	58
2.3.1.1	Ulinganishi wa vivumishi vya sifa katika Ks na Ek.....	58
2.3.1.2	Vivumishi viulizi vya Ks na Ek.....	59
2.3.1.3	Vivumishi vya idadi vya Ks na Ek.....	60
2.3.1.4	Vivumishi vionyeshi vya Ks na Ek.....	60
2.3.1.5	Vivumishi vimilikishi vya Ks na Ek.....	64
2.3.1.6	Vivumishi virejeshi vya Ks na Ek.....	69
2.3.2.0	Viwakilishi vya Ks na Ek.....	69
2.3.2.1	Viwakilishi nafsi vya Ks na Ek.....	69
2.3.3.0	Hitimisho.....	72
	Tanbihi.....	73

SURA YA TATU

3.0.0	Utangulizi.....	74
3.1.0	Aina ya vitenzi katika Ks na Ek.....	74
3.1.1	Vitenzi vikuu na vitenzi visaidizi vya Ks na Ek.....	75
3.1.2	Vitenzi vielekezi na visoelekezi vya Ks na Ek.....	78
3.1.3	Vitenzi vishirikishi vya Ks na Ek.....	80
3.1.4	Vitenzi visoukomo katika Ks na Ek.....	82
3.2.0	Mofolojia ya vitenzi vya Ks na Ek.....	84
3.2.1.0	Uambishaji wa vitenzi vya Ks na Ek.....	85
3.2.1.1	Viambishi vya kukanusha vya Ks na Ek.....	86
3.2.1.2	Viambishi vya kiima vya Ks na Ek.....	89
3.2.1.3	Viambishi vya njeo na hali vya Ks na Ek.....	92
3.2.1.4	Viambishi jirejee vya Ks na Ek.....	102
3.2.1.5	Viambishi vya urejeshi katika Ks na Ek.....	103
3.2.1.6	Viambishi yambwa katika Ks na Ek.....	104
3.2.1.7	Viambishi vya vitenzi visoukomo.....	105
3.2.1.8	Viambishi vya mwisho.....	106

3.2.1.9	Uamilifu wa toni katika Ek.....	110
3.2.2.0	Unyambuaji wa vitenzi vya Ks na Ek.....	111
3.2.2.1	Kauli ya kutendea.....	113
3.2.2.2	Kauli ya kutendwa.....	115
3.2.2.3	Kauli ya kutendesha.....	117
3.2.2.4	Kauli ya kutendana.....	119
3.2.2.5	Kauli ya kutendua.....	121
3.2.2.6	Kauli ya kutendeka.....	122
3.2.2.7	Kauli ya kutendatenda.....	123
3.2.2.8	Kauli ya kudumisha.....	124
3.2.3.0	Kitenzi na uminimalisti.....	125
3.2.4	Hitimisho.....	126
	Tanbihi.....	127

SURA YA NNE

4.0.0	Utangulizi.....	128
4.1.0	Muundo wa KT cha Ks na Ek.....	129
4.1.1.0	KT na vielezi katika Ks na Ek.....	129
4.1.1.1	Vielezi vya wakati.....	129
4.1.1.2	Vielezi vya mahali.....	130
4.1.1.3	Vielezi vya kiasi.....	131
4.1.1.4	Vielezi vya namna.....	132
4.1.2.0	Vihusishi katika Ks na Ek.....	135
4.1.3.0	Vipashio na Muundo wa KT cha Ks na Ek.....	137
4.2.0	Mtazamo wa uminimalisti na KT.....	146
4.2.1	Nadharia ya kukagua sifa.....	150
4.2.2	Usogezi na ukaguzi wa KT.....	157
4.2.3.0	Uchanganuzi wa KT kwa kutumia kanuni ya kukagua sifa..	159
4.2.3.1	Ukaguzi wa sifa katika KT cha Ks na Ek.....	160
4.2.3.2	KT katika kauli ya kutenda kiulinganishi.....	160

4.2.3.3	KT katika kauli ya kutendwa kiulinganishi.....	162
4.2.3.4	KT katika kauli ya kutendea kiulinganishi.....	166
4.2.3.5	KT katika kauli ya kutendesha kiulinganishi.....	168
4.2.4	KT jirejee katika Ks na Ek.....	169
4.2.5	KT katika hali yakinishi na kukanusha.....	171
4.2.6	Njeo na hali.....	172
4.2.7	KT kinachotumia vitenzi visaidizi.....	174
4.2.8	KT kinachotumia vitenzi vishirikishi.....	176
4.2.9	KT cha maswali.....	178
4.3.0	Hitimisho.....	180
	Tanbihi.....	181

SURA YA TANO

5.0	Hitimisho.....	182
5.2.	Mapendekezo	183
	Marejeleo.....	184
	Tafsiri za dhana mbalimbali za uminimalisti.....	188
	Ramani ya wilaya za Kisii.....	190

TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabarukia mume wangu mpendwa Elijah Oichoe ambaye kwa uvumilivu mwingi alishirikiana nami bega kwa bega kwa kugharamia masomo yangu kwa vyovyote.

Vile siwezi kumsahau mamangu marehemu Esther ambaye tangu utotoni mwangu alinihimiza kusoma hadi kiwango cha juu zaidi. Wazia wake hata baada ya kifo ulijirudia maskioni na rohani mwangu.

SHUKRANI

Kwa hakika mtu ni watu, kila binadamu anahitaji binadamu mwingine ili ukamilifu uweze kutokea katika maisha haya kwa lile atendalo. Ndio sababu siwezi kuwa mdeni wa yeyote awaye, ambaye aliweza kuchangia kwa hili na lile kufanikisha kazi yangu.

Kwanza natoa shukrani za dhati kwa wasimamizi ambao wakati wote walijitolea kunipa msaada wa mashauri si haba. Hawa hawakuchoka kwa kufanyia kazi yangu ya tasnifu marekebisho mara kwa mara. Mungu awape mema siku zote kwa bidii yenu ya kufanikisha masomo yangu na kwa misaada ya vitabu na makala mbalimbali. Namshukuru Dkt Schroeder zaidi kwa kuchukua muda wake, mara moja kwa juma kutufundisha nadharia ya uminimalisti kwa kujitolea na mwanzangu Rukiya. Mbali na kutufunza, tulimsumbua mara kwa mara kumwuliza maswali ya kupata uhakikisho, naye aliitikia kilio chetu na alitusaida vitabu mbalimbali.

Nawashukuru Dkt Kinene Wa Mutiso, Prof. Kithaka Wa Mberia na Prof. Okoth Okombo kwa mawaidha, makala, vitabu na miongozo mbalimbali kuhusu usomi wangu. Ni kupitia kwa kujitolea kwenu kwa moyo mkunjufu niliweza kuwasha moto kwani kinga na kinga ndipo moto uwakapo.

Shukrani pia ziwaendee wahadhiri wangu wote ambao walihudhuria mihadhara na kuhakikisha tumemaliza kwa muda unaofaa; Dkt Tom Olali, Dkt Mbatiah, Dkt. Buregeya, Bi Margaret Njuguna, Bi. Mwaliwa. Siwezi kuwasahau kamwe wahadhiri ambao pia walinisaidia kwa njia moja au nyingine kama Bw. Mogambi, Dkt Mwiliki wa Chuo Kikuu cha Kenyatta, Dkt. Habwe wa Kikuyu na Bw.Mungania.

Wanafunzi tuliokuwa tukiogelea pamoja katika bahari hii walikuwa wa manufaa makubwa kwa ufanisi wangu. Hawa walikuwa wanafunzi wa kike nane na wa kiume nane, ambao ni Rukiya Harith, Assumpta Matei Mulila, Mediatrix Rapando, Lilian Nkonge, Frida Kaviti, Veronica Maina, Eddah Wanja, Daniel Theuri, Kyalo, Mungai Paul, Mungai Julius, Were, Wepoh Wesah, Nyabunga na mzee wa mashauri wa ajabu Njiiru wote nimewaweka katika akiba ya roho yangu kwa jinsi tulivyoimizana kwa dhati. Hususani Assumpta, siwezi kukusahau kwa mapenzi na mengi uliyonisabilia.

Milka Muthoni Maina ni mtu wa pekee sana kwangu. Alichukua muda wake kuchapa kazi hii mara kwa mara, hata katika kurudiarudia ilipohitajika. Alijitoa mhanga kuchapa kazi hii sura kwa sura kwa moyo mkunjufu bila kuchoka wa kulalama.

Mungu ndiye mweza yote, kwa hiyo siwezi kumwacha kwani alinipa afya njema, uhai na akili za kufanya kazi hii. Pia, namshukuru Mungu kwa mume wangu aliyestahimili upweke, wakati mwingi akiwa ananitemikia, kuona nimefanikiwa kwa kazi hii. Ndugu zangu siwezi kuwasahau kwa mahimizo yenu ya kila mara. Hawa na wengine Mungu awabariki sana. Singeweza kuwataja nyote kwa msaada mlionipa mbalimbali.

Nashukuru pia chuo cha Nairiobi kwa kuiteua kwa masomo haya, mmeifungua milango mipya maishani mwangu.

**MSHABAHA KATI YA AKIKI NA OTHOGRAFIA YA KS NA EK
KONSONANTI**

AKIKI	OTHOGRAFIA YA KS	OTHOGRAFIA YA EK.
β	-	β b
tʃ	CH ch	CH ch
d	D d	-
nd	ND nd	ND nd
j	Jj	-
ɣ	G g	G g
k	K k	K k
l	L l	-
m	M m	M m
mb	MB mb	MB mb
n	N n	N n
ɲ	Ny ny	Ny ny
ŋ	NG' ng'	NG' ng'
ŋg	Ng ng	NG ng
nt	-	NT Nt
ns	-	NS ns
nk	-	NK nk
nʃ	NCH nch	NCH nch
P	P p	-
r	R r	-
ɾ	-	R r
s	S s	S s
ʃ	SH sh	-
θ	DH dh	-
θ	TH th	-
t	T t	T t

w	W w
j	Y y
f	F f
v	V v
x	KH kh

W w

Y y

- -

- -

- -

VOKALI

AKIKI

OTHOGRAFIA YA

OTHOGRAFIA YA EK

KS

a	Aa	A a
e	E e	E e
E	E e	E e
i	I i	I i
o	O o	O o
u	U u	U u
a:	A A aa	AA aa
e: /ε:	EE ee	EE ee
i:	II ii	II ii
o: /ɔ:	OO oo	OO oo
u:	UU uu	UU uu

MUHTASARI

Kazi hii ni jaribio la kutafiti kiulinganishi kirai tenzi cha lugha ya Ekegusii na Kiswahili sanifu, kwa kutumia nadharia ya uminimalisti. Tumeshughulikia kirai tenzi kimuundo na kiupatanishi kwa kutumia kanuni ya kukagua sifa ya uminimalisti.

Kwa muhtasari tumepanga kazi hii katika sura tano. Sura ya kwanza tumeshughulikia utangulizi wa mada yetu kwa kueleza kirai tenzi ni nini, tumetoa kwa ufupi utangulizi wa lugha hizi mbili. Pia, tumeeleza juu ya tatizo la utafiti, nadharia tete, madhumuni ya somo hili, umuhimu wa utafiti huu, msingi wa nadharia yetu, udurusu wa kazi mbalimbali kuhusu mada yetu na njia za utafiti mbalimbali.

Katika sura ya tatu tumeweka msingi wa kirai tenzi kwa kuangalia vipashio vyake. Tumechunguza makundi ya nomino kimofolojia na kisintaksia katika sura ya pili. Sura ya tatu, tumeangalia muundo wa kitenzi kimofolojia kwa kutazama uambishaji na unyambuaji wake. Vipashio vya kirai tenzi tumevichambua kimuundo katika sura ya nne. Katika sura hiyo pia tumetoa uchanganuzi wa kirai tenzi kwa kutumia kanuni ya kukagua sifa ya uminimalisti. Sura ya sita tumetoa hitimisho na mapendekezo yetu kuhusu kazi hii. Tuligundua kuwa nadharia hii inafanya kazi katika lugha hizi, ingawa zinatofautiana kimuundo na kufanana pia.

ORODHA YA VIFUPISHO NA ISHARA

AKIKI	-	Alfabeti ya Kifonetiki ya Kimataifa.
a	-	Athari ya kile kilichohamishwa
ak	-	Athari Kiima.
AN	-	Kauli ya kutendana
at	-	Athari kitenzi
ay	-	Athari yambwa.
E	-	Kielezi
H	-	Kihusishi
HAL	-	Hali
IA	-	Kauli ya kutendea
IW	-	Kauli ya kutendewa
ESH	-	Kauli ya kutendesha
KAN	-	Ukanusho
Kb	-	Kiambishi (viambishi.)
KE	-	Kirai elezi
KH	-	Kirai kihusishi
khj	-	Kama hapo juu
KIP	-	Kiambishi kipatanishi
KIY	-	Kiambishi cha uyakinishi
KN	-	Kirai Nomino
KR	-	Kirai rejeshi.
KT	-	Kirai Tenzi
KUK	-	Kanuni ya ufafanuzi wa kina.
KUP _K	-	Kirai upatanishi kiima
KUP _Y	-	Kirai cha upatanisho Yambwa
KU	-	Kitenzi kisoukomo
KV	-	Kirai Kivumishi
Kw	-	Kiwakilishi
N	-	Nomino
NI	-	Njeo
Nw	-	Na wengine
n.k	-	Na kadhalika
O	-	Kionyeshi
SB	-	Sarufi bia

SPE	-	Spesifaya
SWAL	-	Swali
SZGM	-	Sarufi Zalishi Geuza Maumbo
T	-	Kitenzi
T _s	-	Kitenzi kisaidizi
Tsh	-	Kitenzi kishirikishi
T.Y	-	Tafsiri yetu
U	-	Kiunganishi
UF	-	Umbo Kifonetiki
UM	-	Umbo mantiki
UP	-	Upatanisho
UPk	-	Upatanisho Kiima
UPy	-	Upatanisho Yambwa
W	-	Kauli ya kutendwa
wkt	-	Wakati
V	-	Kivumishi
Y	-	Yambwa
Ø	-	Mofimu kapa
*	-	Si sawa
()	-	Tafsiri ya Kiswahili sanifu
{ }	-	Mipaka ya mofimu
//	-	Mipaka ya kifonolojia
'	-	Alama ya mpumuo
^	-	Sauti inayotamkiwa menoni
→	-	Mabadiliko

SURA YA KWANZA

1.0.0 Utangulizi

Lugha zilizoshughulikiwa katika utafiti huu ni Ekegusii ikilinganishwa na lugha ya Kiswahili sanifu. Hizi ni lugha za nasaba moja (za Kibantu), kwa hiyo tunatarajia kufanana kwa kiasi fulani kimuundo na kiupatanishi. Pia, kwa kuwa ni lugha ambazo zimetengana kwa muda mrefu, na zinapatikana katika mazingira mbalimbali ya kijiografia, tunakusudia kukumbana na tofauti kati ya lugha hizi vilevile. Hebu basi tuweze kupata maelezo mafupi ya kimsingi kuhusu Kirai Tenzi (KT).

KT kina tafsiri mbalimbali kuambatana na nadharia mbalimbali. Kirai ni mpangilio wa maneno ambao huwa katika kategoria fulani. Kulingana na wanasarufi wa miundo virai, kuna mawanda tano ya virai ambayo ni;

- (i) Kirai Nomino (KN)
- (ii) Kirai Tenzi (KT)
- (iii) Kirai Kivumishi (KV)
- (iv) Kirai Kielezi (KE)
- (v) Kirai Kihusishi (KH)

KT huwa ni kirai mwenza cha KN katika sentensi sahili ya Ks na Ek. Mara nyingi KT kinaweza kubeba KN. Kimaana, KT kulingana na wanamapokeo ni kundi la vitenzi ambalo lina uamilifu sawa kisintaksia kama kitenzi kimoja. Kitenzi kimoja huwa ni kisaidizi na kingine huwa ni kikuu (cha kileksika) mfano

1. Ks. A-na-weza ku-imba vizuri.

Ek. Naβo a-ko-nyara gotera βuya.

Ts kip. Nafsi 3 umoja – kb hali kuendelea – Ts weza kb. Kiso – imba – kiishio vizuri.

Wanasarufi zalishi wanakiona KT kuwa kipana zaidi kuliko wanamapokeo. Kwao, KT ni sehemu yote ya kiarifu ya sentensi. Miundo virai inadai kuwa KT ni sehemu yote ya kiarifu ya sentensi. Kwa mfano,


2. Ks. Amina a-me-enda sokoni

Ek. Amina o-ch-ir-e e-chiro.

Amina kip. Nafsi 3 umoja – mzizi T. enda- hali timilifu - kiishio kb ngeli 9 – sokoni.

Sehemu ya ‘ameenda sokoni (ochiire echiro)’ ndio KTambayo inabeba kitenzi ‘ameenda (ochiire)’ na nomino (N) ‘sokoni (echiuro)’ ambayo ina uamilifu wa kielezi. KT kwa hiyo, ni kundi la maneno ambalo lina T kama neno kuu.

Nadharia ya uminimalisti, inaona KT tofauti. KT ni sentensi sahili ambayo ina spesifaya, T na vipashio vingine. Kipashio kikuu kuambatana na nadharia hii, katika KT, ni T. Kwa hiyo tutashughulikia KT kama sentensi sahili ambayo inaweza kuwa na kitenzi kama neno kuu na vipashio vingine kama ifuatavyo:



Sheria hii haimanishi kuwa KT sharti kina vipashio hivyo vyote, bali kinaweza kujengeka kwa kimojawapo au zaidi ya vipashio hivyo. Katika lugha ya Ks na Ek, KT kinaweza kuwa sentensi sahili bila spesifaya ya kiima. Kwa hiyo, tumejaribu kuonyesha kupitia utafiti huu KT kilicho na spesifaya na kile hakina spesifaya kwa nia ya kukagua mashiko ya nadharia hii ya uminimalisti katika lugha ya Ks na Ek.

1.01 Lugha Ya Ekegusii

Hii ni mojawapo ya lugha za Kibantu inayozungumzwa Magharibi mwa Kenya na watu wanaoitwa Wakisii (Abagusii kama wanavyojiita). Wabantu wengine wanaopatikana Magharibi mwa Kenya ni Waluhya, Wakuria (Tende) na Wasuba.

Wakisii wanapatikana katika mkoa wa Nyanza ambapo wanakaa katika wilaya tatu; Nyamira, Kisii ya kati na Kisii ya Kusini (Gucha). Wakisii wanapakana na wazungumzaji wa lugha za kinailoti ambao ni Wajaluo, Wamaasai na Wakipisigisi.

Prof. Guthrie (1971) aliweza kuainisha lugha za Kibantu katika makundi mbalimbali ambapo lugha ya Ekegusii aliiweka katika ukanda¹ wa E, kundi la 40, nambari ya E42. Ekegusii kinakaribiana na lugha zingine kama Kikuria 43 na lugha ya Kimaragoli E41. Ni dhahiri kuwa lugha hizi zinakaribiana sana anavyoeleza Ochieng.²

Lugha ya Ekegusii ambayo tunaichukulia kuwa sanifu ni ile inayotumiwa katika mawasiliano na inatumiwa katika utangazaji kutoka idhaa ya KBC Kisumu, imetumiwa kuandika vitabu na hadithi za watoto na Biblia, na inafunzwa katika shule za msingi kama somo la lugha ya mama (darasa la kwanza hadi la tatu).

1.0.1 Lugha Ya Kiswahili Sanifu

Kiswahili ni lugha mojawapo ya lugha za Kibantu³ inayozungumzwa Afrika ya mashariki na sehemu za Afrika ya kati. Myachina (1981:2) anasema kuwa 'Kiswahili ni neno la kinasaba ambalo hutumiwa kurejelea lahaja zaidi ya ishirini zinazotumiwa katika kuwasiliana. Lahaja hizo amezigawanya katika makundi matatu makuu;

- 1) Lahaja za Zanzibar ambazo zimejumuisha Kimrima Kingao, Kihadimu, Kitumbatu na kadhalika.
- 2) Lahaja za kisiwa cha Mombasa ambazo ni Kimvita, Kivumba na kadhalika
- 3) Lahaja za kisiwa cha Lamu kama Kisiu, Kiamu, Kitikuu na kadhalika

Pia alitaja lahaja zingine kama Kingwana inayotumika Zairi, Kingozi, Kingazija na Chimiini zilizotumiwa sana katika uandishi wa tenzi.

Lahaja ya hayo, lahaja tunayoishughulikia ni ile ya Kiswahili Sanifu. Kiswahili chini ya utawala wa mkoloni kilianza kusanifishwa kwa malengo ya kutaka lugha ya kutumia kuwafundisha Waafrika shuleni. Lahaja ya Kiunguja ilichaguliwa kutumiwa kama mizani ya kukisanifisha Kiswahili na katika mwaka wa 1930 usanifishaji ulianza. Baadaye, kadiri usanifishaji ulivyoendelea, orthografia iliboreshwa, kamusi sanifu ikaandikwa na vitabu vingine kwa Kiswahili sanifu.

Kufikia sasa, Kiswahili Sanifu (kuanzia sasa na kuendelea Ks) kinachukua nafasi ya kwanza kati ya lugha za Kibantu, jinsi kinavyotumiwa katika mawasiliano nje na ndani ya Afrika⁵

1.0.2 Somo La Utafiti

Utafiti huu unadhamiria kuchambua kiulinganishi muundo na upatanishi wa Kirai Tenzi (KT) kwa kutumia nadharia ya Uminimalisti. Tumechunguza KT katika lugha za Ek na Ks huku tukifafanua jinsi muundo na upatanishi wa kisarufi unavyojitokeza katika KT kwa kutumia nadharia ya uminimalisti.

Nadharia ya uminimalisti iliasisiwa na Chomsky (1993, 1995) kushughulikia Sarufi bia na inaongozwa na kanuni ya kukagua sifa za viambajengo. Katika kanuni hii, inadaiwa kuwa kila mofimu huwa na kichwa chake katika kifundo ili kuonyesha uamilifu wa mofimu hiyo na mabadiliko yake. Kwa mfano; mofimu ya upatanishi wa kiima (UPk), mofimu ya upatanishi wa Yambwa (UPy), Mofimu ya Njeo (NJ) na kadhalika. Mofimu hizi huchukuliwa kama kundi la sifa za viambajengo vinavyozungumzia jinsi, idadi na nafsi, ndio sababu nadharia hii inadai kuwa KT hubeba habari zote katika sentensi kwa kuonyesha sifa za viambajengo ambazo huleta upatanishi kati ya vipashio katika sentensi sahili.

KT katika lugha za kibantu huwa na viambishi vingi vinavyowakilisha vipashio mbalimbali. Lugha ya Ek na Ks huwa ni lugha ambishibainishi anavyotubainishia Johnstone (1919:18-20) anapotoa sifa za jumla kuhusu lugha za Kibantu.

“Ni lugha ambishi kimuundo, maana ya mzizi wa neno hubainika na kupanuliwa kwa kuongezewa viambishi awali na viambishi tamati kwa mzizi kuunda neno kisintaksia, lakini hakuna viambishi kati.” (TY)

Kwa mfano katika lugha ya Ek.

A - ka - mo - it - a

(Alimpiga)

KT hiki katika Ek kina kiambishi {a-} kinachosimamia kiima na upatanishi wa nomino na kitenzi; {-ka-} ni njeo ya wakati uliopita {-mo-} ni mofimu ya mtendwa yaani yambwa na kuna mzizi wa kitenzi {-it-} na mofimu ya mwisho {-a}. Je, viambajengo hivi vimetoa habari zote muhimu ambazo zingebewa na sentensi? Ni maswali kama haya kazi yetu inashughulikia kujibu. Swala kuu ni kwamba, ni sehemu gani basi katika KT inayohusika na upatanishi katika lugha ya Ekegusii na Kiswahili Sanifu?

Tumejaribu tuwezavyo kulinganisha vipashio vya KT kimuundo katika lugha hizi mbili, kwa mfano vipashio kama nomino, vielezi, viwakilishi huku tukiangalia uhusiano wa kitenzi na vipashio hivyo kikamilifu. Pia tumelinganisha KT cha lugha hizi kimofosintaksia hasa kwa kuchunguza upatanisho wake kisarufi.

1.2.0 Sababu Za Kulichagua Somo

- i. Sababu kuu ya kulichagua somo hili ni kulinganisha lugha ya Ek na Ks kimofosintaksia. Nadharia ya Uminimalisti inasisitiza jukumu la uundaji wa maneno kuwa na sehemu muhimu katika sarufi. Lugha ambishibainishi kama Ek na Ks zitatusaidia kufikia uamuzi kuhusu mada: hayo kupitia kwa data tuliyokusanya.

- ii. Utafiti huu pia, utakuwa wa manufaa makubwa kwa wanafunzi wa isimu ikiwa nadharia tunayoitumia itapata mashiko katika lugha hizi tunazoshughulikia
- iii. Somo hili litakuwa limefungua milango mipya ya utafiti wa kiisimu kiulinganishi, na kwa hivyo utakuwa mchango mkubwa katika Sarufi bia kwa kutumia nadharia ya uminimalisti.
- iv. Watafiti walioshughulikia kazi za ulinganishi na wengine waliotafiti KN walipendekeza kufanywe utafiti wa KT. Kwa hivyo tumemotishwa na watafiti hao kama Olali (1997: 194).
- v. Kadiri tunavyofahamu, hakuna ulinganishi uliofanywa wa lugha hizi mbili kwa kutumia nadharia ya uminimalisti. Kwa hivyo kuna nafasi inayofaa kujazwa kupitia kwa kutalii kazi yetu.

1.3.0 Nadharia Tete

Ulinganishi wa lugha hizi mbili una matokeo ya aina mbili; kufanana na kutofautiana. Hata hivyo kuna haipotesia zifuatazo;

1. Viambishi vya ukubaliano (upatanishi) katika lugha ya Ekegusii na Kiswahili sanifu, huandamana na viambajengo vingine katika sentensi.
2. KT huwa na upatanishi wa kiima na yambwa ambao hukifanya kujisimamia kama sentensi katika lugha ya Ek na Ks.
3. Usogezi wa viambajengo hufanywa kwa nia ya kupima sifa za viambajengo katika lugha hizi mbili.
4. Uamilifu wa toni katika lugha ya Ek huwa na majukumu ya njeo na hali.
5. Nadharia ya uminimalisti ina mashiko katika lugha ya Ks na Ek

1.4.0 Madhumuni Ya Utafiti

Kwa mujibu wa TUKI (1990:20) upatanishi ni ule uhusiano wa kisintaksia ambapo neno moja hutawala umbo la kimofolojia la neno au maneno mengine katika tungo.

Kwa mintiratu hii, tunadhamiria mambo yafuatayo;

1. Kuchunguza kama nadharia ya uminimalisti ina mashiko yoyote katika lugha ya Ek na Ks.
2. Kuchunguza na kugundua ni viambishi vipi katika KT vinavyohusika na upatanishi kwa kutumia nadharia ya uminimalisti.
3. Kuchunguza uamilifu wa toni katika lugha ya Ek.
4. Kutafiti kama madai kuwa usogezi wa viambajengo katika kiwango cha leksemu hufanywa ili kupima sifa za viambajengo.
5. Kuchunguza muundo wa KT cha lugha hizi mbili unachukua mpangilio gani wa vipashio.

1.5.0 Upeo Na Mipaka Ya Kazi Hii

Katika somo hili, tumelinganisha kimuundo KT cha lugha ya Ek na Ks. Pia kwa kuwa KT huwa na habari ya nomino, tumeshughulikia muundo wa KN. Vilevile, tumeshughulikia upatanishi wa KT. Tumeeleza viambajengo vya KN na KT.

Pia, tutagusia zaidi masuala ya kimofolojia na kisintaksia, kwa sababu ya kazi yetu na nadharia inayohusishwa ili kupata kwa kina upatanishi wa kisarufi. Katika KN, tumejikita katika makundi ya nomino (ngeli) na upatanishi wao. Katika KT pia tumeshughulikia mofimu za upatanishi, njeco, mtendwa (Yambwa) na upatanishi wa vipashio vyake kimuundo.

Kwa kiasi kikubwa tumeshughulikia sentensi sahili (au Kishazi) kujiepusha na masuala mengine yatakayochibuka katika sentensi ambatani na sentensi changamani.

1.6.0 Udurusu Wa Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili

Wataalamu mbalimbali wameweza kushughulikia kazi ya lugha hizi kwa njia mbalimbali na sehemu za sarufi mbalimbali kuhusu lugha hizi (Ek na Ks).

Lugha ya Ekegusii awali ilishughulikiwa na wazungu kama Whiteley, (1960) ambaye alichapisha kazi kuhusu njeo za lugha hii '*The tense system of Gusi*' kazi ya Whiteley ilitusaidia kuelewa njeo ingawa katika kazi yake hakutofautisha njeo na hali. Aidha, kazi yake ilitusaidia kwa kutoa mwangaza kwa kazi yetu kuhusu kitenzi na mofimu zake.

Mtaalamu mwingine ni Guthrie (1948) ambaye alijishughulisha na lugha za Kibantu kwa jumla. Alifanya kazi nzuri ya kuziweka katika makundi lugha za kibantu akitumia mbinu za kisayansi. Kazi yake ya '*The classification of the Bantu languages*' na '*Comparative Bantu V2*' ilitusaidia kujua lugha ya Ek na Ks ziko katika kundi gani na ni lugha zipi zilizokaribiana nazo, ili kuweza kuzisoma kazi zingine za utafiti kuhusu lugha hizi.

Watafiti kama Osinde (1988) hatuwezi kuwaacha nyuma. Katika tasnifu yake ya M.A ameshughulikia mabadiliko ya kimofonolojia ya konsonanti za Ek. Katika sura ya tatu ya tasnifu yake alifanya kipengele cha kimofolojia juu ya nomino na kitenzi. Sehemu hii ilikuwa ya manufaa kwetu kwani mofolojia ya nomino na vitenzi ndio imejenga msingi wa somo letu.

Gesare (1992) katika tasnifu yake ya M.A alijishughulisha na mofolojia ya lugha ya Ekegusii kwa kutumia nadharia ya Umiundo. Kazi yake ilitufaidi sana kwani ilitusaidia kuelewa muundo wa nomino na kitenzi katika lugha hii-Kutokana na kazi yake Gesare (khj) tuliweza kushughulikia KN na KT katika kazi yetu ipasavyo. ingawa hakugusia chochote kuhusu virai na upatanishi, alitusaidia.

Mayaka (2000) aliangalia na kujadili kuhusu muundo wa sentensi katika lugha ya Ekegusii akitumia nadharia ya Sarufi Zalishi Geuza Maumbo (SZGM) katika tasnifu

yake ya B.A. Alitazama sentensi sahili, sentensi ambatani na sentensi changamani. Kazi yake ilikuwa ya manufaa kwetu, hasa ile schemu ya sentensi sahili ambayo ndiyo upeo wa kazi yetu.

Myachina (1981) alichunguza lugha ya Kiswahili kwa upana na kazi yake ina manufaa makubwa kwetu. Kazi ya Myachina na Polome (1967) zilitusaidia kuelewa muundo wa KT cha Kiswahili, hasa waliposhughulikia mofolojia na sintaksia ya Kiswahili Sanifu.

Kazi ya Prof. Abdulaziz (1996) ambayo ni *Transitivity In Swahili*, ilitusaidia kuelewa mifanyiko mbalimbali ya vitenzi kiuamilifu. Tunapozingatia sura ya pili hadi ya mwisho, hii ni kazi ya msaada sana katika mofosintaksia ya KT.

Tasnifu za utafiti mbalimbali na ambazo tuliweza kuzigusia ni kama Manyora (1981) amejishughulisha na KN katika mojawapo ya lugha za Magharibi ya Logooli (Kiluhya) akitumia nadharia ya Umilikifu na Masharti Loogoli ikiwa ni mojawapo ya lugha za Kibantu, ilitusaidia kuelewa muundo wa KN kwani kwa kutumia Umilikitu na Masharti tuliweza kutahamu muundo wa ndani na wa nje wa sentensi sahili. Kwa kuwa nadharia ya uminimalisti imetokana na udhifu wa nadharia ya Umilikifu na Masharti, tuliweza kuelewa mchango wa nadharia yetu zaidi katika sarufi bia.

Tasnifu ya Olali (1997), ilitusaidia sana kuelewa muundo wa KN cha Kiswahili Sanifu kwa kuwa ameshughulikia KN chini ya nadharia ya Eksibaa. Mchango wake wa kinadharia una nafasi kubwa sana katika somo letu, kwani uminimalisti pia hujumuisha nadharia hii ya Eksibaa.

Baya (1993) katika tasnifu yake ya M.A, amechunguza katika kazi yake KN na anatoa viambajengo vya KN cha Kiswahili Sanifu. Pia ametoa sheria za KT akitumia kitenzi kisaidizi. Kazi yake imetusaidia kuelewa kindani nafasi inayochukuliwa na kitenzi kisaidizi (Ts) katika KT.

Tasnifu ya Mogambi (1998) ya MA aliyechunguza upatanishi wa kisarufi katika sintaksia ya Kiswahili ilikuwa ya manufaa sana. Kazi ya Mogambi ilitusaidia kuelewa uamilifu wa viambishi vya upatanishi na pia vipatanishi kisintaksia. Kazi yake ilihusu mofo-sintaksia na ilitufaidi kufahamu zaidi uhusiano uliopo kati ya KN na KT kiupatanishi, ingawaje alitumia nadharia ya Umilikifu na Masharti iliyo kando na yetu.

Tasnifu nyingine zilizofanya kazi za kiulinganishi ni ile ya Gicheru (1999) ambayo imelinganisha KN cha Kiswahili sanifu na cha Kikikuyu cha Kabete. Amefanya ulinganishi wa kimuundo kwa kutumia nadharia ya Sarufi Amilifu kama ilivyoasisiwa na Dik (1978). Kazi yake ilitupatia mwangaza jinsi ya kuweza kushughulika na somo letu la ulinganishi. Upatanisho wa kisarufi katika sura ya nne ni mchango mkubwa ingawa amejikita tu katika KN.

Maringah (1988) amelinganisha ngeli za Kiswahili sanifu na lugha yake huku akitoa upatanishi katika KN na vipashio vyake. Kazi yake ilitusaidia kuwa na mwelekeo mzuri jinsi ya kulinganisha nomino za lugha ya Ek na lugha ya Ks.

Kazi nyingine ya kiulinganishi iliyotusaidia ni ile ya Omusula (1990) ambapo amelinganisha lugha ya Kikabarasi na Kiswahili kwa upande wa mnyambuliko wa vitenzi. Ingawa ameshughulikia sana masuala ya kimofolojia kazi yake ilitufaa sana kwa kuwa Kikabarasi na Ks zikiwa lugha ya Kibantu, tuliweza kujua jinsi ya kunyambua vitenzi vya Ek na Ks ili kuchunguza sifa za kimofosintaksia za KT cha lugha hizi mbili.

1.6.0 Yaliyoandikwa Kuhusu Nadharia Ya Uminimalisti

Fauka ya hayo, mengi yameandikwa kuhusu nadharia ya uminimalisti kama ilivyoasisiwa na Chomsky (1993, 1995). Kazi hii ya Chomsky, imetusaidia kuelewa nadharia hii kwa undani zaidi. Ameleza jinsi nadharia ya uminimalisti ilivyojitokeza ili kusuluhisha matatizo ya Umilikifu na Masharti. Kwa undani, amefafanua

matumizi ya kanuni ya iktisadi na vijikanuni vyake kwa mawanda makubwa yanayotusaidia kuifahamu zaidi.

Schroeder (2002) katika tasnifu yake ya PhD ametalii lugha ya Toposa katika mpangilio wa maneno katika sentensi akitumia nadharia ya kupima sifa za viambajengo ya uminimalisti. Kazi yake imezama kwa kina katika nadharia hii ya uminimalisti na hivyo kutusaidia kuelewa sana. Ameenleza zaidi na kwa uwazi motisha za kimofolojia kwa sintaksia na matumizi yake katika uminimalisti.

Kazi nyingine iliyokuwa na faida kwetu kinadharia, ni ile ya Cook na Newson (1996) ya *Chomsky's Universal Grammar* ambayo kwa mawanda makubwa ilitusaidia kuelewa uhusiano wa nadharia za awali za Chomsky na uminimalisti. Kazi yao wataalamu hawa, ilituwezesha kuelewa kindani nadharia ya uminimalisti na tofauti kati ya uminimalisti na umilikifu na masharti.

Kazi za Radford (1997) zina faida kubwa kwetu hasa tunapomchukulia kuwa amerahisisha maelezo ya Chomsky (1993, 1995) kuhusu nadharia hii. Radford (khj) ameiweka wazi zaidi nadharia ya uminimalisti hasa ile kanuni ya kukagua sifa za viambajengo mbalimbali kimofosintaksia. Kazi ya Radford (1995b) ilitusaidia zaidi kuelewa uundaji wa miundo kuanzia *numerali* hadi kwa *mdhihiriko* wazi. Kazi za Radford zilitusaidia sana kuelewa kindani nadharia ya uminimalisti.

Kazi nyingi zilizorahisisha uelewa wetu katika nadharia, ni zile za Marantz (1995), katika halili ya Gert Webelhuth (1995) ya *Government and Binding Theory and The Minimalist Program: Principles and Parameters in Syntactic Theory*. Lillian Haegman (1981) na Horrocks (1987) ambazo zilituwekea msingi wa nadharia ya Umilikifu na Masharti hadi kwa Uminimalisti. Pia, zilitusaidia kuelewa muundo wa K!1, hasa kazi ya Haegman (1981) na Horrocks. Kwa lugha ya Kiingereza, hali iliyotuwezesha kuainisha mawazo hayo katika lugha zetu. Kazi hizi na zingine za kiutafiti zilitunufaisha sana kwa mapana kuelewa nadharia hii.

1.7.0 Msingi Wa Nadharia

Tangu kuanzishwa kwa sarufi bia, nadharia nyingi zinazochunguza sarufi ya lugha mbalimbali za dunia zimeibuka. Kwa mfano, Chomsky (1957) alianzisha Sarufi Miundo na katika miaka ya sitini akawa na Sarufi Zalishi Geuza Maumbo (SZMG). Nadharia hii ya SZGM ilijishughulisha tu na kitengo cha Kisintaksia, ambapo sintaksia ilichukuliwa kuwa huru na kuweza kuzalisha sentensi nyingi kisarufi kutoka kwa muundo mmoja. Nadharia hii ya SZGM haifai kwa utafiti wetu kwani inajihusisha na ugeuzaji mwingi ambao huweza kutoa maumbo mbalimbali ya virai.

Katika miaka ya sabini, Chomsky alijitokeza na nadharia ya Wastani ambayo baadaye iliduruswa kuwa nadharia ya Wastani Panuzi. Kwa sababu ya matatizo ya nadharia hii kiisimu, ilifungulia milango nadharia ya Umilikifu na Masharti mwaka wa 1981. Nadharia hii ilikuwa na vijinadharia vingine ndani yake ambavyo ni , Eksibaa, Thita, Uhusika, Masharti, Umilikifu, Ufunge na Utawala, (Horrocks 1987: 101).

Nadharia hii haifai kwa kazi yetu kwa sababu mbali mbali . Baadhi yao zikiwa hal! yake ya kutumia maumbo ndani na maumbo nje⁶ ilhali uminimalisti unatumia umbo moja tu la mjumuiko. Mbali na maumbo, nadharia hii ilichunguza vitengo vya kisemantiki, kifonolojia, na kifonetiki kandokando, lakini nadharia ya uminimalisti inachunguza vitengo hivyo kwa pamoja katika mdhihiriko wazi vikiwa maumbo mawili: Umbo Mantiki na Umbo Fonetiki. Matatizo ya Umilikifu na Masharti ya usogezi wa yambwa tendwa na yambwa tendewa, yana suluhishwa na uminimalisti.

Kwa mujibu wa kazi yetu, tumetumia nadharia ya uminimalisti kama ilivyoasisiwa na Chomsky (1993,1995). Tumechagua nadharia hii kwa sababu inaweza

kuchanganua lugha za Kibantu kwa urahisi bila ugumu wowote na pia kwa sababu ya mtazamo wake wa kushughulikia mofolojia na sintaksia pamoja.

1.7.1 Uminimalisti

Hii ndio nadharia ya kisasa iliyoasisiwa na Chomsky kutokana na nadharia ya Umilikifu na Masharti (1981). Uminimalisti huchukulia lugha kuwa na vitengo viwili; Kitengo cha *Leksikoni* na kitengo cha *mifanyiko ya kimkokotoo*. Kitengo cha leksikoni, ndipo leksika zote na sifa za kisarufi za lugha ya mzungumzaji huhifadhiwa. Vipashio vya kisintaksia na kimofolojia huwa vimeunganishwa katika leksikoni. Kabla ya kuchaguliwa kupitia kwa *Numerali* ili kuingia katika kitengo cha mifanyiko ya kimkokotoo kuanza kujenga miundo. Uminimalisti huwa na mifanyiko ya kimkokotoo⁷ ambayo misingi yake ni kusahilisha na kuasilisha mifumo ya lugha, (Radford 1997:6).

Uminimalisti hujumuisha mifanyiko ya kimkokotoo inayoanzia kwa *Leksikoni* hadi kwa uwakilishaji wa kisintaksia. Katika *leksikoni*, leksika zote huingizwa na habari za kimofosintaksia na kisarufi huingizwa na kuhifadhiwa. *Michakato ya Numerali* hufanywa katika *leksikoni* ambapo uchaguzi wa faridi za kimofosintaksia na kileksika hufanywa kuunda uamilifu wa kiufafanuzi. Kisha, huwa kuna *kuungana* kwa elementi hizo ili kuunda muundo wa kisintaksia. *Muungano* ni sehemu ya mifanyiko ya kujenga miundo. Kujenga miundo hujumuisha *kuungana*, *kusogeza*, *masharti ya udogo kabisa ya kuhusisha*, *kucheleweshwa na kanuni ya ubinafsi* (Cook na Newson 1996:325). Ni muhimu kutaja kuwa kujenga miundo katika uminimalisti unafutilia mbali kanuni ya uvurumishaji na muundo wa ndani na ule wa nje wa Umilikifu na Masharti. Hata hivyo, nadharia ya Eksibaa hubaki katika uminimalisti ikiwa na umbo lililorekebishwa. Miundo hujengwa tu inaporuhusiwa na habari za mofosintaksia na leksika za lugha husika na husukumwa na haja. Kwa hivyo, lugha inaweza kutengeneza kielelezo matawi kikiwa na kichwa bila kijalizo ikiwa hakuna kazi ya

kupima uhusika. Pia, nafasi tupu hazikubaliwi katika nadharia ya uminimalisti katika kuunda miundo kwa sababu ya nadharia ya *iktisadi*. Elementi isiyokuwapo huwa haipewi nafasi ya kichwa.

Baada ya kuungana, huwa kuna mfanyiko wa kujenga – miundo na usogezi. Nadharia ya Umilikifu na Masharti ilikuwa na usogezi uliosisitiza juu ya kusogeza. Yaani kusogeza chochote mahali popote kati ya kiwango cha muundo ndani na muundo nje ikisukumwa na fenomena za kisintaksia. Katika nadharia ya Uminimalisti, usogezi wa maneno hufanywa kwa nia ya kukagua sifa ili kutengeneza nafasi katika mifanyiko ya kimuundo. Kwa mfano nafasi ya Spesifaya huwepo ikiwa tu inahusika kama kiambajengo kinachohitaji kukagua uhusika.

Mofolojia ya Nomino (N) hupimwa *sifa za uhusika* katika nafasi ya Sipesifaya inayofaa kama upatanishi wa kiima (UPk) na Upatanishi yambwa (UPy). Mofolojia ya Uambishaji wa Kitenzi (T) hutoa sifa zinazopimwa kwa Kitenzi kama Njeo, Upatanishi wa kiima na upatanishi wa yambwa. Mofimu za unyambuaji wa kitenzi hupimwa katika hali au kauli mbalimbali za unyambuaji, kama hali ya kutendwa, kutendesha, kutendeka, n.k. Kwa vichwa vingine vinavyobuniwa. Ukaguzi hufanywa tu kwa lengo la kuhakikisha kuwa kuna muundo unaostahili na usanifu wa kisarufi wa kirai umefikiwa.


Usogezi huongozwa na kanuni ya iktisadi ambayo hujumuisha kanuni zingine, ambazo ni; *kanuni ya masharti ya udogo kabisa ya kuhusisha, kanuni ya kuchelewesha, kanuni ya ubinafsi na kanuni ya mwisho kufikiwa*. Kanuni ya *iktisadi* inafanya miundo ya kisarufi kuwa midogo zaidi na huisogeza (kwa mfano hudai maumbo madogo zaidi iwezekanavyo. na husogeza viambajengoc vichache iwezekanavyo kwa masafa mafupi). Kanuni ya *masharti ya udogo kabisa* hukubalia tu usogezi hadi kwa nafasi husika; inasema, sharti ifanye *usogezi* “mfupi kabisa” Chomsky (1995_b: 401). Kanuni ya *ubinafsi* na ya *kuchelewesha*

ni vikwazo kwa usogezi kwani huhitaji usogezi wa elementi ikiwa inatosheleza baadhi ya tabia za elementi inayosogezwa.

Kanuni ya *mwisho kufikiwa* hupendekeza *usogezi* mfupi kabisa iwezekanavyo Marantz (1995:354). Katika ujengaji wa miundo kwa kielelezo matawi, matumizi ya *usogezi* na *kuungana* ni muhimu.

Baada ya kujenga – muundo, mifanyiko ya kimkokotoo hudhihirisha wazi habari za leksikoni kwa mijumuiko miwili ambayo ni umbo la kifonetiki (UF) na umbo la kimantiki (UM). Katika viwango hivi viwili sifa za UF huzalisha habari za kifonetiki na UM hutoa habari za kisemantiki pekee yake. Ikiwa majibu ya unyambujaji katika UF yanaridhisha KUPk inasemekana kukutana katika UF.

Vilevile katika UM ikiwa uwakilishi wake wa kisemantiki umeridhisha KUPk uzalishaji huo wa muundo hukutana katika UM. Ikiwa masharti haya hayafikiwi, uzalishaji huo hugongana katika kiwango cha *Mdhihiriko wazi* Kielelezo kifuatacho huonyesha mifanyiko kutoka *leksikoni* hadi kiwango cha *mjumuiko*.



Kielelezo 1. Mifanyiko ya kimkokotoo

Baada ya *mdhihiriko wazi*, sifa za kisemantiki na zile za kifonetiki za faridi hugawanyika na kushughulikiwa kila moja kandokando. *Mdhihiriko wazi* hujitokeza tu baada ya *Numerali* na *Muungano*.

1.7.2 Kanuni ya kukagua sifa.

Kanuni ya kukagua sifa katika uminimalisiti, ndiyo tutakayotumia katika kazi yetu. Hivyo ni muhimu kueleza jinsi inavyojitokeza. Tunachukulia kwanza kuwa kila neno huwa na sifa tatu za kisarufi zifuatazo:

- (a) Sifa za kichwa au neno kuu ambazo hufafanua sifa zote za kisarufi za neno hilo.
- (b) Sifa za kijalizo ambazo hueleza kuhusu vijalizo vipi ambavyo neno kuu laweza kuchukua.
- (c) Sifa za spesifaya ambazo hueleza kuhusu spesifaya inayoweza kuchukuliwa na neno kuu. (Radford 1997b:68) (TY)

Sifa za kijalizo za neno fulani hueleza ni kijalizo cha aina gani ambacho neno hilo lapaswa kuchukua na sifa za spesifaya hueleza sifa za neno ambazo huhitajika neno hilo kuu kuchukua kama kiima chake au yambwa ya neno hilo. Kwa hivyo sifa zinazokaguliwa katika uminimalisti ni zile sifa za kisarufi za kategoria fulani ya kipashio.

Sifa nyingine za kisarufi zinaweza kufafanuliwa na nyingine haziwezi kufafanuliwa. Zile sifa ambazo hazifafanuliwi hufutwa na kubakia sifa zile zinazoweza kufafanuliwa.


Chomsky (1995b) anaeleza kuwa lugha zinaweza kuwa na sifa thabiti au sifa dhaifu za upatanishi. Lugha zenye sifa thabiti zinapokaguliwa hutumia mbinu ya usogezi. Lugha ya Ks na Ek kwa sababu ya sifa zao thabiti za upatanishi kimofolojia, hutumia usogezi kwa kukagua sifa thabiti. Ukaguzi wa sifa na usogezi huruhusiwa kimofolojia au kileksika.

Sifa iliyokaguliwa ndiyo huweza kupitia mkondo wa mifanyiko ya kimkokotoo lakini haitakiwi kuonekana katika umbo mantiki; kama vile sifa za jinsia, idadi, kundi n.k. Sifa zingine baada ya kukaguliwa haziruhusiwi kuingia mifanyiko ya kimkokotoo, kama vile sifa za uhusika (Chomsky 1995b. 178). Ufuatao ni mfano jinsi ya kukagua sifa na usogezi wa vipashio.

Ks. A-li-m-pig-a m-toto

Ek. A -ka -mo -it -a omu -ana

Kip. Nafsi 3 umoja – wkt uliopita – kip. Yambwa – mzizi T piga. –
kiishio kb. Ngeli 1 – mtoto



KT hiki kina vipashio viwili ambavyo ni kitenzi (T) na Nomino (N) yenye uamilifu wa yambwa. T kinatawala T na N. KT hiki hakina spesifaya ya kiima na kwa hiyo haionyeshwi katika kielelezo hiki. Katika kukagua sifa, tunaanzia chini kwa KT kujenga miundo kwenda juu, na vipashio vya kwanza vinakaguliwa kwanza. Nomino yambwa Omwana (mtoto) inasogezwa kutoka kwa N ya T hadi kwa SPE ya KUPy kwa nia ya kukagua sifa za uhusika wake. Inaacha nyuma athari zake baada ya kusogezwa ambazo husaidia kufuatilia mahali ambapo N hiyo imesogezwa (ay). T kimesogezwa toka T ya T hadi kwa UPy kwa nia ya kukagua sifa za uhusika yambwa. Baadaye kinasogezwa hadi kwa NJ ya NJ kwa malengo ya kukagua sifa za njeo, ambazo ni wakati uliopita na hatimaye kutulia kwa Upk ya Upk kwa kukagua sifa za upatanishi kiima. Mahali pote kimepitia, T

kinaacha pia athari yake hapo, ambayo ni nyayo za kuweza kufuatilia jinsi kilivyosogezwa kama inavyoonyeshwa na mistari ya mishale katika kielelezo matawi chetu hapo juu.

1.7.3 Nafasi ya mofolojia katika uminimalisti

Kimapokeo, sarufi iligawanywa katika vikundi viwili tofauti ambavyo vinakaribiana sana kimtalaa. Vikundi hivyo ni mofolojia na sintaksia. Mofolojia hujihusisha na maumbo ya maneno ilhali sintaksia hujihusisha na uchanganuzi wa mpangilio na uhusiano wa vipashio katika virai na sentensi (TUKI 1990). Ikiwa basi hii ndio sarufi, basi kuna umuhimu wa kuchunguza nafasi ya mofolojia katika sarufi badala ya kutegemea tu sintaksia.

Radford (1997:6) anasema kuwa sarufi inapaswa kuwa sahili kama iwezakanavyo, ili kuwe na utendaji kazi wa viambajengo vidogo zaidi vya kisarufi ambavyo huifanya kustahili kama fenomena ya isimu. Viambajengo vidogo zaidi huwa ni sehemu ya mofolojia ya kuunda maneno.

Maneno yote huwa katika kategoria fulani ya kisarufi. Kategoria ni kundi la maelezo yaliyo na sifa zinazofanana ambazo hugawana seti za sifa za kisarufi. Maneno huwa na miundo ya kimofolojia-sintaksia. Ushahidi wa kimofolojia hujitokeza katika mofolojia ya unyambuaji na mofolojia ya uambishaji. Sifa za uambishaji hujumuisha mofimu za uambishaji ambazo hufungamanishwa na nomino au kitenzi kuonyesha uamilifu mbalimbali wa kisarufi wa neno. Sifa za unyambuaji hujumuisha mofimu za unyambuaji ambazo hutumiwa kuunda maneno ya kategoria tofauti kwa kutumia shina la neno (Yule 1996:74-75).

Majukumu ya mofolojia katika uminimalisti ni ya muhimu lakini si kama yalivyokuwa katika Umilikifu na Masharti. Leksikoni sasa si mkusanyiko wa mizizi na mashina ya vitenzi na nomino tu, bali pia hubeba ujumbe unaohusiana na mofolojia ambishi ya kategoria hizi.


Katika Umilikifu na Masharti, mofolojia na sintaksia zilishughulikiwa kama vitengo kandokando lakini katika uminimalisti imekuwa sasa ni mofo-sintaksia ambapo sifa za uambishaji hupewa nomino na vitenzi katika leksikoni, na kategoria zilizoambishwa ndizo huzalishwa tayari zikiwa na mofolojia uhusika (Case Morphology)

Kwa hiyo, usogezi wa kitenzi (T) hauamriwi na uambishaji bali na mifanyiko ya kukagua ambapo sifa dhahania za uambishaji hupimwa kwa usahihi wao katika sintaksia. Katika uminimalisti, mofimu zilizoambishwa na zile zilizonyambuliwa hupewa mahali pa kichwa, kama Njeo (NJ), UPk, UPy, hali sababishi, nakadhalika.

Katika uminimalisti, elementi za kitenzi kama NJ na UPk hushirikishwa na kitenzi katika leksikoni na huitwa sifa – T. Uamilifu wa sifa – T ni kupima sifa za kitenzi ambazo huchaguliwa katika leksikoni kabla ya kuonekana katika UF na UM.

Lugha huweza kuwa na upatanishi ulio thabiti au ulio dhaifu. Upatanisho imara huonekana katika UF ilhali ule dhaifu hauonekani. Kwa mfano, lugha ya Kiingereza ina upatanishi dhaifu ilhali Kiswahili Sanifu na lugha za Kibantu huwa na upatanishi thabiti.

Lugha zilizo na Upatanishi thabiti, hulazimisha kitenzi kusogezwa ili kufutilia mbali kitita cha sifa dhahania kabla ya mdhihiriko wazi. Lugha dhaifu kiupatanishi hazilazimishi usogezi kwani hazina sifa za kukaguliwa. Kielelezo matawi hiki kifuatacho huonyesha muundo wa sentensi katika ukamilifu wake, kama tulivyotafsiri kutoka Chomsky 1995.



UPk na UPy ni kitita cha sifa zinazotofautisha upatanisho kati ya kiima na yambwa, sifa hizo ni jinsia, idadi na nafsi. Nadharia ya kukagua sifa iliweza kutatua tatizo la yambwa – (yambwa tendwa na yambwa tendewa) lilokuwa katika nadharia ya Umilikifu na Masharti. Lugha zilizo na vitenzi vinavyonyambuliwa kwa upana zaidi, kama za Kibantu, zinaweza kuundiwa vichwa katika nafasi za kielelezo matawi ili kuruhusu ukaguzi wa sifa na usogezi kutekelezwa.

L.8.0 Njia Za Utafiti

Utafiti wetu tuliufanya kwa kudurusu vitabu, majalida na majuzuu mbalimbali maktabani kwa mujibu wa kukusanya data. Tuliweza kupitia vitabu vinavyohusu nadharia yetu, ili kuelewa jinsi ya kuitumia katika kazi hii.

Pia tulisoma kazi mbalimbali za utafiti ili kuhakikisha kuwa tumeelewa mada yetu sahihi, ili tuweze kuchuja mawazo mbalimbali kwa kuyalinganisha na kulinganua ili tupate yatakayokuwa ya msaada kwetu, na tujue palipo pengo la kujazwa kupitia kazi yetu.

Isitoshe, tulitumia tajiriba yetu kuhusu lugha ya Ek. Hata hivyo, tuliwahoji na kurekodi data kutoka kwa wasemaji wengine wa lugha hii, kwa kutumia hojaji.

Na zaidi, tuliwahoji wataalamu wa isimu ya Kiswahili na Kiingereza kwa kuwaomba msaada ili kuelewa maswala mbalimbali kuhusu somo letu.

TANBIHI

1. Neno 'Group' tumelitafasiri kuwa 'ukanda' kwa madhumuni ya kutofautisha na 'class' ambalo tumeliita 'kundi'
2. Tazama Ochieng, w. *A short history of the Gusii of Western Kenya*.
3. Tazama Polome, E.C (1967) *Swahili Language Handbook* u.k. 13.
4. Tumemnuuu Ohly, R (1977) kutoka kwa Gicheru, D.M. (1999) Ulinganishi wa Muundo wa KN cha Kiswahili Sanifu na Kikuyu cha Kabete. Tasnifu ya M.A. uk 4.
5. Tumetafsiri 'control theory' kama kanuni ya utawala.
6. 'Projection Principle' imetafsiriwa kuwa kanuni ya uvurumishaji.

SURA YA PILI

2.2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tunadhamiria kuchunguza mofolojia ya nomino kwa kuzingatia uambishaji na unyambujaji. Pia, tutashughulikia nomino kisintaksia, kisha tutaangazia muundo wa KN, cha lugha ya Ekegusii (Ek) na Kiswahili sanifu (Ks). Haja yetu kuu katika sura hii, ni kutambua maumbo ya nomino kimofolojia, na upatanishi wake kisintaksia.

Nadharia ya uminimalisti huchukulia kitengo cha mofolojia kuwa sehemu muhimu. Katika sarufi ya lugha yoyote ile, sifa za kimofolojia husaidia kutambua umbo la elementi inayohusika kisarufi. Zaidi, nadharia ya uminimalisti ina kanuni ya kukagua sifa za sarufi kwa kutazama mofimu za maneno. Kwa hiyo, ni muhimu kutazama, ingawa si kwa undani, msingi wa nomino kimofolojia.

Upatanisho wa maneno katika KT hujumuisha nomino zilizo na uamilifu wa kiima, yambwa tendwa na yambwa tendewa. Kwa sababu hii, mahusiano ya ukubaliano katika nomino na kitenzi hudhihirika kupitia kwa nomino au viambishi viwakilishi nomino katika kitenzi. Kwa mfano.

- | | | | |
|-----|------|----|--|
| (1) | (a) | Ks | A-li-m-pig-a, |
| | (b) | Ek | A-ka-mo-it-a (alimpiga) |
| (a) | A- | — | Kiambishi kiwakilishi kiima
(nafsi ya 3) kipatanishi ngeli ya I |
| | li- | — | Kiambishi cha wakati uliopita. |
| | m- | — | Kiambishi kiwakilishi yambwa (kitendewa) |
| | Pig- | — | Mofimu ya mzizi wa kitenzi |
| | a | — | Vokali ya mwisho |
| (b) | A- | — | Kiambishi kiwakilishi kiima
(nafsi ya 3 umoja) ngeli ya I. |

ka-	—	Kiambishi cha wakati uliopita.
mo-	—	Kiambishi kiwakilishi kitendewa (yambwa)
it-	—	Mzizi wa kitenzi
a	—	Vokali ya mwisho

Viambishi {m-} na {-mo} huwakilisha nomino tendewa katika KT katika lugha zote mbili kwa hiyo, kuna manufaa makubwa ya kuchunguza nomino.

Kujenga-miundo katika uminimalisti, huhitaji usogezi wa leksika mbalimbali zikiwemo nomino, kwa nia ya kukagua sifa za uhusika. Huku tukifahamu kuwa, kila kategoria ya kisarufi huwa na uamilifu wake katika sarufi, nomino hukaguliwa aidha kama kitambulishi cha uhusika kiima au kitambulishi cha uhusika yambwa. Kwa sababu hiyo, ni muhimu pia kuangalia nomino katika lugha hizi mbili.

Mofolojia na sintaksia ya lugha ya Ks na Ek kwa jumla huwa na ruwaza sawa kama lugha za Kibantu ambazo ni ambishibainishi. Hizi ni lugha zenye ukwasi mwingi wa kimofolojia kwa kuwa zinaweza kuambishwa na kunyambuliwa. Anavyosema Guthrie (1948:11), ni lugha zenye viambishi awali na zinazoweka majina katika nambari za makundi mbalimbali. Hayo ni makundi yenye mpangilio maalumu wa kuwa katika hali ya umoja na wingi. Viambishi vya umoja na wingi huwa na mkubaliano fulani na nomino tajwa katika makundi hayo mawili. Makundi ya majina ya Kibantu huwa hayana viambishi vya kuonyesha jinsia ya kike au kiume. Mwisho majina hayo huonyesha upatanishi mkubwa na viambajengo vingine hasa vivumishi.

Kwa matilaba ya kazi yetu, tunashughulikia uainishaji wa nomino kimofolojia na kisintaksia ili kufikia madhumuni yetu ya kuangalia KT kimofosintaksia.

2.1.0 Mofolojia ya Nomino

Uanishaji wa nomino za lugha za Kibantu hujikita katika vitengo vya kisemantiki, kimofolojia na kisintaksia. Ingawa baadhi ya sifa za kisarufi za nomino hujitokeza kisemantiki, hatutaingilia kindani sana ngeli kisemantiki. Lakini, ni muhimu kutambua kuwa semantiki ina hadhi muhimu katika sintaksia. Kwa mfano.

(2) a. M-toto yu-le a-me-kuj-a.

b. **Omw-ana o-ria o-chire**

kb.ngeli 1 mtoto kip nafsi 3 umoja – kionyeshi mbali kip nafsi 3
umoja – mzizi T kuja-hali timilifu - kiishio

c. — a-me-kuj-a

d. — **o-chire.**

Kip nafsi 3 umoja – mzizi T kuja – hali timilifu – kiishio.

Mfano wa (2) c na d huonyesha pengo ambalo kisintaksia lahitaji kujazwa na nomino. Ni bayana kuwa jibu la nomino linalohitajika kisemantiki ni lile linalorejelea nomino yenye uhai. Kwa sababu ya vipatanishi vya virai hivyo. Hivyo, semantiki ina majukumu makubwa katika mofu-sintaksia ya lugha za Kibantu.

Kimofolojia, tumetenga nomino katika makundi mawili mapana; nomino ambishwa na nomino nyambuliwa.

2.1.1.0 Uambishaji wa nomino

Uambishaji ni ule utaratibu wa kuweka viambishi kwenye mzizi wa neno ili kulipa maana mahususi¹. Uambishaji huwa haubadili aina ya neno, yaani neno haliwezi kuwa leksemu tofauti na neno la awali². Nomino huambishwa kwa kuwekewa viambishi awali ambavyo hutambulisha makundi ya ngeli. Lugha ya Ks na Ek, nomino huchukua muundo wa viambishi awali na mzizi wa nomino. Ek huwa na visabiki vya viambishi awali kinyume na Ks. Mfano:

Ks

3. /mu + tu/ → [mtu]

Ek

/o + mo + nto/ – [omonto]

Viambishi awali hupatanisha na pia husimamia idadi katika makundi mbali mbali ya ngeli. Viambishi awali huashiria hali ya umoja na wingi, katika nomino, ingawa si ngeli zote zilizo na viambishi vya umoja na wingi wa nomino. Kwa mfano, Ks ngeli 9/10 haina viambishi vya umoja na wingi ilhali Ek ngeli hizi zina umoja na wingi.

Kiswahili sanifu

Ekegusii

(4)	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Tafsiri</u>
(i)	Nyumba	Nyumba	Enyomba	Chinyomba	(nyumba)
(ii)	Ngozi	Ngozi	Eyanga	Chianga	(nguo)
(iii)	Sabuni	Sabuni	Emoti	Chimoti	(fimbo)

Pia, kuna viambishi vya ukubwa na udogo vya nomino ambapo Ks huchukua {Ji-} na {ma-} na Ek huwa na {ri-} na {ma-} katika umoja na wingi, ukubwa. Udogo, Ks huchukua {ki} na {vi-}, umoja na wingi mtawalia, na Ek huchukua {ka- / ga} na {βi} katika umoja na wingi udogo.

Kuna njia nyingi zilizotolewa na wataalamu mbalimbali za kuainisha ngeli za nomino. Hatutajiingiza katika hoja ya mpangilio, kwani itakiuka upeo na mipaka ya kazi yetu. Mpangilio tutakaoufuata ni ule wa nambari na mofimu au viambishi awali alioutumia Meinhof (1932 : 38-39)

Jedwali 1. Mpangilio wa ngeli za Ks.

Ngeli	Viambishi awali	Mifano
1.	Mu-/ m-/mw-	M-tu
2.	wa-	Wa-tu
3.	mu-/m-	m-ti
4.	mi-	mi-ti
5.	Ji-/Ø	ji-cho
6.	ma	ma-cho
7.	ki-/ ch	ki-atu
8.	vi-/ vy	vi-atu
9.	n	ngozi
10.	n	ngozi
11.	u-	Øuso
10a	n-	Ny-uso
11a	u-	u-gonjwa
6a	ma-	ma-gojwa
15	ku-	ku-lima
16	pa-	pa-le
17	ku-	ku-le
18	mu-	m-le

Jedwali 2. Mpangilio wa nomino za ngeli za Ekegusii.

Ngeli	Visabiki vya viambishi awali	Viambishi awali	Mifano	Tafsiri
1.	o-	-mo-	omonto	'mtu'
2.	a-	βa-	aβanto	'watu'
3.	o-	mo-	omote	'mti'
4.	e-	me-	emete	'miti'
5.	e/-Ø	ri-	erino	'jino'
6.	a-	ma-	amaino	'meno'
7.	e-	ge/ke-	egetaβu	'kitabu'
8.	e-	βi-	eβitabu	'vitabu'
9.	e-	n-	enyomba	'nyumba'
10.	chi	n-	chinyomba	'nyumba'
11.	o-	ro-	orobago	'ukuta'
10a.	chi-	n-	chimbago	'kuta'
11b.	o	ko	okogoro	'mguu'
6a.	a-	ma-	amagoro	'miguu'
12.	a-	ka-	akana	'kitoto'
8a.	e-	βi-	eβiana	'vitoto'
14.	o-	βo-	oβonda	'utajiri'
15.	o-	ko-/go-	okorema	'kulima'
16.	a-	aa-	aase	'mahali/pahali'
17.	a-	aa-	aase	'mahali/pahali'
18.	-	ime-	ime	'ndani ya'

Jedwali hii tumeidondoa kutoka kwa Osinde (1988:68-69) lakini tumefanya marekebisho mengi kulingana na uchanganuzi wetu. Kwa mfano, tumcongaza ngeli za 11/10a/, 11a/6a, 8a, na 17. Katika kuzingatia mpangilio wa Meinhof (1948), tuliweza kugundua kuwa majina mengine yanapaswa kupewa makundi hayo, kwani Osinde alikuwa ameyafungia nje bila sababu yoyote.

2.1.2.0 Ufafanuzi Wa Ngeli Hizi Kiulinganishi

Kwa kulinganisha, tutaziweka nomino za ngeli katika makundi ya umoja na wingi pamoja ili kurahisisha uchanganuzi huu kwa kifupi. Mpangilio wa nomino katika makundi ngeli katika lugha hizi yanatofautiana kwa mengi. Kwa upande mmoja, nomino inaweza kupatikana katika Ks katika kundi fulani la ngeli, lakini nomino hiyo katika Ek ipatikane katika kundi tofauti lisilokuwa lile katika Ks. Kwa mfano nomino ‘mguu’ katika Ks hupatikana ngeli ya 3 / 4 , lakini katika Ek hupatikana katika ngeli ya 11b na 6a.

2.1.2.1 Ngeli 1/2

Kisemantiki, ngeli hizi huwa na nomino za watu, kadiri lugha zote za mame – Bantu. Ngeli ya 1 hutambulika katika Ks kwa kiambishi {m-} ambacho kina viambishi vingine vinavyokitambulisha (alomofu) kama {mu-} na {mw-}. Wingi wa ngeli hii ni ngeli ya 2 ambayo mara nyingi huchukua kiambishi {wa-}, ingawa nomino zingine hazichukui viambishi hivi vyote katika umoja na wingi kama; baba, mama, shangazi n.k.

Lugha ya Ek, viambishi vitambulishi vya ngeli hizi huwa vinachukua visabiki hali ambayo haipo katika lugha ya Ks. Ngeli ya 1 Ek huchukua kiambishi {mo} na alomofu zake ni {mu-} na {mw-}, vikitanguliwa na kisabiki kiambishi awali {o-}. Ngeli ya 2 huchukua {βa -} ambayo hutanguliwa na {a-} kuonyesha wingi. Nomino za watu zinazopatikana katika ngeli hizi ni:

	Kiswahili Sanifu		Ekegusii	
6)	<u>Umoja</u>	<u>wingi</u>	<u>umoja</u>	<u>wingi</u>
	m-tu	wa-tu	o-mo-nto	a-βa-nto
	m-sichana	wa-sichana	o-mo-iseke	a-βa-iseke

m-ke	wa-ke	o-mo-kungu	a-βa-kungu
m-toto	wa-toto	o-mu-ana	a-βa-ana

Wataalamu wengi wanaeleza kuwa kitambulishi cha ngeli ya l katika lugha za Kibantu kilikuwa mofimu {mu} ambayo baadaye ilipoteza irabu /u/ na kwingine irabu /u/ ikaimarika kuwa /w/ ambayo ni nusu irabu na nusu konsonanti kwa baadhi ya nomino. Mabadiliko haya ya u→ w/- irabu /a / ni kwa ajili ya kusawazisha matamshi. Lugha ya Ek na Ks zinakubalia mabadiliko hayo.

Hebu tazama mifano.

Kiswahili sanifu

7) /mu+ana/ → [mwana]
/mu+alimu/ → [mwalimu]

Ekegusii

/omu+ana/ → [omwana] (mtoto)
/omu+orokia/ → [omworokia]

Bakari (1982) anaeleza kuwa mofimu {βa} ya wingi ni ile imedhohofika kutokana na {ba-} ya mame-bantu³. Wakisii hawana {ba-} isipokuwa pale imeambatana na nazali /n/ kama ‘mbagenda (wameenda)’.

/n+ βagenda/ → [mbagenda]

Kutokana na mfano huu mabadiliko yanayoonyeshwa ni mawili muhimu;

1. n → m / -β
2. β → b / n -

Kwanza / n / inabadilika na kuwa / m / katika mazingira ya kutangulia / β /.

Pili / β / inabadilika kwa kuimarika na kuwa / b / katika mazingira ya kufuata / n /.

Majina yanayopatikana katika kundi hili ni kama yale yanayoonyesha uhusiano wa kijamii, 8(i), watenda kazi 8(ii), majina ya makabila na ya kuonyesha utaiifa 8(iii), majina yaliyoundwa kutokana na vitenzi na vivumishi 8(iv) na mengine mengi.

Kiswahili sanifu**Ekegusii**

8) (i)	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Tafsiri</u>
	m-jomba	wa-jomba	o-mo-mame	a-βa-mame	(mjomba)
	m-zee	wa-zee	o-mo-gaka	a-βa-gaka	(mzee)
	m-ke	wa-ke	o-mo-kungu	a-βa-kungu	(mke)
	m-zazi	wa-zazi	o-mo-iβori	a-βa-i βori	(Wazazi)
(ii)	m-chungaji	wa-chungaji	o-mo-risia	a-βa-risia	(mchungaji)
	m-somaji	wa-somaji	o-mo-somi	a-βa-somi	(msomi)
	mu-alimu	wa-limu	o-mo-agachi	a-βa-agachi	(mjenzi)
	mu-uguzi	wa-uguzi	o-mo-nyagitari	a-βa-nyagitari	(Daktari)
(iii)	m-kamba	wa-kamba	o-mo-masaai	a-βa-masaai	(Mmasaai)
	m-kisii	wa-kisii	o-mo-meru	a-βa-meru	(Mmeru)
	m-ganda	wa-ganda	o-mo-gikoyo	a-βa-gikoyo	(Mkikuyu)
	m-kenya	wa-kenya	o-mo-samaria	a-βa-samaria	(Msomalia)
(iv)	m-shenzi	wa-shenzi	o-mo-iti	a-βa-iti	(mwuaji)
	m-panzi	wa-panzi	o-mo-teri	a-βa-teri	(mwimbaji)
	mu-imbaji	wa-imbaji	o-mo-iβi	a-βa-iβi	(mwizi)
	m-linzi	wa-linzi	o-mo-rendi	a-βa-rendi	(mlinzi)

Lugha ya Ks ina baadhi ya majina ambayo hayachukui viambishi hivi vya {m-} na {wa}. Aidha, majina hayo hayana wingi au yanachukua wingi wa viambishi vya ngeli tofauti.

- 9) (i) baba, mama, wifa,
(ii) shangazi – mashangazi
(iii) seremala – maseremala
(iv) tabibu – matabibu

Majina ya watu waliotelema katika lugha zote, hayapatikani katika ngeli hizi.

2.1. 2.2 Ngeli ya 3/4

Viambishi vitambulishi vya ngeli ya 3 (umoja) katika lugha hizi mbili vinafanana. Ngeli ya Ks ina {m}, {mu-} na {mw-}, Ek ina mofimu {mo-}, {mu} na {mw-}. Ngeli ya 4 (wingi) hutambuliwa kwa kiambishi {mi} katika Ks na {me} katika Ek. Nomino nyingi katika kundi hili huwa ni majina ya miti na mimea katika lugha hizi mbili kama ilivyo katika 10(i), pia kuna baadhi ya majina ya sehemu za mwili kama katika 10(ii) majina ya vifaa na vyombo 10(iii) na majina ya fenomena za kiasili 10(iv).

Kiswahili Sanifu

Ekegusii

10) (i) <u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Tafsiri</u>
m-ti	mi-ti	o-mo-gomba	emegomba	mgomba
m-che	mi-che	o-mo-te	e-me-te	mti
m-pera	mi-pera	o-mo-si	e-me-si	muwa
m-nanasi	mi-nanasi	o-mu-ogo	e-mi-ogo	mhogo
m-nazi	mi-nazi	o-mu-ongo	e-mi-ongo	malenge
(ii) m-wili	mi-ili	o-mo-beta	e-me-beta	mwili
m-kono	mi-kono	o-mo-kono	e-me-kono	mkono
m-guu	mi-guu	o-mo-twe	e-me-twe	kichwa
m-domo	mi-domo	o-mo-nwa	e-me-nwa	mdomo
(iii) m-keka	mi-keka	o-mo-nyo	e-mi-onyo	chumvi
m-kuki	mi-kuki	o-mo-tego	e-me-tega	mtego
mu-avuli	mi-avuli			
(iv) mu-anga	mi-anga	o-mo-beta	e-me-beta	mwanga
m-to	mi-to	o-mo-tienyi	e-me-tienyi	miezi
m-lima	mi-lima.			

Mbali na Ks, Ek kina majina ya matukio na majanga ya kiasili katika kundi hili ambayo huwa katika kundi tofauti katika Ks, na huchukua viambishi vilevile vya ngeli hii. Angalia mifano ya 11.

Ekegusii

11)(i) <u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Tafsiri</u>
o-mo-rindo	e-me-rindo	mawimbi
o-mo-βosokano	e-me-βosokano	ajali
o-mo-tengecho	e-me-tengecho	zilizala
o-mo-chando	e-me-chando	shida

Ek pia kina majina ya watu wenye ulemavu wa aina fulani katika ngeli hizi. Kwa mfano

11)(ii) <u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Tafsiri</u>
O-mo-tino	e-me-tino	(kiziwi)
O-mo-uko	e-me-uko	(kipofu)

2.1.2.3 Ngeli ya 5/6

Ngeli ya 5 hutambuliwa kwa kiambishi {ji-} katika Ks ingawa mengi ya majina hayana kiambishi hiki. Ek hutumia kiambishi {ri-} katika ngeli hii, ambapo huenda kiambishi hiki kitanguliwe au kisitanguliwe na irabu /e/.

Wingi wa nomino hizi huchukua kiambishi {ma-} katika lugha zote. Kiambishi {ma-} hutumika kijumla kuonyesha ukamilifu au ujumla wa vitu au mambo katika lugha za kibantu⁴, mbali na kutumiwa katika ngeli ya 6.

Nomino katika kundi hili kwa Ks huwa changamani sana kwani lina majina ainati yaliyo ya vitu mbalimbali. Kunao katika Ks na Ek nomino za majina ya sehemu za mwili kama katika 12(i) majina ya sehemu za miti 12(ii), majina ya vitu viowevu na hayana umoja 12(iii), majina ya watu na kazi zao na hali zao za

kimwili au kiakili (hasa waliopunguani katika lugha ya Ekegusii) 12(iv), majina ya vifaa na vyombo vilivyotengenezwa 12(v).

Kiswahili sanifu

Ekegusii

	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Umoja</u>	<u>Wingu</u>	<u>Tafsiri</u>
12)(i)	ji-che	ma-cho	e-ri-so	a-ma-iso	jicho
	go-ti	ma-goti	ri-ru	a-ma-ru	goti
	ji-no	me-no	e-ri-no	a-ma-ino	jino
	be-ga	ma-bega	ri-reko	a-ma-reko	bega
(ii)	Øtunda	ma-tunda	ri-tunda	a-ma-tunda	tunda
	Øshina	ma-shina	ri-tina	a-ma-tina	shina
	Øjani	ma-jani	ri-to	a-ma-to	jani
			;		
(iii)	maji		amache		maji
	mafuta		amaguta		mafuta
	maziwa		ama ßere		maziwa
	damu		amanyinga		damu
	mavi		amaßi		mavi
	machози		amariga		machози
	mavumbi		amaroßa		mavumbi
(iv)	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	
	Øjambazi	ma-jambazi	ri-chara	a-ma-chara	watu wenye akili punguani (bubu)
	Øbubu	ma-bubu	ri-siasia	a-ma-siasia	
	Øhakimu	ma-hakimu	ri-mama	a-ma-mama	

Kiswahili Sanifu		Ekegusii			
12(v)	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Tafsiri</u>
	jiko	meko	ri-βuri	a-ma-βuri	(mwavuli)
	jembe	majembe	ri-timo	a-ma-timo	(mkuki)

Ks mbali na Ek huwa na majina yaliyokopwa kutoka lugha za kigeni katika ngeli hizi. Mifano.

13. (i)	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>
	Øduka	ma-duka
	Øjuma	ma-juma
	Øshamba	ma-shamba

Ks pia ina majina ya dhana za kidhahania katika kundi hili. Dhana hizi hazina umoja bali ni wingi tu. Majina mengi hayana kiambishi cha umoja bali ni wingi tu.

- (ii) kosa –makosa, wazo – mawazo, ua – maua, shauri- mashauri, umbo- maumbo.
- (iii) maisha, maana, mauti, mali n.k.

Mbali na kuonyesha umoja na wingi, viambishi hivi Ks {ji-}, Ek. {ri-} na {ma-} vinatumika kisarufi kuonyesha hali ya ukubwa katika lugha hizo. Mifano.

Kiswahili Sanifu		Ekegusii		
14	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>
	ji-bwa	ma-ji-bwa	ri-sese	a-ma-sese
	ji-tu	ma-ji-tu	ri-mo-nto	a-ma-monto
	ji-zee	ma-ji-zee	ri-gaka	a-ma-gaka

Kiambishi {ji} cha Ks hutumiwa pia katika kuonyesha hali ya udogo zaidi kikitanguliwa na kiambishi {ki-}. Mfano: ki-ji-bwa, ki-ji-tu, ki-ji-toto n.k.

2.1.2.4 Ngeli ya 7/8

Mofimu zinazotambulisha nomino katika ngeli ya 7 katika Ks ni {ki-} na {ke-/ge-} katika Ek. Ngeli ya 8 ambayo ni wingi wa nomino hutambulika kwa mofimu {vi} na {βi-} katika Ks na Ek mtawaliao. Kiambishi {ki-} cha Kiswahili hupitia mabadiliko ya ukaakaishaji ikiwa mzizi wa nomino unaanza na irabu / a,e,i,o,u/ na kuwa / tʃ -/ katika umoja na wingi /vj-/ ili kusawazisha au kurahisisha matamshi⁵ mifano.

15) <u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>
/ki+ombo/ → [tʃombo]	/vi+ombo/ → [vjombo]
/ki+andalua/ → [tʃandalua]	/vi+andalua/ → [vjandalua]
/ki+etezo/ → [tʃetezo]	/vi+etezo/ → [vjetezo]

Kutokana mifano hii tunaona kisheria kuwa;

k → tʃ /-irabu

a
e
i
o
u

Lugha ya Ek haina ukaakashaji wa aina hiyo katika kundi hili la ngeli. Kunao madai kuwa kundi hili huwa na majina ya vitu visivyokuwa na uhai⁶. Madai haya hayana mashiko kwani kuna nomino za watu, majina ya watu wenye ulemavu fulani, majina ya wanyama na ndege katika lugha hizi mbili, kama katika 16(i). Mengi ya majina huwa ni ya vitu, vyombo vya matumizi mbalimbali, hali, mazoea na matukio ya kimaisha kama 16(ii) majina ya schemu za mwili 16 (iii)

Kiswahili Sanifu		Ekegusii		
	<u>Wingi</u>	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Tafsiri</u>
16) (i) <u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Tafsiri</u>
ki-pofu	vi-pofu	e-ge-susu	e- βi-susi	sungura
ki-faru	vi-faru	e-ge-chure	e- βi-chure	swara

	ki-faranga	vi-faranga	e-gi-oto	e-βi-oto	chura
	ch-ura	vy-ura	e-ke-gonkoru	e-βi-gonkuru	kunguru
	ki-wete	vi-wete	e-ge-sogora	e-βi-sogora	kiguru
(ii)	ki-atu	vi-atu	e-ge-koroto	e-βi-koroto	kiatu
	ki-pini	vi-pini	e-ge-chiko	e-βi-chiko	kijiko
	ki-ng'ora	vi-ng'ora	e-ge-kombe	e-βi-kombe	kikombe
	ki-su	vi-su	e-ge-tambaa	e-βi-tambaa	kitambaa
(iii)	ki-sigino	vi-sigino	e-ke-gokoro	e-βi-gokoro	kiwiko
	ki-dole	vi-dole	e-ki-ara	e-βi-ara	kidole
	ki-fundo	vi-fundo	e-ge-chara	e-βi-chara	ukucha

Pia viambishi; {ki-} na {vi-} hutumiwa katika Ks kuonyesha hali ya udogo katika umoja na wingi. Viambishi vya udogo huchukua nafasi ya ngeli ya 12 katika lugha za Kibantu. Mifano hii huonyesha hali ya udogo katika lugha ya Ks.

Ngeli 7

Kibuzi

Kigozi

Kijito

Ngeli 8

Vibuzi

Vigozi

Vijito

2.1.2.5 Ngeli ya 9/10

Majina katika kundi hili katika lugha ya Ks, hayabainiki kuwa na wingi au umoja, bali hutambulishwa kwa kutumia kiambishi {n-}. Kiambishi hiki pia ni kitambulishi cha muundo wa ndani katika lugha ya Ek katika umoja ambapo vekali /e-/ huja towanzoni kabla ya /n-/. Hata hivyo, si majina yote katika lugha hizi yanayoanza na kiambishi {n}, ni baadhi kama ilivyo katika mfano wa 17 (i). Lugha ya Ek, huwa na wingi wa nomino katika ngeli ya 10, ambazo kiambishi cha wingi huwa ni {chi-}.

17) (i) **Kiswahili sanifu****Ekegusii**

	<u>umoja</u>	<u>wingi</u>	<u>Tafsiri</u>
ngozi	e-nyomba	chi-nyomba	nyumba
ngoma	e-nyanya	chi-nyanya	nyanya
nyumba	e-nyange	chi-nyange	baiskeli

Nomino katika kundi hili, lugha ya Ks na Ek, hujumuisha nomino za wanyama (ii), nomino zilizokopwa (iii) nomino za sehemu za mwili (iv) na virembesho na vifaa vingine mbalimbali.

Kiswahili sanifu**Ekegusii**

	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Tafsiri</u>
(ii) ngamia	e-ng'ombe	chi-ombe	ng'ombe
mbuzi	e-mbori	chi-mbori	mbuzi
ng'onda	e-sese	chi-sese	mbwa
nyangumi	e-ngondi	chi-ngondi	kondoo
(iii) Ømeza	e-suguria	chi-suguria	sufuria
Øsabuni	e-redio	chi-redio	radio
Øsufuria	e-ka βati	chi-kabati	kabati
(iv) ndewe	e-mioro	chimioro	pua
Øpua	e-nyigo	chinyigo	figo
Økope	e-ngoro	chi-ngoro	moyo
(v) Øpete	e-yanga	chi-anga	ngue
nguo	e-βangiri	chi-βangiri	bangili
Øzeze	e-ngoβo	chi-ngoβo	nguo
ngoma	e-rumba	chi-rumba	ushanga

Vile vile, majina ya matukio na majanga ya kiasili hupatikana katika kundi hili.

Kiswahili sanifu	Ekegusii		
	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Tafsiri</u>
Njaa	e-ndwari	chi-ndwari	maradhi
Radi	e-nchara	chi-nchara	njaa
	e-toigo	chi-toigo	mazika
	e-nkoḽa	chi-rikoḽa	radi
	o-roche	chi-ndoche	mtoto
	e-mbeo	chi-mbeo	upepo.

2.1.2.6 Ngeli ya 11/10a/6a/11a

Hili ni kundi lenye majina ya nomino ainati ambazo zina uambishi mchanganyiko. Katika Ks, kuna zile nomino ambazo zina kiambishi {u-} katika umoja na wingi ni kupoteza ile /u-/. Pia lugha hii ina nomino ambazo hazina viambishi vya umoja (huwa ni kapa) lakini wingi huchukua {n-} tazama mifano ya 18(ii).

Kiswahili Sanifu

18) (i) <u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	18(ii) <u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>
u-kuta	Økuta	uso	nyuso
u-kucha	Økucha	wembe	nyembe
u-teo	Øteo	waraka	nyaraka
		uzi	nyuzi

Lugha ya Ks, nomino zinazoanza na /u/, na wingi wao huchukua /ɲ/ ambapo /n/ hufuata /u/

/ n / → ɲ / - u

Ni muhimu kutambua kuwa kiyeyushi /w/ hutokana na kuimarika kwa irabu /u-/ katika kupata nomino za ‘wembe’ na ‘waraka’. Hivyo kutokana na uundaji wa viyeyusho, tunachukulia kuwa nomino ‘wembe’ hutokana na /u+embe/ → [wembe].

Lugha ya Ek na Ks, zote zina kundi la 11a/6a ambapo nomino za Ks huambishwa mwanzoni na {u-} katika umoja (ngeli ya 11a) na {ma-} katika wingi (ngeli ya 6a). Ek huchukua {oβo-} katika umoja na {ama-} katika wingi. Mifano ni kama ilivyo katika 18(iii)

Kiswahili Sanifu

Ekegusii

18) (iii)	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Tafsiri</u>
	u-gonjwa	ma-gonjwa	o- βo -sio	a-ma-sio	Uso
	u-gomvi	ma-gomvi	o- βu-embe	a-me-mbe	wembe
	u-lezi	ma-lezi	o- βu-ato	a-ma-to	safina
			o- βo-ngo	a-mo-ngo.	(ubongo)

Ek huwa na nomino zingine ambazo huchukua viambishi vya umoja kuna {oko-/ogo-} na wingi huchukua kile kiambishi cha 6a ambacho ni {ama-}. Nomino hizi hazipatikani katika Ks. Tazama mifano hii ya 18 (iv)

Ekegusii

<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Tafsiri</u>
o-ko-boko	a-ma-βoko	mkono - mikono
o-ko-goro	a-ma-goro	mguu – miguu
o-go-to	a-ma-to	sikio – masikio

2.1.2.7 Ngeli ya 12/8a

Kundi hili lina nomino za lugha ya Ekegusii. Nomino za kuonyesha hali ya udogo katika umoja (ngeli ya 12) na wingi (ngeli, 8a) katika Ek. Lakini katika Ks kundi hili lilijumuishwa katika ngeli ya 7/8 kama tulivyodokeza. Viambishi ambishi katika Ek kwa kundi hili ni {aka-} na {eβi-}. Tazama mifano ifuatayo.

Ekegusii

20)	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Tafsiri</u>
	a-ka-na	c-βi-ana	kitoto - vitoto
	a-ka-βusi	o-βo-βusi	kijipaka -vijipaka
	a-ka-monto	e-βi-monto	kijitu -vijitu
	a-ga-iseke	e-βi-iseke	kijisichana – vijisichana

Lugha ya Ek inapotumia viambishi vya udogo, haimaanishi tu kuwa nomino inayorejelea ni ndogo tu, bali pia inatumika kuonyesha uzuri na ukaribu wa kihusiano wa umri ikiwa msemaji anarejelea watu. Kwa mfano.

E βiana βiane βiachire (vitoto vyangu vimekuja).

Msemaji ni mtu wa umri mkubwa anayehusiana kijamii na wanaorejelewa, na anaonyesha mapenzi yake kwa watoto na wala si madharau au hali ya kudunisha. Aidha, mara nyingi hutumika kuonyesha udogo wa nomino zingine na pia hali ya kudunisha (isokuwa na thamani kubwa). Kwa mfano.

Aka-meza ka-o ka-βunek-ir-e.

Kb ngeli – meza kip ngeli – kb kimilikishi kip – mzizi T vunjika- hali - kiishio
(Kimeza chako kimevunjika.)

Sentensi hii humaanisha ni meza ndogo na mbovu.

2.1.2.8 Ngeli ya 14

Nomino za ngeli hii huwa ni dhahania, na mara nyingi hazina wingi. Lugha ya Ek Osinde (1980) anadai kuwa ngeli hii ina viambishi vya wingi ambavyo ni {ama-} ingawa anasema hivyo, sisi hatukubaliani naye kwani kimazungumzo na kiupatanishi huwa si sahihi. Kwa hiyo, nomino hizi hujitokeza katika ngeli hii katika hali ya umoja tu. Hata hivyo, Ks huwa na nomino dhahania ambazo huwa na wingi na tumeziorodhesha katika makundi yaliyopita. Mifano ya ngeli hii ni:

20)	Kiswahili Sanifu	Ekegusii	
	U-rembo, u-zuri, u-jinga	o- βo-gotu(uzee),	O- βo-noru (unene)
	U-alimu, u-tu, u-nyama n.k.	o- βo-rimo (uongo),	O-βo-taka (umasikini)

Nomino hizi zimeundwa kutokana na vivumishi, vitenzi na baadhi kutokana na nomino zingine.

2.1.2.9 Ngeli ya 15

Nomino katika ngeli hii zimeundwa kutokana na vitenzi, ndio sababu wasanii wengi huziita nomino vitenzi⁷. Wataalamu wengine huziita nomino za vitenzi visoukomo, kwa sababu zimeambishwa mofimu {ku-} ambayo huvifanya vitenzi hivyo kuwa nomino. Nomino hizi huwa na uamilifu mbalimbali kama tutakavyoona katika sura ya tatu. Mofimu ya kunominisha katika Ek ni {oko-/ogo-}, na Ks ni {ku-}, zote hutangulia mzizi wa kitenzi. Nomino hizi hazina wingi wao.

Kiswahili Sanifu

21) (i) <u>Kitenzi</u>	<u>Nomino</u>
lim-a	/ku-lim-a/ — kulima
chez-a	/ku-chez-a/ — kucheza
ib-a	/ku-ib-a/ — kuiba

Ekegusii

(ii) <u>Kitenzi</u>	<u>Nomino</u>	<u>Tafsiri</u>
rem-a	/oko-rema/ - [okorema]	kulima
sek-a	/ogo-seka/ - [ogoseka]	kucheka
tam-a	/0go-tama/- [ogotama]	kutoroka

2.1.2.10 Ngeli ya 16/17/18

Viambishi vya ngeli hizi katika Ks ni {pa-/po-} (ngeli ya 16), {ku/-ko-} (ngeli ya 17) na {mu/mo} (ngeli ya 18). Ni viambishi vinavyoonyesha mahali au pahali. Nomino za kundi hili ni mbili tu; mahali/pahali, na hutumika kulingana na muktadha fulani.

Kiambishi {pa/po} hurejelea mahali maalumu, panapojulikana au panapodhihirika na {mu-/mo-} huonyesha mahali ndani. Viambishi hivi havitumiwi kwa pamoja katika sentensi kwani hupotosha maana kisemantiki, isipokuwa tu pale maana inadhihirika wazi.

Kwa mfano:

Maria alihama hapa, akaenda kule kusikojulikana, mwishowe anaishi mle mjini.

Ekegusii ni tofauti na viambishi hivi. Viambishi vya 16 na 17 hufanana {a-} kwa sababu wazungumzaji, wa lugha hii hutumia vielezi vingine kudhihirisha mahali. Mahali ndani huashiriwa kwa kutumia neno 'ime' (ndani).

22) E-ngiti ya-so-ir-e e-ngoro ime

kb. ngeli 9- nyoka kip. ngeli 9 – mzizi T. ingia – hali timilifu- kiishio kb.ngeli 9 – shimo ndani

(Nyoka ameingia shimo ndani)

Kufikia hapa, tumejaribu kueleza muundo wa nomino, wa lugha hizi mbili. Tumetoa viambishi vya kimofolojia. Jedwali ifuatayo, inaonyesha ufupisho wa maelezo kwa kutoa viambishi awali vya ngeli za nomino za kila lugha hizi mbili.

Kiswahili Sanifu

Ekegusii

Ngeli	Viambishi	Mfano	Viambishi	Mfano	Tafsiri
1	m-/mu-/mw-	Mtu	Omo-	Omonto	Mtu
2	wa	Watu	A-βa-	Aβanto	Watu
3	m-/mu-/mw-	Mti	o-mo-	Omote	Mti
4	mi-	Miti	e-me-	Emete	Miti
5	Ji-/Ø	Yai	ri-	Rigena	Jiwe
6	Ma	Mayai	a-ma-	Amagenā	Mawe
7	Ki	Kizingiti	e-ke-/e-ge-	Egekombe	Kikombe
8	Vi	Vizingiti	e-βi-	Eβikombe	Vikombe
9	N	Nyumba	e-	Enyomba	Nyumba
10	N	Nyumba	chi-	Chinyomba	Nyumba
11	U	Uso	oβo-	Oβosio	Uso
10a/6a	N	Nyuso	a-ma-	Amasio	Nyuso
11a	U	Ulezi	o-βo-	Oβongo	Ubongo
6a	Ma	Malezi	a-mo-	Amongo	Ubongo
11b	-	-	o-ko-/ogo-	Okogoro	Mguu
6a	-	-	a-ma-	Amagoro	Miguu
12	-	-	a-ka	Akana	Kitoto
8a	-	-	e-βi	Eβiana	Vitoto
14	U-	urembo	o-bo-	Oβogotu	Uzee
15	KU-	kulima	o-ko/ogo-	Okorema	Kulima
16	Pa/po	pahali/mahali	aa	Aase	Mahali
17	Ku/Ko	kule/kote	aa	Aase	Mahali
18	Mu/Mo	mle/mote	-	ime	Ndani ya

Kwa jumla, mpangilio huu, unaonyesha kuwa, kunaofauti kati ya mpangilio wa makundi ya ngeli katika lugha ya Ks na Ek. Kwa kutofautiana, makundi ya ngeli za Ek ni mengi kuliko yale ya Ks. Kwa mfano Ks haina kundi la 11b/6a na 12/8a, Ingawa kundi la ngeli la 12/8a, limejumuishwa, katika kundi la 7/8 katika Ks-.

Pili, makundi fulani kwa Ek yana wingi ambapo makundi yayo hayo yana umoja tu katika Ks; kwa mfano kundi la 9/10. Kwingineko pale ambapo Ks kimechukua umoja kiambishi {u}na wingi kiambishi {u-}, Ek huchukua wingi {ma } kama kundi la 11/10a/6a. Pia katika makundi ya mahali/pahali, Ks huwa na viambishi vitatu, iihali Ek kina viambishi viwili. Hata hivyo kwa pakubwa mpangilio wa makundi ya ngeli unafanana.

2.2.0 Unyambuaji Wa Nomino

Nomino zinazoundwa kwa kunyambuliwa ni zile zinazoundwa kutokana na kategoria zingine kama vitenzi, vivumishi na nomino. Nomino nyambuliwa huwa zinapewa viambishi awali vya ngeli na kuongezewa kiambishi tamati cha nomino kwa mzizi wa aidha kitenzi kivumishi au nomino husika⁸. Lugha ya Ks na Ek zina unyambuaji mwingi wa nomino kupitia kwa njia hiyo, lakini tutatoa mifano michache tu, yakuweza kutoa mwelekeo wa unyambuaji wa nomino.

Nomino nyingi zinazonyambuliwa katika lugha ya Ks na Ek hutokana na vitenzi, baadhi hutokana na vivumishi na nomino zingine. Vilevile, nyingi za zile zinazoundwa kwa kunyambuliwa huwa katika kundi la ngeli ya 1/2, 7/8, 14 na 15. Ndiyo kusema kwamba, aidha huonyesha mtu (mtenda, mtendaji, mtendewa nk) kifaa, hali na nomino zisizoukomo. Viambishi tamati vya unominishaji mara nyingi hushirikiana na viambishi awali vya kutambulisha ngeli.

Jedwali 4.

<u>Kiswahili Sanifu</u>			<u>Ekegusii</u>		
1.	<u>Kitenzi</u>	<u>Nomino</u>	<u>Kitenzi</u>	<u>Nomino</u>	<u>Tafsiri</u>
	lewa	<u>mlevi</u>	toerera	<u>oβotoereru</u>	utilivu
	ongoza	<u>uongozi</u>	rosa	<u>oβorosu</u>	uchovu
	cheza	<u>mchezaji</u>	agacha	<u>omwagachi</u>	mjenzi
	shinda	<u>ushindi</u>	rema	<u>oβoremi</u>	ukulima
	hama	<u>mahame</u>	tonga	<u>egetongwa</u>	kiumbe
	iba	<u>kuiba</u>	iβa	<u>okoiβa</u>	kuiba
	tuma	<u>mtume</u>	toma	<u>omotomwa</u>	mtumwa
	ziba	<u>kizibo</u>	aβusa	<u>ekiaβuso</u>	kifagio
	lisha	<u>malisho</u>	igota	<u>omoigoto</u>	shibe
			i		
2.	<u>Kivumishi</u>	<u>Nomino</u>	<u>Kivumishi</u>	<u>Nomino</u>	
	-zito	<u>uzito/mzito</u>	-mwamu	<u>oβomwamu/omomwamu</u>	
	-zuri	<u>uzuri/mzuri</u>	-βuya	<u>oβuya/omuya</u> (mzuri/uzuri)	
	jinga	<u>ujinga/mjinga</u>	-βoβe	<u>oβoβe/omōβe</u> (ubaya/mbaya)	
	-baya	<u>ubaya/mbaya</u>	-riri	<u>oβoriri/omoriri</u> (ujinga/mjinga)	
3.	<u>Nomino</u>	<u>Nomino</u>	<u>Nomino</u>	<u>Nomino</u>	<u>Tafsiri</u>
	Mwanaume	<u>Uanaume</u>	Omosacha	<u>Oβosacha</u>	Uanaume
	Msichana	<u>Usichana</u>	Omomura	<u>Oβomura</u>	Uvulana
	Mtoto	<u>Utoto</u>	Omwana	<u>Oβwana</u>	Utoto

Katika jedwali hii, viambishi vya unyambujaji vimepigwiwa misitari. Viambishi awali huonyesha kundi la ngeli viambishi tamati, ndivyo vilivyonyambuliwa kwa kutoa hali ya unominishaji, huku vikishirikiana na viambishi awali. Kwa kuzingatia mifano hiyo na mingine, viambishi vya uundaji vya inwishi, mara nyingi huwa ni vokali katika lugha zote mbili, isipokuwa baadhi ya nomino katika Kiswahili sanifu ambazo huchukua kiambishi {-ji} na Ek mara nyingine huchukua nusu-irabu {-w-} kama kwa omo-soerwa (mshitakiwa), ege-tongwa (kiumbe).

Lugha ya Ek na Ks zina unyambujaji mwingine ambao ni wa kuunganisha nomino mbili huru pamoja ili kuunda nomino moja changamano. Hebu tazama mifano hii.

Kiswahili Sanifu

23) /mcheza+kamari/ — mchezakamari
 /mwana+maji/ — mwanamaji
 /kipaza + sauti / — kipazasauti

Ekegusii

/omominchori+ imi/ — mominchorimi
 /enda+mwamu/ — endamwamu
 (tumbo + eusi) (wivu)
 /risoni + eng'ombe/ — risoning,ombe
 (mti + ng'ombe) (mti wa kiasili)

Kufikia hapa tumejaribu kuchanganua nomino kimofolojia kwa kuzingatia vipengele vya mofolojia ambishi na mofolojia nyambujaji. Kwa sababu tunadhamiria kuchunguza upatanishi, hebu sasa tuangalie mpangilio wa nomino kisintaksia.

2.3.0 Uainishaji Wa Ngeli Kisintaksia

Schemu hii ya uainishaji ni muhimu kwa sababu utafiti wetu unashughulikia masuala ya kimofolojia na kisintaksia (mofolojia-sintaksia) katika lugha ya Ek na Ks. Kwa kuwa kuna mwingiliano kati ya mofolojia na sintaksia kama vitengo vya lugha, ni muhimu basi kutazama nafasi ya sintaksia katika sarufi ya lugha hizi, hasa katika ile hali ya kupatanisha vipashio mbalimbali. Upatanisho ni mojawapo ya madhumuni yetu, na likiwa suala la kisintaksia, mara nyingi hutegemea mofolojia yake, hasa viambishi.

Kisintaksia, ngeli hugawanyika kwa kuzingatia viambishi vya upatanishi wa kisarufi vinavyoleta mshikamano wa maneno katika tungo⁹. Kapinga (1983:33) ametoa mpangilio wa viambishi kisintaksia kwa lugha ya Ks ambao tunaona kuwa ni muwala kuutumia. Lugha ya Ek, tutatumia mpangilio wetu ulio mwafaka na unaoona na ule wa Kapinga (1983).

Tutatoa ufafanuzi wa makundi ya ngeli kwa pamoja katika umoja na wingi kama yanavyohusiana na vitenzi, kwa sababu kategoria zingine tutatoa upatanishi wao katika sehemu itakayofuata ya vipashio vya KN.

2.2.1 Kundi la ngeli ya 1/2

Viambishi vya lugha ya Ks {M-/Mu-/Mw} umoja na wingi ni {wa-} kimofolojia. Lugha ya Ek viambishi vyake ni {m-/mo-/mu-/mw-} umoja na {- βa} katika wingi. Viambishi vina uhusiano mkubwa kati ya nomino na vipashio vingine kama vivumishi na vitenzi. Upatanishi wa vivumishi huchukua viambishi hivi, kwa mifano.

24) Ks. M-sichana m-zuri.

Ek. **Omo-iske omu-ya.**

Mahusiano ya nomino na kitenzi huchukua viambishi tofauti, ambapo katika Ks huwa ni {a-} na {wa-} umoja na wingi, na Ek huchukua {o-} na {βa-} umoja na wingi. Hebu tazama mifano hii.

25) Ks. (i) M-sichana a-me-rudi.

(ii) Wa-sichana wa-me-rudi.

Ek (i) **Omo-iseke o-iran-ir-e**

Kb ngeli 1 msichana kip nafsi 3 umoja – mzizi T rudi – hali timilifu – kiishio.

(Msichana amerudi.)

(ii) **Aβa-iseke βa-iran-ir-e**

Kb ngeli 2 msichana kip nafsi 3 wingi – mzizi T rudi – hali timilifu – kiishio.

(Wasichana wamerudi.)

Upatanishi kati ya nomino na kitenzi katika lugha ya Ek hubadilika kulingana na wakati hali na nafsi inayohusishwa mbali na Ks ambayo hubakia kuwa {a-} na

{wa-}. Suala hili tutalijadili katika sura ya tatu sehemu ya KT. Kwa sasa tazama mfano huu wa wakati uliopita katika lugha ya Ek.

26) **Omo-iseke n-a-iran-a.**

kb ngeli 1 msichana kiy – kip nafsi 3 umoja- wkt pita – mzizi T rudi - kiishio

(Msichana alirudi.)

Aβa-iseke m-ba-iran-a.

kb ngeli 1 msichana kiy – kip nafsi 3 wingi - wkt pita – mzizi T rudi - kiishio

(Wasichana walirudi.)

Viambishi vipatanishi ni {na-} na {mba-} ambapo $n \rightarrow m/\beta$ ili kurahisisha matamshi kupitia kwa usilimisho wa nazali. Viambishi hivi vya upatanishi vya wakati uliopita vinatofautiana na vile vya hali timilifu na katika wakati ujao, viambishi huwa ni {na-} na {mba-}.

Upatanishi katika Ks ni sawa, uwe wa wanyama, wadudu, ndege au binadamu, ilhali Ek huwa wanyama wadudu, ndege, samaki na viumbe wengine wenye uhai, upatanishi wao ni kama ule wa vitu visivyo na uhai kutegemea ngeli penye nomino hiyo imeanishwa. Kama Mfano.

27) Ks. Mbwa yule amenona.

Ek. **Esee eria yanorire.** (Tafsiri Ks)

Mbwa katika lugha ya Ks amepewa hadhi sawa na binadamu, katika Ek hupewa hadhi sawa na kitu chochote katika kundi la ngeli ya 9/10. Kwa hiyo, Wakisi hawawezi kusema:

*Ese oria onorire.

(Mbwa yule amenona).

Kiambishi kisabiki cha wanyama na viumbe wengine wenye uhai huwa ni {e-} (au bila -e) ambacho hutoa kibali cha nomino hizo kuwa katika kundi la vitu tofauti

na watu huwa ni kiambishi kisabiki {o-}. Hii haimaanishi kuwa hizi ndizo nomino tu huwa na visabiki hivi, bali kuna nomino nyingine nyingi.

2.2.2 Kundi la ngeli ya 3/4

Kisintaksia kundi hili la ngeli huchukua viambishi {u-} na {i-} katika Ks, na {o-} na {ya-} katika Ek, kwa umoja na wingi mifano

28) Ks (i) M-kono wa-ngu u-me-vunjik-a.

(ii) Mi-kono y-angu i-me-vunjik-a.

Ek (i) **Omo-kono o-ne o-βunek-ir-e.**

Kb ngeli 3-mkono kip – kimilikishi kip mzizi T vunja – hali timilifu- kiishio.

(Mkono wangu umevunjika.)

(ii) **Eme-kono y-ane ya-βunek-ire-**

Kb ngeli 5-mikono kip – kimilikishi kip mzizi T vunja – hali timilifu- kiishio.

(Mikono yangu imevunjika.)

Kama tulivyotaja awali, majina ya ulemavu katika Ek yanayochukua ngeli hii, upatanishi wao si kama ule wa Ks, bali hupatanishwa kama miti au mimea. Kwa mfano, omouko (kipofu) – emeuko (vipofu) hutumiwa hivi katika sentensi;

29) Ek **Omo-uko o-gu-r-e inse.**

kb ngeli 3 kipofu kip-mzizi T anguka- hali- kiishio chini.

(Kipofu amanguka chini.)

Eme-uko ya-gu-r-e inse.

kb ngeli 4 vipofu kip-mzizi T anguka- hali- kiishio chini.

(Vipofu wameanguka chini.)

Hasa unaweza kugundua kwamba, ingawa ni binadamu, upatanishi wake ni sawa na ule wa mti.

Omo-te o-gu-r-e.

Kb ngeli 3-mti kip –mzizi T – hali timilifu – kiishio.

(mti umeanguka)

Kuonyesha kuwa Wakisii wanawapa walemavu hadhi sawa na vitu, sawa na lugha zingine za Kibantu kama Kikamba na Kikikuyu isipokuwa Ks.

2.2.3 Kundi la 5/6

Ks huchukua {li-} katika umoja {ya-} katika wingi na Ek huchukua {ri-} katika umoja na {a-} katika wingi. Tazama mifano ifuatayo;

30) Ks. (i) Yai li-li-vunj-ik-a.

(ii) Ma-yai ya-li-vunj-ik-a.

Ek. (iii) Er-iso ria-rwar-ir-e.

Kb ngeli 5 – jicho kip – mzizi T – hali - kiishio

(Jicho limegonjeka)

(iv) Ama-iso a-rwar-ir-e.

Kb ngeli 6 – macho kip – mzizi T – hali - kiishio

(Macho yamegonjeka.)

(v) E-riso n-dirwa-r-e.

Kb ngeli 5 – jicho kip – mzizi T – njco/ kiishio

(Jicho litagonjeka.)

Katika mfano wa (v) wa Ek. Kipatanishi /r/ kinabadilika na kuwa /d/ katika mazingira za kufuatilia /n/

/r → d /n-

/ n + riarwarire / → [ndiarwarire]

Haya ni mabadiliko ya kimofofolojia yanayosababishwa na upatanishi wa wakati katika lugha ya Ek.

2.2.4 Kundi la 7/8.

Mofimu za upatanishi katika lugha ya Ks ni {ki-} na {vi-} katika umoja na wingi.

Ek huchukua mofimu {ki-} na {βi-} katika umoja na wingi vilevile.

Tazama mifano ifuatayo.

31) Ks. (i) Ki-atu hi-ki ki-li-pote-a.

(ii) Vi-atu hi-vi vi-li-pote-a.

Ek (i) **Eke-rato** ke-ria kia-yi-r-e

Kb ngeli 7 kiatu kip – kionyeshi kip mzizi T – hali – kiishio.

(Kiatu kile kimeungua)

(ii) **Eβi-rato** βi-ria βia-yi-r-e

Kb ngeli 8 kiatu kip – kionyeshi kip mzizi T – hali – kiishio.

(Viatu vile vimeungua)

Kama tulivyosema, mabadiliko ya wakati katika kundi hili huwa kama:

Ekerato keria kiayire/ nkeyie nkiayia/ nkiayete.

(Kiatu kile kimeungua / kitaungua/ kiliungua.)

Eβirato βiria βiayire/mbyie/mbyia/mbyiete;

(Viatu vile vimeungua / vitaungua / viliungua / viliungua zamani kidogo)

Hapa katika wingi mfano: /n/ hubadilika kuwa /m/ katika mazingira ya kufuata /β/.

/n/→m/-β.

2.2.5 Kundi La 9/10

Kisintaksia upatanishi kati ya nomino na kitenzi katika lugha ya Ks huchukua viambishi {i-} na {zi-} na Ek huchukua {ya-} na {chi-}, katika hali timilifu.

Mifano.

32) Ks: (1) Nyumba hii i-ta-anguk-a.

(2) Nyumba hizi zi-ta-anguk-a.

Ek (3) E-nyomba e-ye n-e-gw-e.

Kb ngeli 9 nyumba kip – kionyeshi kiy – kip – mzizi T – kiishio
(Nyumba hii imeanguka.)

(4) Chi-nyomba e-chi n-chi-gw-e.

Kb ngeli 10 nyumba kip – kionyeshi kiy – kip – mzizi T – kiishio
(Nyumba hizi zitaanguka.)

(5) E-nyomba e-ye ya-gu-r-e.

Kb ngeli 9 nyumba kip – kionyeshi kip – mzizi T – hali -kiishio.
(Nyumba hii imeanguka.)

(6) Chi-nyomba e-chi chi-agu-r-e.

Kb ngeli 10 nyumba kip – kionyeshi kip – mzizi T – hali -kiishio
(Nyumba hizi zimeanguka.)

Tumetoa mifano miwili katika lugha ya Ek kwa kusudi la kuonyesha tofauti zilizopo kati ya upatanishi kimofosintaksia kuambatana na wakati. Kundi la 1/2 tulieleza kwa kifupi tu kuwa, upatanishi katika lugha ya Ek hauna mpangilio mahususi bali hubadilika kwa kuzingatia wakati na hali. Kwa mifano sentensi (iii) na (iv) ni za wakati ujao ilhali zile za (v), (vi) ni za hali timilifu utaona vipatanishi katika wakati ujao ni {ne-} na {nchi-} na katika hali timilifu ni {ya-} na {chi-}.

2.2.6 Kikundi la 11/10a/11a/6a

Ks katika kundi hili huwa viambishi vya upatanishi ni vya aina mbili {u-} umoja na {zi-} na {u-} na {ya-} katika umoja na wingi. Ek huwa na viambishi vya aina tatu, {βu-} na {a-} (ambavyo vina sura kama {βu-/βwa-/mbwa-/mbwa-}) na {ru-} na {chia-} (ambavyo huchukua sura mbalimbali kama {ru- /rwa/ndwa-/ndo-} na {chia-/ nchi-}) {ku-} na {a-} (ambavyo pia huchukua sura mbalimbali kama {ku-/kwa-/nkwa-/nko-}) na {a-/na-}. Hebu sasa chunguza mifano ifuatayo.

- 33) Ks. (i) Uso umeparara.
(ii) Nyuso zimeparara

- (iii) Ugonjwa umcnea
 - (iv) Magonjwa yameenea.
- Ek
- (i) **Oβosio βwomire/mbwoma/mbwome.**
(uso umeaparara/uliparara/utaparara.)
 - (ii) **Amasio aomire/noma/nome (naome/- (nome)**
(Nyuso zimeparara.)
 - (iii) **Oraβambo rwagure/ndwagua/ndogwe.**
(mkeka umeanguka/ulianguka/utaanguka.)
 - (iv) **Chimbambo chiagure/nchiagwa/nchigwe.**
(Mikeka imeanguka/ ilianguka/ itaanguka.)
 - (v) **Okogoro kwane kwabunekire/nkwabuneka/nkobuneke.**
(mguu wangu umevunjika/ulivunjika / utavunjika).
 - (vi) **Amagoro ane abunekire/nabuneka/nabuneke.**
(Miguu yangu imevunjika / ilivunjika/ itavunjika.)

Mabadiliko ya vipatanishi tunayoyaona katika lugha ya Ek, hutokea kwa kuzingatia sheria za kimofonolojia. Mabadiliko haya hayatokei tu kwa kundi hili bali kwa makundi yote kama tulivyodokeza.

2.2.7 Kundi la ngeli ya 12/8a

Kundi hili la ngeli katika Ks, hupatikana katika kundi la 7/8 kiupatanishi, lugha ya Ek vipatanishi huwa ni {ka-/ga-} umoja na wingi ni (βi-). Hapa vipatanishi hivi huchukua mabadiliko yale tuliyotaja ya wakati. Mifano:

34) (i) (a) Aka-na ka-ne ga-ch-ir-e.

kb ngeli 12 – kitoto kip – kimilikishi kip – mzizi T – hali – kiishio.

(Kitoto chirangu kinnekuja.)

(b) Eβi-ana βi-ane βia-chi-r-e.

kb ngeli 8a – vitoto kip – kimilikishi kip – mzizi T – hali – kiishio.

(vitoto vyangu vimekuja)

(ii) (a) Aga-iseke ka-ria n-go-som-a ka-r-e.

kb ngeli 12 – kisichana kip kionyeshi kiy – hali – mzizi T – kiishio kip – hali – kiishio.

(Kijisichana kile kinasoma.)

(c) Eβi-iseke βi-ria n-go-som-a βi-r-e.

kb ngeli 8 – visichana kip kionyeshi kiy – hali – mzizi T – kiishio kip – hali – kiishio.

(Vijisichana vile vimesoma)

2.2.8 Kundi La 14

Kisemantiki majina katika kundi hili huwa ni nomino za kidhahania katika lugha zote mbili. Upatanishi kisintaksia kwa Ks huchukua {u-}, na kwa baadhi ya nomino zinazochukua wingi huwa ni {ya-} kama katika mfano (i) na (ii). Ek vipatanishi ni {βu-} kama inavyodhihirika katika mifano (iii) umoja.

35) Ks (i) Uovu u-me-m-shind-a.

Ma-ovu ya-me-m-shind-a.

(ii) U-jinga wa-ke u-me-mw-umiz-a.

Ek (i) Oβo-gotu βwa-mo-nyar-ir-e.

Kb ngeli – uzee kip –yambwa – mzizi T – hali – kiishio.

(Uzee umemlemea)

2.2.9 Kundi la 15.

Viambishi vya upatanishi katika ngeli hii kwa Ks ni {ku-} sawa na Ek ambacho huchukua {ku-} pia

Mifano:

36) Ks. Kulima kwake kunapendeza

Ek. **Okorema** kwaye kwangokirie. (Tafsiri ya Ks)

Katika Ek.

/ 0 / → w / - a.

/ko+aremire/ → (kwaremire).

/ko+ aŋgokirie/ → [kwaŋgokirie]

Pia katika Ek. /n/ hubadilika na kuwa /ŋ/ ikiwa inatanguliwa na /g/

/ n / → ŋ / - g

/n-gokirie/ → [ŋgokirie]

2.2.10 Kundi la 16/17/18

Viambishi vipatanishi katika lugha hizi mbili ni vile vya kimofolojia, ambapo Ks ni {pa-/po-} {ku/ka}, {mu-/mo-} na Ek huchukua {a-} kwa kundi la 16/17. Kunao tofauti kubwa kati ya Ks na Ek katika upatanishi wa kuonyesha mahali ndani. Ek haina viambishi vipatanishi vya mahali ndani bali upatanishi wa mahali ndani hupatanishwa na nomino inayohusishwa na mahali ndani. Kwa hiyo, katika Ek upatanishi wake hubadilika kuambatana na nomino, mfano wa (v) na (vi).

37. Ks (i) pahali pale panavutia
(ii) Mahali kule kunapendeza
(iii) Dukani humo mna nyoka
(iv) **Aase** ayio abeire
(mahali-hapo pamekuwa)


- (v) **Eduka ime engiti neroo**
(Dukani nyoka ako)
- (vi) **Nyomba ime amache aerire**
(Nyumbani maji yameisha)

2.3.0 Ulinganishi Wa Kirai Nomino Cha Ks Na Ek

Kwa sababu ya nafasi inayochukuliwa na KN katika KT tumeona kuwa ni muhimu kuchunguza muundo na upatanishi wa KN, hasa katika kuangalia vipatanisho vyake. KN ni neno au kundi la maneno ambalo lina nomino au kiwakilishi nomino kama neno kuu linalofanya kazi kama kiima. Kundi hili la maneno pia hufanya kazi kama nomino¹⁰ KN kinaweza kufanyakazi kama kijalizo na chagizo¹¹, pia katika KT, KN uamilifu wake huweza kuwa ule wa yambwa, yambwa tendwa au tendewa. Virai nomino huwa havina muundo wa kiima kiarifu bali huwa muundo wake umejikita kwenye nomino au mahusiano ya nomino na neno au mafungu ya maneno¹². Muundo wa KN huwa au unaweza kuwa na vipashio vifuatavyo:

- i) Nomino peke yake au nomino mbili na zaidi
- ii) Nomino na kivumishi au vivumishi
- iii) Nomino kivumishi na kielezi
- iv) Nomino na kirai kivumishi
- v) Nomino, kirai rejeshi
- vi) Nomino, kirai kivumishi na kirai kirejeshi

Kisheria tunaweza kufupisha muundo huu wa KN kama ;



Sheria hii haimaanishi kwamba lazima KN kiwe na vipashio hivi, bali KN kinaweza kuchukua nomino na kimojawapo au baadhi ya vipashio hivi ili kuunda KN katika lugha hizi. Hebu tuchambue vipashio hivi, huku tukionyesha muundo na upatanishi wao na nomino kama neno kuu la KN, katika lugha ya Ks na Ek.

2.3.1.0 Vivumishi katika Ks na Ek

Vivumishi ni maneno ambayo yanahusiana sana na nomino na majukumu yao kisarafu, ni kueleza zaidi au kutoa habari juu ya nomino au kikundi cha nomino¹⁵. Vivumishi pia huwa na upatanishi na nomino zinazovumishwa navyo. Vipo vivumishi kadha wa kadha kama vile; vivumishi vya sifa, vivumishi viulizi, vivumishi vya idadi, vionyeshi, vimilikishi, virejeshi na vya a- unganifu.

2.3.1.1 Ulinganishi wa Vivumishi vya sifa katika Ks na Ek

Haya ni maneno yanayotoa sifa za mtu au kitu jinsi mtu au kitu hicho kinavyoonekana. Vivumishi hivi, huchukua viambishi vya ngeli inayohusiana na sifa iliyotajwa ili kupatanisha nomino na sifa katika lugha ya Ks na Ek. Kwa mfano, viambishi huambatanishwa na sifa hizi: Ek (Ks) – ya (-zuri), nene (-nene), rabu (-eupe), mwamu (-eusi), -tambe (-refu), -eng'e (-fupi) n.k.

- 38) Ks . Mvulana mweusi
Nguo nyeusi

Kitabu kizuri

Ek . **Omomura omomwamu**

Eyanga emwamu

Egetabu ekiya

Viambishi vilivyopigiwa mistari huonyesha upatanishi wa viambishi na nomino na vile vya vivumishi vya sifa katika lugha ya Ks na Ek. Kimuundo sifa hufuata nomino katika lugha ya Ks na Ek.

2.3.1.2 Vivumishi viulizi vya Ks na Ek

Vivumishi viulizi ni maneno yanayotumiwa kuulizia swali kuhusu nomino na kimuundo hufuata nomino katika lugha ya Ks na Ek. Ikiwa viulizi vitatangulia huwa ni viwakilishi na hutumiwa bila kutaja nomino yenyewe. Wataalamu wengi hupendekeza kuwa Ks ina aina tatu za viulizi ambapo **-pi** na **-ngapi** huchukua viambishi vya ngeli ya upatanisho, na **gani** huwa hakichukui viambishi bali hutumiwa tu hivyo. Lugha ya Ek, pia ina vivumishi viulizi vitatu ambavyo **ni -ri**, **(-ipi)** , **-renga (- ngapi)** na **ki (gani)** ambacho hakichukui viambishi vya ngeli, kama Ks. Inaonekana kuwa, vivumishi viulizi vinafanana katika lugha hizi mbili.

Mfano:

- 39) Ks i) Msichana yupi aliyekuja?
 ii) Mliimba wimbo upi?
 iii) Viti vingapi vimetengenezwa?
 iv) Aliingia nyumba gani?
- Ek i) **Monto ki oata? (mtu gani alivunja?)**
 ii) **Enyomba ereri yagwa? (nyumba ipi ilianguka?)**
 iii) **Emete erenga? (miti mingapi?)**
 iv) **Aβana βarenga?(watoto wangapi?)**

2.3.1.3 Vivumishi vya idadi vya Ks na Ek

Kiulinganishi , lugha ya Ks na Ek huwa na vivumishi vya idadi ambavyo ni vya aina mbili; vile vya idadi maalumu na vile vya maneno ya kujumlisha kiidadi. Lugha ya Ks kwa mfano huambisha idadi kuanzia moja hadi tano , na nane , lakini sita saba, tisa, na kumi haziambishwi viambishi kuambatana na ngeli; Lugha ya Ek pia huambatanisha idadi ya nambari ya kwanza hadi nane isipokuwa tisa na kumi ambazo hazichukui viambishi vya ngeli. Kwa mfano.

40 Ks mtu mmoja / wwili / watatu /watano/ sita / kumi.

Ek omonto oyomo /βabere /βatato / βatano/ βatanomo / βatano βabere/ ikomi.

Maneno ya kuonyesha idadi kwa jumla bila kubainisha idadi kamili katika Ks na Ek ni kama yafuatayo, Ek (Ks) -**ke (-chache)** , -**nge (- ingi)**, -**onsi (- ote)**, -**nde (ingine + o)**, mifano ya KN.

41) Ks -**ingi** – watu wengi , miti mingi , meno mengi , nyumba nyingi.

Ek -**nge** – aβanto abange ,emente emenge , amaino amange , chinyomba chinyinge

Ks : -**chache** - - vitabu vichache , wasichana wachache

Ek : -**ke** –eβitaβu βike, aβaiske βake.

Ks: - **ote** – mikuki yote , nguo zote , mahindi yote

Ek: - **onsi**- amatimo onsi, chianga chionsi , eβituma βionsi

2.3.1.4 Vivumishi Vionyeshi / Viashiria

Vionyeshi ni vipashio vinavyotumiwa kurejelea kwenye muktadha wa mahali alipo msemaji na uamilifu wake ni uonyeshi¹⁴. Hutumika kuonyesha nomino zikiwa mbali au karibu na msemaji au msikilizaji huku vikiashiria kwa mahali au wakati.

Vivumishi vionyeshi katika lugha ya Ks na Ek huwa ni vya aina tatu. Kwanza, kuna vile vivumishi vionyeshi vya karibu katika lugha ya Ks na Ek, ambavyo huashiria ujirani wa karibu¹⁵ kiasi kwamba msemaji anaweza kuzigusa au kuzishika. Katika lugha ya Ks, vionyeshi hivi huundwa kutokana na mzizi **ha- hi** – na **hu-** kisha unafuatwa na viambishi vya upatanishi vya nomino kuambatana na ngeli. Ek vionyeshi vya karibu vingi huchukua viambishi vya upatanishi, na baadhi huchukua visabiki vya nomino ambatanishi na kiyeyusho /j/ kikifuatwa na vokali ya kipatanishi.

Jedwali 5 Vionyeshi vya karibu katika Ks na Ek.

Ngeli	Kiswahili Sanifu		Ekegusii		Kiswahilio
	Vionyeshi	Mifano	Vionyeshi	Mifano	
1	Hu+yu – huyu	Mtu huyu	0+j+o – ojo	Omonto oyo	Mtu huyu
2	Ha+wa – hawa	Watu hawa	a+β+a – aβa	Aβanto aβa	Watu hawa
3	Hu+u – huu	Mti huu	o+j+o – ojo	Omote oyo	Mti huu
4	Hi+i – hii	Miti hii	e+j+e – eje	Emete eye	Miti hii
5	Hi+li – hili	Tunda hili	e+r+i – eri	Eriso eri	Jicho hili
6	Ha+ya – haya	Matunda haya	a+j+ta – aja	Amaiso aya	Macho haya
7	Hi + ki – hiki	Kiti hiki	e+k-e – eke	Ekerogo eke	Kiti hiki
8	Hi+vi – hivi	Viti hivi	e+β-i – eβi	Eβirogo eβi	Viti hivi
9	Hi + i – hii	Nguo hii	e+j+e – eje	Eyanga eye	Nguo hii
10	Hi + zi – hizi	Nguo hizi	e+t j- et j	Chianga echi	Nguo hizi
11	Hu+u – huu	Ukuta huu	o+r+o – oro	oroβago oro	Ukuta huu
10a	Ha + ya – haya	Kuta hizi	e+t j+ - et j	Chimbago echi	Kuta hizi
11	Hu+u – huu	Ugonjwa huu	o+β-o-oβo	Oβorwaire oβo	Ugonjwa huu
6a	Ha+ya – haya	Magonjwa haya	a+j+a-aj a	Amarwaire aya	Magonjwa haya
11b	-	-	o+k+o-oko	Okogoro oko	Mguu huu
6b	-	-	a+j +a-aj a	Amagoro aya	Miguu hii
12	-	-	a+ka-aka	Akana aka	Kitoto hiki
8a	-	-	e+βi – eβi	Eβiana eβi	Vitoto hivi
14	Hu+u-huu	Ujinga huu	o+βo –oβo	Oβoriri oβo	Ujinga huu
15	Hu+ku-huku	Kulima huku	o+ko-oko	Okorema oko	Kulima huku
16	Ha+pa-hapa	Pahali hapa	a'a-aa	Ase aa	Mahali huku
17	Hu+ku-huku	Mahali huku	a+a-aa	Ase aa	Mahali huku
18 *	Hu+mu-humu	Dukani humu	i+m+a-ima	Nyomba imaa	Nyumbani humu

Vionyeshi vya karibu vya lugha ya Ek mara nyingi hutumiwa pamoja na neno-
'iga' kumaanisha vitu/watu/wanyama walio karibu na msemaji. Neno hili 'iga'
hutumiwa kubainisha na kusisitiza hali ya ujirani wa karibu.

42) **Eβitabu eβiiga.**
(vitabu hivi)

Pili, kuna vionyeshi vya kuonyesha ujirani wa mbali. Hivi katika lugha ya Ks
huundwa kwa kuongeza viambishi ngeli kwenye shina la mofimu {-le}¹⁶. Katika
lugha ya Ek mzizi wa kionyeshi hiki ni {-ria} ambao pia huambishwa vipatanishi
vya nomino kutegemea ngeli. Tazama jedwali 6.

Jedwali 6. Vionyeshi vya kuonyesha ujirani wa mbali.

Ng eli	Kiswahili Sanifu		Ekegusii		
	Vionyeshi	Mifano	Vionyeshi	Mifano	Tafsiri
1	Yu+le – yule	Mtu yule	O+ria-oria	Omonto oria	Mtu yule
2	Wa+le – wale	Watu wale	βa+ria – baria	Aβanto baria	Watu wale
3	U+le – ule	Mti ule	O+ria – oria	Omote oria	Mti ule
4	I+le – ile	Miti ile	E+ria – eria	Emete eria	Miti ile
5	Li+le – lile	Tunda lile	Ri+ria – riria	Eriso riria	Jicho lile
6	Ya+le- yale	Matunda yale	A+ria – aria	Amaiso aria	Macho yale
7	Ki+le – kille	Kiti kile	Ke+ria – Keria	Ekerogo keria	Kiti kile
8	Vi+le- vile	Viti vile	βi+ria – βiria	Eβirogo βiria	Viti vile
9	I+le – ile	Nguo ile	E+ria – eria	Eyanga eria	Nguo ile
10	Zi+le – zile	Nguo zile	Chi+ria-chiria	Chianga chiria	Nguo zile
11	U+le – ule	Ukuta ule	Ro+ria roria	Oroβago roria	Ukuta ule
10a	Zi+le – zile	Kuta zile	Chi+ria chiria	Chimbago chiria	Kuta zile
11a	U+le – ule	Ugonjwa ule	βo+ria-βoria	Oβorwaire βoria	Ugonjwa ule
6a	Ya+le –yale	Magonjwa yale	A+ria – aria	Amarwaire aria	Magonjwa yale
11b	-	-	Ko+ria – koria	Okogoro koria	Mguu ule
6b	-	-	A+ria – aria	Amagoro aria	Miguu ile.
12	-	-	Ka+ria-karia	Akana karia	Kitoto kile
8a	-	-	βi+ria – βiria	Eβiana βiria	Vitoto vile

14	u+le – ule	urembo ule	β+ria –βoria	Oβoriri βoria	Ujinga ule
15	ku+le – kule	kulima kule	Ko+ria –koria	Okorema koria	Kulima kule
16	pa+le – pale	pahali pale	A+ria – aria	Aase aria	Mahali pale
17	ku+le – kule	mahali kule	A+ria – aria	Aase aria	Mahali kule
18	m+le – mle	dukani mle	Ime+a+ria- amearia	Nyuimba imaria	Nyumbani mle

Aina ya tatu ya vionyeshi ni vile vinavyoonyesha nomino iliyokwisha tajwa na imefahamika. Mara nyingine nomino tajwa inaweza kuwa haionekani au inaonekana, na wazungumzaji. Pia vivumishi vionyeshi hivi huitwa virejeshi. Lugha ya Ks na Ek huwa na irabu {-o} mwishoni mwa kila kirejeshi, mwanzoni huwa na mzizi aidha {hi-}, {hu-} au {ha-} ambao hupatanishwa na vipatanishi vya nomino. Ek nayo ina irabu {-uo} au {-io} mwishoni na mwanzoni huchukua viambishi vipatanishi vya nomino kutegemea na nomino inayovumishwa. Tazama mifano katika Jedwali hii

Jedwali 7. Vionyeshi virejeshi vya Ks na Ek.

Ngeli	Kiswahili Sanifu		Ekegusi:	
	Vionyeshi	Mifano	Vionyeshi	Mifano
1	Hu+yo – huyo	Mtu huyo	O+y+io-oyio	Omonto oyio
2	Ha+o – hao	Watu hao	A+β+uo→a β wo	Aβanto aβwo
3	Hu+o – huo	Mti huo	O+y+io-oyio	Mote oyio
4	Hi+yo – hiyo	Miti hiyo	E+y+io- eyio	Emete eyio
5	Hi+lo – hilo	Tunda hilo	E+r+io-erio	Rituna erio
6	Ha+yo – hayo	Matunda hayo	A+y+io-ayio	Amatunda ayio
7	Hi+cho – hicho	Kiti hicho	E+k+io – ekio	Ekerogo ekio
8	Hi+vyo – hivyo	Viti hivyo	E+ β +io – e β io	Eβirogo ebio
9	Hi+yo – hiyo	Nguo hiyo	E+y+io-Eyio	Eyanga eyio
10	Hi+zo – hizo	Nguo hizo	E+y+io – echio	Chianga echio
11	Hu+o – huo	Ukuta huo	O+r+uo – orwo	Orobago orwo
10a	Hi+zo – hizo	Kuta hizo	E+y+io – echio	Chimbago echio
11a	Hu+o – huo	Ugonjwa huo	O+ β +uo o β wo	Oβorwaire oβwo
6a	Ha+yo – hayo	Magonjwa hayo	A+y+io – ayio	Amarwire ayio
11b	-	-	O+k+uo- okwo	Okogoro okwo
6b	-	-	A+y+io- ayio	Amagoro ayio
12	-	-	A+k+uo akwo	Akana akwo
8a	-	-	E+ β i+io – e β io	Eβiana eβio
14	hu+o – huo	urembo huo	O+ β +uo- o β wo	Oβoriri oβwo
15	hu+ko-huko	kulima huko	O+k+uo- okwo	Okorema okwo
16	ha+po-hapo	pahali hapo	A+g+uo- agwo	Aase agwo
17	hu+ko – huko	mahali huko	A+g+uo- agwo	Ase agwo
18	hu+mo - humo	dukani humo	Ime+a+ β +uo imaβwo	Nyumba imaiβwo

Aina hii ya vionyeshi inaweza kutumiwa kama vionyeshi vya karibu, ikiwa nomino inayoashiriwa iko karibu na msikilizaji na mbali kutoka kwa msemaji, katika lugha ya Ks na Ek. Huenda, ndio sababu, inayowafanya wanaisimu wengine kuviita vionyeshi vya karibu. Ni muhimu kudokeza kuwa, Ek mbali na Ks, vionyeshi vya ngeli ya 18 huandamana na neno **ime** (ndani) ili kubainisha uonyeshi wa ndani.

Vivumishi vionyeshi kwa jumla, kimuundo huwa vinafuata nomino katika lugha hizi mbili. Lakini wakati mwingine katika Ks vionyeshi vinaweza kutangulia nomino tofauti na Ek ambapo kwa vyovyote vionyeshi havitangulii nomino katika KN, isipokuwa kwa sentensi tu kwa mfano:

- 43) Ks (i) Yule m-zee.
Ek (ii) **Omo-gaka o-ria.** (Mzee yule.)
Kb ngeli 1 mzee kip nafsi 3 umoja kionyeshi mbali.
Ek (iii) **O-ria no mo-gaka.** (Yule ni mzee.)
Kip nafsi 3 umoja Tsh kb ngeli zee.

2.3.1.5 Vivumishi vimilikishi vya Ks na Ek

Vimilikishi ni aina ya maneno ambayo huonyesha uhusiano wa kitu kuwa mali ya mtu¹⁵. Maelezo haya bado yana upungufu kwa kuwa hayadokezi wazi hali ya kuvumisha. Kwa hiyo, twaweza kusema kuwa vimilikishi ni maneno yanayotoa dhana ya 'kuwa na' au kumiliki nomino fulani au sifa za nomino fulani na nomino nyingine. Ni maneno yanayoonyesha hali ya kumiliki.

Kimsingi, lugha ya Ks na Ek zina mizizi mitatu ya vimilikishi, ambayo katika umoja na wingi wake huwa ni sita. Mizizi hii ya vimilikishi katika lugha ya Ks na Ek, huambishwa viambishi vya upatanisho vya nomino mbalimbali katika ngeli. Mizizi hiyo hutegemea nafsi.

	Kiswahili Sanifu		Ekegusii	
	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>	<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>
Nafsi ya 1	-angu	-etu	-ne	-ito
Nafsi ya 2	-ako	-enu	-o	-ino
Nafsi ya 3	-ake	-ao	-ye	-βo

Mifano katika KN ambayo huonyesha upatanishi kati ya nomino na vivumishi vimilikishi katika lugha ya Ks na Ek ni:

- 43) Ks. (i) M-toto w-angu/w-ako/w-ake.
 Wa-toto w-etu/w-enu/w-ao.
- (ii) **Omwa-na o-ne/o-o/o-ye.**
 Kb ngeli 1 mtoto kip angu/kip ako/kip/ake.
Aba-na βa-ito/ βa-ino/ βa-bo.
 Kb ngeli 2 watoto kip angu/kip ako/kip/ake.

Kimuundo, vimilikishi huwa na mofimu mbili; ya kwanza ni mofimu ya upatanishi na ya pili ni mzizi wa vimilikishi. Kwa mfano.

44) Kiswahili Sanifu	Ekegusii
[Wangu] ← /wa+angu/	[one] — /o+ne/ (wangu)
[Wangu] ← /wa+angu/	[one] — /o+ne/(wangu)
[Wetu] ← /wa+etu/	[oino] — /o+ino/(wenu)
[Wake] ← /wa+ake/	[βaβo] — /βa+βo/(wao)

Kutokana na mifano ya lugha ya Ks, kuna mabadiliko ya vokali ambayo huchukua vokali na pia udondoshaji wa vokali.

Kwa Mfano:

/wa+angu/, /a/ moja inadondoshwa na kuwa [wangu], na katika/wa+etu/, vokali/a/ inadondoshwa, hivyo kuwa [wetu]

Hata hivyo, vimilikishi kwa jumla huwa na elementi tatu kuu; kipatanishi, kiwakilishi ngeli na mzizi wa kimilikishi husika. Osinde (1988) anaongezea kuwa vimilikishi vya Ek vina kiambatanishi cha a-unganifu.

Jedwali 8 ifuatayo inaonyesha viambishi vipatanishi vimilikishi katika lugha ya Ks.

Ngeli	Viambishi vipatanishi	Vimilikishi		
		Nafsi ya 1	Nafsi ya 2	Nafsi 3
1	Wa	<u>W</u> angu/ <u>w</u> etu	<u>W</u> ako/ <u>w</u> enu	<u>W</u> ake/ <u>w</u> ao
2	Wa	<u>W</u> angu/ <u>w</u> etu	<u>W</u> ako/ <u>w</u> enu	<u>W</u> ake/ <u>w</u> ao
3	U	<u>U</u> angu/ <u>u</u> etu	<u>U</u> ako/ <u>u</u> enu	<u>U</u> ake/ <u>u</u> ao
4	I	<u>Y</u> angu/ <u>y</u> etu	<u>Y</u> ako/ <u>y</u> enu	<u>Y</u> ake/ <u>y</u> ao
5	Li	<u>L</u> angu/ <u>l</u> etu	<u>L</u> ako/ <u>l</u> enu	<u>L</u> ake/ <u>l</u> ao
6	Ya	<u>Y</u> angu/ <u>y</u> etu	<u>Y</u> ako/ <u>y</u> enu	<u>Y</u> ake/ <u>y</u> ao
7	Ki	<u>C</u> hangu/ <u>ch</u> etu	<u>C</u> hako/ <u>ch</u> enu	<u>C</u> hake/ <u>ch</u> ao
8	Vi	<u>Y</u> angu/ <u>vy</u> etu	<u>Vy</u> ako/ <u>vy</u> enu	<u>Vy</u> ake/ <u>vy</u> ao
9	I	<u>Y</u> angu/ <u>y</u> etu	<u>Y</u> ako/ <u>y</u> enu	<u>Y</u> ake/ <u>y</u> ao
10	Zi	<u>Z</u> angu/ <u>z</u> etu	<u>Z</u> ako/ <u>z</u> enu	<u>Z</u> ake/ <u>z</u> ao
11	U	<u>W</u> angu/ <u>w</u> etu	<u>W</u> ako/ <u>w</u> enu	<u>W</u> ake/ <u>w</u> ao
10a	Zi	<u>Z</u> angu/ <u>z</u> etu	<u>z</u> ako/ <u>z</u> enu	<u>Z</u> ake/ <u>z</u> ao
11a	U	<u>W</u> angu/ <u>w</u> etu	<u>W</u> ako/ <u>w</u> enu	<u>W</u> ake/ <u>w</u> ao
6a	Ya	<u>Y</u> angu/ <u>y</u> etu	<u>Y</u> ako/ <u>y</u> enu	<u>Y</u> ake/ <u>y</u> ao
14	U	<u>W</u> angu/ <u>w</u> etu	<u>W</u> ako/ <u>w</u> enu	<u>W</u> ake/ <u>w</u> ao
15	Ku	<u>Y</u> angu/ <u>y</u> etu	<u>Kw</u> ako/ <u>kw</u> enu	<u>Kw</u> ake/ <u>kw</u> ao
16	Pa	<u>W</u> angu/ <u>w</u> etu	<u>P</u> ako/ <u>p</u> enu	<u>P</u> ake/ <u>p</u> ao
17	Ku	<u>Kw</u> angu/ <u>kw</u> etu	<u>Kw</u> ako/ <u>kw</u> enu	<u>Kw</u> ake/ <u>kw</u> ao
18	mu	<u>Mw</u> angu/ <u>mw</u> etu	<u>Mw</u> ako/ <u>mw</u> enu	<u>Mw</u> ake/ <u>mw</u> ao

Jedwali 9 viambishi vipatanishi na vimilikishi vya lugha ya Ek.

Ngeli	Viambishi vipatanishi	Vimilikishi		
		Nafsi ya 1	Nafsi ya 2	Nafsi ya 3
1	o-	<u>O</u> ne/ <u>o</u> itop	<u>O</u> o/ <u>o</u> ino	<u>O</u> ye/ <u>o</u> βo
2	βa-	<u>β</u> ane/ <u>β</u> aito	<u>β</u> ao/ <u>β</u> aino	<u>β</u> aye/ <u>β</u> aβo
3	o-	<u>O</u> ne/ <u>o</u> ito	<u>O</u> o/ <u>o</u> ino	<u>O</u> ye/ <u>β</u> aβo
4	ya-	<u>Y</u> ane/ <u>y</u> aito	<u>Y</u> ao/ <u>y</u> aino	<u>Y</u> aye/ <u>y</u> aβo
5	ri-	<u>R</u> aine/ <u>r</u> iato	<u>R</u> iao/ <u>r</u> aino	<u>R</u> iaye/ <u>r</u> ia βo
6	a-	<u>A</u> ne/ <u>a</u> itu	<u>A</u> o/ <u>a</u> ino	<u>A</u> ye/ <u>a</u> βo
7	ki/gi-	<u>K</u> iane/ <u>g</u> iato	<u>K</u> iao/ <u>k</u> aino	<u>K</u> iaye/ <u>k</u> iaβo
8	βia-	<u>β</u> iane/ <u>β</u> iato	<u>β</u> iao/ <u>β</u> aino	<u>β</u> iaye/ <u>β</u> ia βo
9	ya-	<u>Y</u> ane/ <u>y</u> ato	<u>Y</u> ao/ <u>y</u> aino	<u>Y</u> aye/ <u>Y</u> a βo
10	chia-	<u>C</u> hiano/ <u>ch</u> iato	<u>C</u> hiao/ <u>ch</u> aino	<u>C</u> hiate/ <u>ch</u> ia βo
11	ru-	<u>R</u> wane/ <u>r</u> waito	<u>R</u> wao/ <u>r</u> waino	<u>R</u> waye/ <u>r</u> waβo
10a	chia-	<u>C</u> hiane/ <u>ch</u> iaito	<u>C</u> hiao/ <u>ch</u> iano	<u>C</u> hiaye/ <u>ch</u> iaβo
11a	βu-	<u>β</u> wane/ <u>β</u> waito	<u>β</u> wao/ <u>β</u> waino	<u>β</u> waye/ <u>β</u> waβo
6a	a-	<u>A</u> ne/ <u>a</u> ito	<u>A</u> o/ <u>a</u> ino	<u>A</u> ye/ <u>a</u> βo
11b	kugu-	<u>K</u> wane/ <u>g</u> waito	<u>K</u> wao/ <u>k</u> waino	<u>K</u> waye/ <u>k</u> waβo
6b	a-	<u>A</u> ne/ <u>a</u> ito	<u>A</u> o/ <u>a</u> ino	<u>A</u> ye/ <u>a</u> βo
12	ka-	<u>K</u> ane/ <u>g</u> aito	<u>K</u> ao/ <u>k</u> aino	<u>K</u> aye/ <u>k</u> aβo
8a	βi-	<u>β</u> iane/ <u>β</u> iaito	<u>β</u> iao/ <u>β</u> iaro	<u>β</u> iaye/ <u>β</u> iaβo
14	βu-	<u>β</u> wane/ <u>β</u> waito	<u>β</u> wao/ <u>β</u> wairio	<u>β</u> waye/ <u>k</u> waβo
15	kugu-	<u>K</u> wane/ <u>g</u> waito	<u>K</u> wao, <u>k</u> waino	<u>K</u> waye/ <u>k</u> waβo
16/n	a-	<u>A</u> ne/ <u>a</u> ito	<u>A</u> o/ <u>a</u> ino	<u>A</u> ye/ <u>a</u> βo
18	mu-	<u>M</u> wane/ <u>m</u> inito	<u>M</u> wao/ <u>m</u> ino	<u>M</u> waye/ <u>m</u> waβo

Tunapochunguza jedwali hizo za vimilikishi tunaona kuwa kuna mabadiliko mengi ya kimofofolojia ambayo hutokea kwa ajili ya kurahisisha matamshi.

Kwa mfano katika lugha ya Ek, /k/ inabadilika na kuwa / / pale ambapo mzizi wa kimilikishi huwa konsonanti ya ufizi kizuiwa /t/. Km.

/Ku+a+ito/ →[ɣwaito]

Umilikishi katika lugha hizi pia huonyeshwa na mizizi ya vivumishi kama {-enye} na {enyewe} katika lugha ya Ks, na Ek kwa kutumia {-nyene} (enye/enyewe). Tofauti kati ya lugha hizi katika vivumishi hivi ni kuwa, lugha ya Ek ina mzizi mmoja {nyene} ambao ni sawa na mizizi miwili ya lugha ya Ks {-enye} na {enyewe}. Mizizi hii hutumiwa kuonyesha hali ya 'kuwa na' Tazama mifano ya 45.

- 45) Ks. (i) Mvulana mwenye hekima.
(ii) Mkurugenzi mwenye gari.
(iii) **Omoiseke oβwate oβongaini**
(Msichana mwenye akili.)
Ek. (iv) **Omongina omonyene enyomba.**
(Mama mwenye nyumba.)

Kutokana na mifano hii, tunaweza kuona kwamba hali ya kumiliki katika lugha ya Ek huwa ni uwezo wa binadamu, tena anamiliki tu mali. Ikiwa mtu anamiliki tabia au hali fulani huwa mzizi unabadilika na kuwa aidha {-are} au {-βwate} (kuwa na) kuonyesha hali hiyo inadumu, kwa mfano wa (iv) hapo juu.

Katika lugha zote mbili, mizizi {enyewe} na {enyene} hutumiwa kumaanisha hali ya kuisitiza na pia kubainisha nomino husika. Kwa mifano

- 46) Ks: Mama mwenyewe ametoka.
Ek: **Omongina omonyene osokire.**
Ks: Mwenyewe ni Maria.
Ek: **Omonyene Maria.**
Ks: Kitabu chenyewe ni hiki.
Ek: **Egetaβu ekenyene nakio eko.**

2.3.1.6 Vivumishi Virejeshi Vya Ks na Ek

Katika lugha ya Ks virejeshi ni **amba-** na – **o-rejeshi**. Mbali na Ks, lugha ya Ek, ina tu kirejeshi ambacho pia huwa ni kionyeshi kirejeshi ambacho kiuamilifu hutumiwa kama amba-, mzizi wake ni {-ria}, kama lugha zingine za kibantu. Mizizi hii katika lugha hizi mbili huambishwa viambishi vipatanishi vya ngeli. Tazama mfano wa

47) Ks: Mti **ambao** ulikatwa umeoza.

Ek: Omote **oria** onachetwe ogundire.

Lugha ya Ek huwa haitofautishi kirejeshi **amba-** na **o-rejeshi** kama Ks, bali hutumia vionyeshi virejeshi kama o- rejeshi.

2.3.2.0 Viwakilishi Vya Ks na Ek

Kapinga (1983: 79) anaeleza viwakilishi kuwa ni maneno yoyote yanayosimama badala ya majina ili kujulisha kitu kinachohusika na maonyesho, ulizo au kitenzi kinachoarifu tukio fulani, ambapo jina la kitu chenyewe halitajwi. Kwa minajili hii, huwa nomino inayowakilishwa na kiwakilishi inafahamika au inaeleweka awali. Viwakilishi hivi vinavyofanana navyo ni: viwakilishi nafsi, viwakilishi vimilikishi, viwakilishi vionyeshi, viwakilishi viulizi, viwakilishi vya idadi na viwakilishi virejeshi.

2.3.2.1 Viwakilishi nafsi vya Ks na Ek

Haya huwa ni maneno huru na pia ni viambishi ambavyo hufanya kazi kama nomino katika nafsi zote tatu, kwa lugha ya Ek na Ks. Viwakilishi hivi vikiwa maneno huwa haviambishwi ilhali viambishi vyenycwe huambishwa kwa

kushikamanishwa na mizizi au viambishi vingine ndipo maana ijitokeze. Kwa hiyo, tumeviita viwakilishi **nafsi huru** na viwakilishi **nafsi funge**.

Viwakilishi **nafsi huru** ni kama:

	Kiswahili Sanifu		Ekegusii	
	<u>Umoja</u>	<u>wingi</u>	<u>umoja</u>	<u>wingi</u>
Nafsi ya 1.	mimi	sisi	inche	intwe
Nafsi ya 2.	wewe	nyinyi	aye	inwe
Nafsi ya 3.	yeye	wao	ere	βaraβwo

Mifano ya Sentensi

	Kiswahili Sanifu	Ekegusii
48) (i)	Mimi ninaimba	inche ngoterande.
(ii)	Wewe unasoma	ayengosomore.
(iii)	Yeye ameenda	ere ochire
(iv)	Sisi tunaimba	ntwe nkoteratore.

Viwakilishi nafsi funge ni:

	Kiswahili sanifu		Ekegusii		
	Nafsi	umoja	wingi	umoja	wingi
1.	ni-		tu-	n-	to-
2.	u-		m-	o-	mo-
3.	a-		wa-	a-	βa-
49) (i)	<u>N</u> inalima – <u>T</u> unalima		Nkorema <u>n</u> de – nkorema <u>t</u> ore		
(ii)	<u>U</u> nalima – <u>m</u> nalima		Nkorema <u>o</u> re – nkorema <u>m</u> ore		
(iii)	<u>A</u> nalima – <u>w</u> analima		Nkorema <u>a</u> re – nkorema <u>β</u> are		

Kutokana na mifano hii, viwakilishi funge vya lugha ya Ks, katika hali ya kuendelea, huchukua nafasi ya kwanza kimuundo katika KT, na vile vya Ek huchukua nafasi ya pili toka mwisho. Hii haimaanishi kuwa viwakilishi hivi havichukui nafasi nyingine. Vinaweza kubadilisha nafasi kuambatana na muundo

wa kirai. Viwakilishi vingine huwa ni sawa na vivumishi tulivyovishughulikia, isipokuwa vinatumika bila nomino ili kuwa vibadala. Kwa hivyo, rejelea sehemu ya vivumishi iliyopita ya sura hii.

Baada ya kueleza vipashio mbalimbali vya KN, tunaweza sasa kurudia yale mawazo yetu ya awali kuhusu KN cha lugha ya Ks na Ek. Tuliona kuwa kimuundo KN kinaweza kuwa na nomino peke yake au nomino mbili na zaidi. Kwa mifano:

- 50) Ks. Mama a-me-toka
Mama na baba wa-me-tok-a.
Ek. Moraa o-ch-ir-e
Moraa na Makori βa-ch-ir-e

Zilizopigiwa mistari ni nomino za KN katika lugha ya Ks na Ek.

Pia KN kinaweza kuwa na kivumishi au vivumishi na au virai vivumishi. Tumeshughulikia vivumishi aina nyingi, je vitapangikaje kimuundo katika KN. Hebu tazama mifano ifuatayo;

- 51) Ks (i) Msichana yule mweupe ameenda.
(ii) Msichana yule mwenye viatu vyeusi ameenda.
Ek (iii) **Omoiseke oria ochire.**
(msichana yule ameenda)
(iv) **Omoiseke oria omobariri obwate eyaanga embariri.**
(Msichana yule mweupe mwenye nguo nyekundu)

Sentensi ya 51 (i) ina vivumishi vya aina mbili; Kivumishi kionyeshi 'yule' na kivumishi cha sifa 'mweupe'. Kwa hiyo KN cha (i) ni msichana yule mweupe. Sentensi ya (ii) ina KN chenye nomino 'msichana'. Kionyeshi 'yule' na kirai kivumishi (KV) mwenye viatu vyeusi'. Sentensi ya (iii) ina kionyeshi 'oria'

(yule) na KN kina nomino ‘Omoiseke’ (msichana) na kionyeshi ‘oria’. Sentensi ya (iv) ina vilevile KN chenye nomino na kirai kivumishi. Kwa hiyo, KN kinaweza kuwa na nomino, kivumishi na au KV.

Pia KN cha lugha hizi kinaweza kuwa na muundo wa nomino, kivumishi na kielezi.

52) Ks. Mvulana huyu mrefu sana.

Ek. **Omomura oyo omotambe mono.**

Katika mifano hii, nomino ni ‘mvulana (omomura)’ kivumishi ni huyu (oyo) na mrefu (omotambe) na kielezi ni ‘sana (mono)’. KN kinaweza kuwa na muundo wa nomino na kirai rejeshi au pia nomino, kivumishi na kirai rejeshi. Hebu tuangalie mifano ifuatayo ya lugha ya Ks na Ek.

53) Ks. Mtoto ambaye alipita mtihani wake ameitwa.

Omwana oria oetete ametemwa aye orangerigwe.

(tafsiri ni ya Ks)

Kutokana na mifano hii nomino ni ‘mtoto (omwana)’ kirai rejeshi ni ‘oria oetete ametemwa aye’ (ambaye alipita mtihani wake). Lugha ya Ks huwa na kirai rejeshi chenye ‘o’ rejeshi ambayo lugha ya Ek haina. Badala ya o-rejeshi, Ek hubakia tu na kirejeshi kionyeshi. Kwa mfano:

54) Ks. Mtoto aliyepita mtihani wake ameitwa.

Ek. **Omwana oyio oetete ametemwa aye orangeriwe.**

Kwa kifupi, KN huwa na muundo huu lakini ni muhimu tukumbuke kuwa ‘kielezi’ tutakishughulikia katika sura ya tatu.

2.3.3 Hitimisho

Katika sura hii, tumejaribu kuweka msingi wa mada yetu kwa kuangalia mofolojia ya nomino, sintaksia ya nomino, vipashio vya KN na muundo na upatanishi wa KN. Ingawa hatukueleza upatanishi kama sehemu kando, tumeieleza pamoja na vipashio vya KN kwa sababu ingekuwa kama ni kujirudia kama tungeiweka kando kama sehemu. Hatukushughulikia sura hii kindani kwa sababu nia yetu ilikuwa kuonyesha KN kama elementi tutakayoitumia katika kufafanua KT chetu.

TANBIHI

1. Kamusi Sanifu Isimu na Lugha (1990) Tuki. Dar-es-salaam uk 32.
2. Mgullu, R.S (1999) Mtala wa Isimu: Fonetiki, Fonololija na Mofolojia ya Kiswahili. Longhorn Publishers uk 97.
3. Bakari, M. (1982) The Morphology of Kenyan Swahili Dialects. uk 215
4. Tumetoa maelezo ya Polome, E (1967) katika Swahili Language Handbook. uk 87.
5. Maoni ya Myachina, E (1973) Katika The Swahili Language: A Descriptive Grammar uk 28.
6. Kapinga, M (1983) Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu. Tuki. Dar-es-Salaam. uk. 48.
7. Mohammed, M. (1999) Modern Swahili Grammar uk 87.
8. Kama 4 hapo juu uk 77.
9. Mdee, J (1986) Kiswahili Muundo na Matumizi yake uk 35.
10. Todd, L. (1987) An introduction to Linguistics uk 60.
11. Kama 1 hapo juu. uk 42.
12. Maw, J (1969) Sentences in Swahili. A study in their internal Relationships Uk 32.
13. Massamba, D.P.B na wengine (1999) Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu. uk 77.
14. Kama 1 hapo juu uk. 40.
15. Kama 1 hapo juu uk 19.
16. Kama 5 hapo juu uk 79.

SURA YA TATU

3.0.0 Utangulizi

Sura hii inakusudia kuangazia msingi wa KT kwa kuchanganua muundo wa kitenzi cha lugha ya Ks na Ek. Haja kuu ya kutufanya tuchunguze kitenzi kimuundo, ni ile nafasi muhimu inayochukuliwa na kitenzi katika KT. Kama tulivyotanguliza katika sura ya kwanza, KT huongozwa au hutawaliwa na leksika kuu ambayo ni kitenzi. Pia nadharia ya uminimalisti huchunguza sifa za kimofolojia za vipashio kwa kukagua sifa za kisarufi za KT, kwa hiyo ni muhimu kwetu kuwekea msingi nadharia yetu kwa kuangalia muundo wa vitenzi.

Lugha ya Ks na Ek zina aina mbalimbali za vitenzi. Kwa minajili ya usogezi wa vitenzi ambayo ni kanuni mojawapo ya uminimalisti, tunahitaji pia kuwekea msingi aina ya vitenzi. Kwa sababu hii, tutaweza kugusia aina za vitenzi kijuujui kwa sababu ya muda tulionao mfupi.

3.1.0 Aina Za Vitenzi Katika Ks Na Ek

Kwa kuzingatia uamilifu na uhusiano wa vitenzi na maneno mengine katika kirai, tunaweza kuainisha vitenzi katika makundi manne makuu.

1. Vitenzi vikuu na vitenzi visaidizi.
2. Vitenzi vielekezi na visoelekezi.
3. Vitenzi vishirikishi.
4. Vitenzi visoukomo

3.1.1 Vitenzi Vikuu Na Vitenzi Visaidizi

Wataalamu wengi huita vitenzi vikuu vitenzi halisi ambavyo huonyesha hali ya kutendeka kwa jambo (Habwe J. 2004, Mgullu, R. 1999). Naye Mohammed (1999 : 80) anasema kuwa vitenzi kamili huonyesha idadi, kauli na dhamira ya sentensi.

Pia, tungependa kuongezea kuwa, vitenzi leksika huonyesha njeo, hali ya uyaikinishi au ukanushi na nafsi katika lugha hizi mbili. Aidha, ni muhimu kudokeza kuwa, vitenzi visaidizi navyo huonyesha idadi, njeo na hali yaikinishi au kanushi.

Vitenzi vikuu katika lugha ya Ks na Ek, huishia kwa vokali [-a] kama lugha zingine za Kibantu. Kwa mfano 1.

1) Ks. Som-a, lim-a, pik-a, imb-a

Ek. **Som-a, rem-a, rug-a, tɛr-a.** (Tafsiri ya Ks)

Ni muhimu kutaja kuwa lugha ya Ks ina vitenzi vilivyokopwa kutoka lugha zingine ambavyo havichukui vokali /a/ mwishoni kama katika mfano 2.

2) Sameh-e, tub-u, hubir-i, salim-u, nk.

Vitenzi vikuu katika lugha hizi mbili, vinaweza kuchukua viambishi tofauti kati ya mzizi na irabu [a] ikiwa kitenzi hicho kinachukua kauli tofauti, tazama mfano wa;

3) Ks. Mama a-li-m-l-ish-a mtoto.

Ek. **βaβa n-a-mo-rager-et-i-e omwana.**

Mama kiy. -kip. Nafsi 3 umoja — yambwa – mzizi T la – wkt pita - kauli ish-kiishio kb. ngeli I mtoto

(Mama alimlisha mtoto)

Kutokana na mifano hii, tunaweza kuona kuwa, mfano wa Ks, kitenzi {l-}

kimeongezewa [-ish-] kati ya mzizi {l-} na {-a}. Hata hivyo, mwishoni

kumedumisha ile irabu {-a}. Tukitazama mfano wa Ek, tunaweza kuona mzizi wa

kitenzi {rager} umeongezewa mofimu {-et-i-e} ambapo mofimu ya mwisho ni [-e], [i] ni ya kuonyesha kauli ya kutendesha kama ile ya Ks ambayo ni {-ish}, na {-et} ni mofimu ya wakati uliopita kwa lugha ya Ek. Tutaeleza zaidi katika sehemu ya mofolojia ya kitenzi. Pia, mfano wa 3 huonyesha idadi, ambapo katika Ks mofimu {-a} na Ek {n-a}, ambazo hurejelea hali ya umoja nafsi ya tatu katika ngeli ya 1.

Vitenzi visaidizi ni vitenzi vinavyosaidia vitenzi vikuu kutoa maana kamili.

Vitenzi visaidizi hushirikiana na vitenzi vikuu kufafanua maana ya kitendo kinachokusudiwa katika Ks na Ek ili kukamilisha uarififu wake.

Vitenzi visaidizi hubeba mofimu za njeo, (au hali), idadi, kundi la ngeli na hali ya uyaakinishi au ukanushi, katika sentensi kama vitenzi vikuu. Kwa hiyo, vitenzi visaidizi husaidia kutofautisha dhamira, hali na kauli (Mohammed 2001: 81)

Katika lugha ya Ks na Ek, vitenzi visaidizi hutangulia vitenzi vikuu, na hufuatwa na vitenzi vikuu. Hata hivyo, lugha ya Ek, inaweza kuchukua muundo mwingine ambapo kitenzi kisaidizi 'kuwa' kinaweza kufuata kitenzi kikuu kinyume na Kiswahili sanifu. Kwa mfano;

4) Ks. (i) A-li-kuwa a-na-som-a kitabu.

Ek. (ii) **A-renge go-som-a ege-taβu.** (Tafsiri ya Ks)

Kip. Nafsi 3 umoja -wkt pita -Ts kuwa kb. Hali - mzizi T soma - kiishio kb. Ngeli 7
mzizi kitabu

(Alikuwa anasoma kitabu)

(iii) **η-go-som-a a-renge egetaβu.**

kiy-hali kuendelea-mzizi T soma-kiishio kip. nafsi 3- umoja -wkt pita -Ts kuwa Kb ngeli
7 kitabu.

(kusoma alikuwa kitabu.)

Mfano 4) (iii) unaonyesha uwezekano wa lugha ya Ek, kitenzi kisaidizi kufuata kitenzi kikuu, ambapo kitenzi kikuu kinachukua nafasi ya kwanza kimuundo. Ingawa kitenzi kisaidizi 'kuwa' (-reng) hutangulia kitenzi kikuu, katika lugha ya

Ek. huhitaji visaidizi vingine kama 'nigo' ili kuonyesha wakati kamili. Kw^a
mfano.

5. (i) **Omo-rugi nigo a-enge ko-ruga.**

kb. Ngeli 1 –pika hali kuendelea kip. Nafsi 3 umoja – wkt pita -Ts kuwa
kip. Hali – pika.

(Mpishi alikuwa anapika)

'nigo' huonyesha hali ya kuendelea kwa kitenzi na hukanushwa pamoja na kuwa
kama katika;

(ii) **Omo-rugi t-a-enge ko-ruga**

kb. Ngeli 1 –pika kb. Kukana – kip. Nafsi 3 umoja – wkt pita- Ts kuwa kb. Hali – mzizi T pika-

(Mpishi hakuwa anapika)

Vitenzi visaidizi vingine vyote hutangulia vitenzi vikuu sawa na lugha ya Ks.

Mifano ya vitenzi visaidizi katika lugha hizi ni kama; Ks (Ek): Weza (-nyara), -
kuja (-che), -taka (-gania), kwenda (-genda) kwisha (ikire), kuwa (-reng) n.k.

Tazama katika sentensi.

6) (i) U-na-weza kwenda sokoni?

(ii) **N-o-nyar-e ko-gend-a e-chiiro?**

Kiy. –kip. Nafsi 2 umoja –Ts weza-kiishio ngeli 15 – mzizi T enda –kiishio kb ngeli 9
soko.

(Unaweza kwenda sokoni)

(iii) Mgonjwa a-na-taka ku-nyw-a uji.

(iv) **Omo-rwaire n-a-gan-et-i-e ko-nywa e-rongori.**

Kb. Ngeli 1 –mgonjwa kiy –kip. Nafsi 3 umoja – Ts taka – kiishio kb. Kis^o
– mzizi T kunywa uji.

(Mgonjwa anataka kunywa uji)

(v) Nyumba hii i-ta-ku-j-a kuangukia.

(vi) **E-Flomba eye n-e-che ko-gwa.**

Kb. Ngeli 9 – nyumba kip. Ngeli 9 – kionyeshi kiy-Kip ngeii 9 – Ts kuja –
wkt ujao-kiishio kb. Ngeli 9.

(Nyumba hii itakuja anguka.)

Katika lugha zote ukanushi hufanyiwa vitenzi visaidizi ili kuonyesha kukana kwa vitenzi vikuu. Tazama ukanushi wa mifano ya 6 hapo juu.

7) (i) Hu-wez-i kwenda sokoni?

(ii) **T-o-ko-nyara ko-genda echiro?**

Kb. Kukana- kip. Nafsi 2 umoja- hali kuendelea- Ts weza kb. Kiso- mzizi T enda sokoni.

(iii) Mgonjwa h-a-tak-i ku-nywa uji.

(iv) **Omo-rwarire t-a-gan-et-i ko-nywa eroЛgori.**

Kb. Ngeli 1-mgonjwa kb. Kukana- kip. Nafsi 3 umoja – Ts taka – kiishio kb. Kiso – kunywa uji.

(Mgonjwa hataki kunywa uji)

(v) Lumba hii ha-i-ta-ku-j-a ku-anguka.

(vi) **Е-Лomba e-ye t-e-go-ch-a ko-gwa.**

Kip. Ngeli 9 –nyumba kip. Kionyeshi kb kukana – kip ngeli 9 – hali ya kuendelea – Ts. Kuja – kiishio kb. Kiso - anguka.

(Nyumba hii haitakuja kuanguka)

3.1.2 Ulinganishi wa vitenzi vielekezi na visoelekezi.

TUKI (1990 : 57) wanaeleza kuwa kitenzi elekezi ni kitenzi ambacho hakiwezi kujitosheleza kimawasiliano bila yambwa. Vitale (1981: 24) naye anaeleza kuwa uelekezi hutegemea idadi na aina ya KN ambacho kitenzi huchukua. Kwa mfano, anasema kuwa, sentensi inaweza kuchukua KN mbili, moja ikiwa ni kiima na nyingine yambwa. Tungependa kuongezea kuwa uelekezi wa kitenzi huhusishwa zaidi na KN kilicho na uamilifu yambwa kuliko kiima, si kama anavyodai Vitale. Yambwa inaweza kuwa yambwa tendwa au yambwa tendewa. Lugha ya Ks na Ek kama lugha za Kibantu, zina uwezo wa kuchukua yambwa kwa vitenzi elekezi. Vitenzi visoelekezi ni vile ambavyo havihitaji yambwa ili kutoa urejeshi kamili, bali vinaweza kufuatwa na vielekezi au kirai kielekezi (KE). Kwa mfano.

8. Ks. Mtoto alilala chumbani siku nzima.

Ek **Omw-ana a-ka-rara nyomba ri-tuko ri-gima.**

Kb. Ngeli 1 mtoto kip. Nafsi 3 umoja – wkt pita-mzizi T lala nyumbani kb.

Ngeli 5 siku kip. Ngeli 5 nzima.

(Mtoto alilala chumbani siku nzima)

Sentensi hizi zimetumia kitenzi kisoelekezi ‘lal-a’ (rara) ambacho kinafuatwa katika lugha zote na KE kinachoongozwa na kielezi (E) cha mahali ‘chumbani’.

Mbali na kutochukua KN (yambwa), vitenzi visoelekezi haviwezi kugeuzwa kwa kauli ya kutendwa kama vitenzi vielekezi. Hata hivyo, kuna uhusiano wa kisarufi kati ya vitenzi vielekezi na visoelekezi katika lugha ya Ks na Ek. Vitenzi vielekezi vinaweza kuondolewa uelekezi wao vikawa visoelekezi, kwa mfano wa;

9) Ks (i) M-toto a-me-funga dirisha. (elekezi)

(ii) Dirisha li-me-fungika. (sielekezi)

Ek (i) **Omw-ana o-siek-ir-e etirisa.**

Kb.ngeli 1 – mtoto kip. Nafsi 3 – mzizi T funga – hali timilifu-kiishio kb.

Ngeli 9 dirisha.

(Mtoto amefunga dirisha)

(ii) **E-tirisa ya-siek-ek-ir-e.**

Kb. Ngeli 9 dirisha kip. Ngeli 9 mzizi T funga -kauli tendeka – hali

timilifu kiishio

(Dirisha limejifunga.)

Sentensi za (i) katika Ks na Ek ni elekezi kwa sababu zinachukua KN ambacho kiuamilifu ni yambwa. Sentensi za 10 (ii) si elekezi kwani hazichukui yambwa. Ingawa kitenzi ‘funga’ ni elekezi, kinaweza pia kuwa si elekezi kwa kuongezewa mofimu [-ik-] kwa Ks na {ek} kwa Ek kwa kunyambuliwa. Vilevile, vitenzi visoelekezi vinaweza kufanywa kuwa elekezi kwa kuongezewa mofimu fulani kimofolojia. Mara nyingi huwa ni viambishi tamati vinavyoongezwa ili kuzalisia vitenzi vyenye maana tofauti katika sentensi mfano:

- 10) Ks (i) M-toto a-me-la-la
(ii) Mama a-me-m-lal-ish-a mtoto.

Ek (i) **Omw-ana o-rar-ir-e**

Kb. Ngeli 1 mtoto kip. nafsi 3 umoja – mzizi T lala – hali timilifu – kauli ish – kiishio.

(Mtoto amelala)

(ii) **βaβa o-mo-rar-ir-i-e omwana.**

Mama kip. Nafsi 3 umoja- kip yambwa- mzizi T lala – hali timilifu – kauli ish – kiishio kb. Ngeli 1 mtoto.

(Mama amemlalisha mtoto)

Viambishi vya hali ya kutendesha vimefanya sentensi zisizoelekezi kuwa elekezi

11 (i) kwa kutumia viambishi {-esh-} katika Ks na {-i-} katika Ek. Ni bayana kutokana na mifano hii kuwa vitenzi elekezi na visoelekezi vya lugha hizi vinafanana shilingi kwa ya pili.

3.1.3 Ulinganishi wa vitenzi vishirikishi vya Ks na Ek.

Vitenzi vishirikishi ni aina ya vitenzi ambavyo havionyeshi kutendeka kamili kwa kitendo bali huonyesha hali. Vitenzi hivi havina uarifu kamili bali hutumia vijalizo ili kukamilisha uarifu wao kimaana. Bila vijalizo, vitenzi vishirikishi havina maana kamili. Mohammed (2002:85) anasema kuwa uamilifu wao mkuu ni kuhusisha vipashio vya kishazi, hasa kiima na kijalizo.

Vitenzi vishirikishi huwa vya aina mbili katika lugha ya Ks na Ek. Kwanza, kuna vishirikishi vya 'kuwa' na pili vishirikishi vya 'kuwa na'. Lugha ya Ks huwa na vishirikishi vya 'kuwa; vingi kuliko lugha ya Ek. Mifano ya vishirikishiki vya kuwa katika Ks ni kama;ni, si, ndi- li-, -mo, yu, u, si. na kadhalika. Mifano katika sentensi;

- 11 a (i) Halima ndiye mganga.
(ii) Yohana ni mwizi wa kutajika.

- (iii) Yohana si mwizi.
- (iv) Chifu yumo afisini
- (v) Aliye mtundu huadhibiwa.

Mifano ya vishirikishi vya 'kuwa' katika lugha ya Ek ni kama; ni-, ti-, -re, nao, Mifano katika sentensi.

11b (i) **Omw-arimu o-yo no-muya.**

Kb. Ngeli 1 mwalimu kip nafsi 3 umoja kionyeshi Tsh – mzuri.

(mwalimu huyu ni mzuri)

(ii) **Omw-arimu o-yo t-a-ri muya**

Kb. Ngeli 1 mwalimu kip nafsi 3 umoja – kionyeshi kb. Kukana –

kip. Nafsi 3 umoja – hali kutokuwa mzuri

(Mwalimu huyu si mzuri)

Kwa jumla, vitenzi vishirikishi huchukua vijalizo vya aina mbalimbali kama vile kishazi nomino, vivumishi, visoukomo kama inavyoonekana katika mifano ya 11 (a) na (b).

Aina ya pili ya vishirikishi ni vishirikishi vya 'kuwa na' au 'pamoja na' Mifano katika Ks na Ek ni kama;

12. Ks: (i) Maria ana kitabu
- (ii) Juma alikuwa na Maria
- (iii) Walio na akili ni wachache.

Ek: (i) **Maria n-a-re n-ege-taβu.**

Maria kiy. Kip. Nafsi 3 umoja – Tsh kuwa na –kiy -kb. Ngeli 7 kitabu

(Maria ana kitabu)

(ii) **Chuma m-ba-rengē na Maria.**

Chuma kiy- kip nafsi 3 wingi -- Tsh kuwa na Maria.

(Juma alikuwa na Maria)

(iii) **Aβa-re n-echisemi n-aβa-ke.**

Kip. Nafsi 3 wingi – Tsh kuwa na kb. ngeli 10 akili ni – nafsi 3 wingi -- chache.

(Walio na akili ni wachache)

Sentensi hizi zinaonyesha hali ya 'kuwa na' lakini sentensi za (ii) zinaweza pia kumaanisha 'pamoja na'.

3.1.4 Ulinganishi wa vitenzi visoukomo katika Ks na Ek

Vitenzi visoukomo ni vile vitenzi ambavyo havionyeshi hatima ya kutendeka kwao. Vitenzi visoukomo havina vipengele vya wakati na nafsi kiima kama vitenzi ukomo lakini vinaweza kuchukua kiambishi cha yambwa. Aghalabu vitenzi visoukoma hudhihirika kwa kiambishi awali {ku-} katika lugha ya Ks, na kiambishi. {go-/ ko-} katika lugha ya Ek. Kwa mfano.

13 Ks. Ku-cheza mpira

Ek. **Ko-gosoria om-opir-a**

Kb. Kiso-mzizi T cheza – kiisio kb. Ngeli 3 mpira

(Kucheza mpira)

Tukumbuke kwamba vitenzi visoukomo vina sifa za aina mbili za kuwa vitenzi na sifa za kuwa nomino. Kama vitenzi, vitenzi visoukomo vinaweza kunyambuliwa kama vitenzi vingine kwa mfano

Ks; kulimisha, kulimia kulimika, kulimiwa n.k.

Ek; okoremia, okoremera, okoremeka, okoremerwa n.k.

Pia huchukua yambwa kama;

14. Ks Ku-m-pik-i-a mama chakula.

Ek. **Ko-mo-rose-ri-a βaβa endagera.**

Kb. Kiso-kip yambwa -mzizi T pika - kauli tendea – kiishio mama chakula.

(Kumpikia mama chakula)

'Mama chakula' na 'βaβa endagera' ni yambwa tendewa na tendwa katika lugha zote mbili. Vitenzi visoukomo vya Ks and Ek hukanushwa kama vitenzi vingine vyovyote. Katika kukanusha Ks huchukua kiambishi {-to-} baada ya {ku-} na Ek huchukua {t-} baada ya {ku-/go-}. Tazama mfano 15.

15. Ks. A-me-shauri-w-a ku-to-shiriki ulevi.

Ek. **O-semi-ir-iw-e go-t-a-tind-a**

Kip. Nafsi 3 umoja – mzizi T shauri – hali – kauli iw – kiishio kb. Kiso kukana – kip. Nafsi 3 umoja. Mzizi T ulevi kiishio

(Ameshauriwa kutoshiriki ulevi)

Vitenzi visoukomo kama vitenzi vingine, huwa maneno makuu au vichwa vya KT, katika lugha hizi mbili. Kwa mfano.

16 Ks. Fatuma a –me-end-a ku-mw-imbia Raisi.

Ek. **Fatuma o-ch-ir-e ko-mo-ter-er-a omo-gambi**

Kip. Nafsi 3 mzizi T enda – hali timilifu – kiishio kb. Kiso. Kip. Yambwa – mzizi T imba – kauli tendea – kiishio raisi

(Fatuma ameenda kumwimbua Raisi)

Kama vitenzi vielekezi, vitenzi visoukomo vinachukua KN chenye uamilifu wa yambwa au yambwa tendewa. Vikitumiwa pamoja na ‘kuwa’ vinachukua vijalizo katika lugha hizi mbili. Hebu tazama mfano; 1& (i)-(iv).

17. Ks (i) Ku-m-nunuli-a m-toto ki-tabu.

Ek (ii) **Ko-gor-er-a omw-ana ege-taβu.**

Kb. Kiso-mzizi T nunua- kauli tendea – kiishio kb. Ngeli 1 mtoto kb ngeli 7 - kitabu

(Kumnunulia mtoto kitabu)

Vilevile vitenzi visoukomo vinaweza kuchukua vielezi vya aina yote.

18 Ks. A-li-faulu kwa ku-soma kwa bidii

Ek. **A-et-et-e ase ogo-soma nomokia.**

Kip. Nafsi 3 umoja- mzizi T faulu -wkt pita- kiishio Kwa kb. Kiso.- mzizi soma kiishio kwa bidii.

(Alifaulu kwa kusoma kwa bidii)

Kitenzi kisoukomo huwa ni kitenzi kikuu cha kileksika pale ambapo kinatumika na kitenzi kisaidizi chochote. Ni muhimu kutaja kuwa kama vitenzi vingine, kitenzi hiki hakichukui viambishi vya njoo na nafsi.

Aidha, pale ambapo kitenzi kisoukomo hutumika bila {ku-} kwa kuonyesha hali ya kutokoma kwa kitendo, katika lugha ya Ks hutumia vitenzi visaidizi na kitenzi kisoukomo hutumiwa bila mofimu {ku}. Kwa mfano;

19. Mtoto ataka soma.

Mtoto aweza tembea.

Vitenzi visoukomo katika lugha ya Ks na Ek vinafanana na vimechukua muundo mmoja ulio sawa. Kufikia hapa, tumejaribu kuonyesha aina za vitenzi katika lugha ya Ks na Ek kiulinganishi. Kwa jumla vitenzi katika lugha hizi huwa na ruwaza hii.

- (i) Vitenzi vinavyochukua yambwa.
- (ii) Vitenzi vinavyochukua yambwa mbili.
- (iii) Vitenzi visivyochukua vijalizo.
- (iv) Vitenzi visivyochukua yambwa au kijalizo.
- (v) Vitenzi vishirikishi vinavyochukua kiima kijalizo.

3.2.0 Mofolojia Ya Vitenzi Vya Ks Na Ek

Mofolojia ya vitenzi vya lugha za Kibantu huwa ni changamano wanavyodai wanaisimu wengi (Polome, 1967, Guthrie 1971, Myachina 1981).

Kimsingi, muundo wa vitenzi kwa jumla huwa na maumbo mawili; mzizi wa kitenzi na viambishi vya mzizi. Mzizi huwa ni mofimu funge bila viambishi na viambishi vilevile huwa funge bila mzizi.

Mzizi wa kitenzi huweza kujengeka kifonetiki kwa vokali (v) au vokali konsonanti (vk), Vokali konsonanti konsonanti (vkk), konsonanti nusu konsonanti na vokali (kkv) na miundo mingine mingi. kama

2

KS

- i) V kama kwa u-a, o-a,
- ii) VK kama um-a, it-a, ib-a n.k.
- iii) VKK kama kwa kwa imb-a, end-a, ach-a, n.k.
- iv) KV kama vile li-a, tu-a, za-a,
- v) KVK mifano kama pig-a, pik-a, som-a, n.k.

- vi) K K/2 V kama twa-a,
- vii) KVKKV kama tembe-a, kimbi-a, n.k.
- viii) KKVKKVKV kama changanua, n.k.

Ek Pia huwa na muundo huu wa kifonetiki:

- i) V kama a-a (kuchuna mboga ua majani yoyote),
- ii) VVK kama a:k-a (piga), e:ni-a, (kuweka mahali panapofaa)
- iii) VK kama iβa, it-a (piga) et-a (pita).
- v) KVK kama tom-a (tuma), tuβ-a, (vunika),n.k.
- vi) KVVK kama teer-a (imba), reet-a (leta), tiir-a (ende juu).
- vii) KK/2VK kama twom-a (sukuma), twor-a (paza sauti).
- viii) KVKVKKVK kama tirimbok-a (teremka), nk
- ix) KVKVK kama simek-a (panda), samor-a (vuna) n.k

Maumbo ya kifonetiki katika vitenzi vya lugha hizi yanafanana katika mzizi wa kitenzi. Hata hivyo, muundo wa VVK hautumiki sana katika Ks kama katika Ek.

Viambishi katika vitenzi huwa vya aina mbili.

- (i) Viambishi vya uambishaji (inflectional affixes).
- (ii) Viambishi vya unyambuaji (Derivative affixes).

3.2.1.0 Uambishaji Wa Vitenzi Vya Ks Na Ek

Schemu iliyopita tumejaribu kuonyesha umbo la mzizi, na sasa umbo la viambishi vya kuambishwa katika lugha hizi huwa ni mofimu zinazowakilisha maumbo yafuatayo katika lugha ya Ks na Ek pamoja.

1. Kiambishi cha kukanusha.
2. Kiima (kiambishi cha kiima)
3. Kiambishi cha wakati / hali
4. Kiambishi cha yambwa.
5. Kiambishi cha urejeshi. (o-rejeshi)
6. Kiambishi cha kujirejelea.

7. Kiambishi cha mwisho (kiishio)

8. Kiambishi cha usoukomo.

Viambishi hivi hujipanga kutoka kushoto kuelekea kulia katika kitenzi. Huwa havitokei kwa pamoja katika kitenzi bali huwa vimechukua ukubaliano wa aina fulani kati ya kitenzi na nomino. Ikiwa sentensi au kirai kiko katika hali ya uyaikinishi, huwa kiambishi cha kiima huja mwanzoni lakini katika hali ya ukanushi, kiambishi cha kukanusha huchukua nafasi ya kwanza katika lugha hizi. Lakini pia tukumbuke kwamba, ikiwa kitenzi kiko katika hali ya mazoea katika lugha hizi, viambishi vya hali ya mazoea huchukua nafasi ya kwanza ambayo hufuatwa na kiambishi cha kiima. Kwa mfano

7. Ks. Mwanafunzi hu-som-a

Kb hali-mzizi T - kiishio

Ek **Omworokigwa a:soma.**

Mwanafunzi kb. hali- kip – mzizi T som – kiishio.

(Mwanafunzi husoma)

Maelezo zaidi ni katika viambishi vya njeo.

3.2.1.1 Viambishi vya ukanushi katika Ks na Ek

Lugha ya Ks ina viambishi vya kukanusha ambavyo ni {ha-} na {si-} vinachukua nafasi ya kwanza katika kitenzi na {-i} huchukua nafasi ya mwisho badala ya {-a} ikiwa kitenzi kiko katika hali ya mazoea au wakati uliopo au unaoendelea, kwa mfano;

24. (i) Waimbaji wa-na-imb-a

Waimbaji ha-wa-imb-i

(ii) Mimi hu-som-a

Mimi si-som-i.

(iii) Wewe hu-imb-a

Wewe hu-imb-i.

Kiambishi {hu-} katika sentensi ya tatu ni kile cha {ha-} isipokuwa irabu /a/ imedondoshwa kwa kufuatwa na irabu /u/ ili kuepuka kufuatana kwa vokali, muundo unaopendelewa.

/ha+u+imb-i/ → [Huimbi]

Kiambishi cha kukanusha katika lugha ya Ek ni (ti-) na alomofu zake ni {ta-} na {t-}. Kiambishi cha kukanusha huchukua nafasi ya kwanza katika kitenzi na hufuatwa na kiambishi cha kiima. Mofimu hii ya ukanushi katika Ek, hubadilikabadilika kwa sababu za kifonolojia hasa katika ngeli ya 1. Kwa mfano, ikiwa [ti-] inafuatwa na kiwakilishi nomino chenye vokali tu huwa kiambishi hiki cha kukanusha hudondosha irabu yake /i/ na kuchukua ile ya kiima. Athari hizi hutokea katika dhamira arifu, agizi na tegemezi: Tazama mifano:

25. (i) **Tera (-imba)**

T-o-ter-a

kb. kukana –kip nafsi 3 umoja – mzizi T imba – kiishio.

(Usiimbe)

(ii) **O-som-e (usome)**

T-o-som-a

kb. kukana – kip nafsi 3 umoja – mzizi T soma - kiishio

(Uisome).

Kama Ks, Ek hukana irabu ya mwisho ya kitenzi katika wakati uliopo na ule wa kuendelea, kwa kutumia irabu {-i} badala ya {-e} Mfano.

26. (i) **N-ko-rem-a-r-e.**

Kiy. –hali kuendelea – mzizi T lima – kip nafsi 3 umoja – hali - kiishio

(Analima)

T-a-ri-ko-rem-a.

Kb. kukana-kip nafsi 3 umoja – hali iliyopo- hali kuendelea – mzizi T lima kiishio

(Halimi)

(ii) **N-ko-rem-a-βa-re**

Kiy. – hali kuendelea – mzizi lima - kiishio – kip nafsi 3 wingi – hali.

(Wanalima)

Ti-ba-ri-ko-rem-a.

Kb. kukana – kip nafsi 3 wingi – hali iliopo - hali kuendelea – mzizi T lima - kiishio.

(Hawalimi.)

Kiambishi cha kukanusha kinapochukua nafasi ya kwanza, kiambishi cha uyaikinishi huwa hakipo tena katika lugha ya Ek. Pia, kiambishi cha wakati uliopo {-re} ambacho huwa mwishoni mwa kitenzi katika hali yaikinishi wakati wa kukanusha hubadilisha nafasi yake na kuchukua nafasi ya kufuata kiambishi kiwakilishi kiima ambayo ni ya tatu, tokea mwanzo wa kitenzi na /e/ hubadilika na kuwa /i/. Kiambishi {ko} au {go} cha hali ya kuendelea kwa kitenzi huchukua nafasi ya pili baada ya kiambishi kiyakinishi, lakini katika kukanusha huchukua nafasi ya nne. Kwa jumla, ukanushi katika wakati uliopo wa hali ya kuendelea katika lugha ya Ek, viambishi vya kitenzi hupitia mabadiliko mengi.

Katika kishazi kirejeshi, kiambishi cha kukanusha [ti-]katika lugha ya Ek, huchukua nafasi ya pili baada ya kiambishi cha kiima. Kwa mfano.

27. (i) **Oria ogwete.** (ambao ulianguka)

Oria o-t-a-gwete. (ambao hukuanguka)

Sheria 1.

/ u / → w / - e

/ o-gu-cte / → [ogwete]

Tunaweza kusema kuwa viambishi vya kukanusha katika lugha ya Ks huwa havibadilishi nafasi zao kama kiambishi cha ukanushi cha Ek, kutegemea mazingira ya utungo.

3.2.1.2

Kiambishi cha kiima

Vitenzi vyote katika lugha hizi hubainika kwa upatanisho kati ya kiima cha sentensi au kirai kuambatana na kundi la ngeli ya nomino iliyohusishwa katika KN. Katika sura ya pili, sehemu ya 2.2 tulitoa uainishaji wa ngeli kisintaksia kwa kuangalia upatanishi kati ya KN na kitenzi. Kila nomino hupatanishwa na kitenzi kwa kutumia kiambishi kiwakilishi nomino. Nomino za ngeli huwa na vipatanishi kiima viwili (umoja na wingi) isipokuwa ngeli ya 1 ambayo upatanishi wake unaweza vilevile kuchukua viwakilishi nafsi. Kwa mfano Ks.

21. Ngeli 1 (i) M-toto a-me-it-w-a.

kb. Ngeli 1-mtoto kip. Nafsi 3 umoja – hali – mzizi T – kauli tendwa - kiishio

(ii) U-me-it-w-a u-end-e.

Kip. Nafsi 2 umoja – hali –mzizi T – kauli tendwa – kiishio kip. Nafsi 2-mzizi T- kiishio

(iii) Ni-me-it-w-a ni-end-e.

Kip. Nafsi 1 umoja –hali - mzizi T- kauli tendwa-kiishio kip. Nafsi 1-mzizi T – kiishio.

Ngeli 3/4 (i)M-ti u-me-anguk-a

Kb. Ngeli 3-mti kip.ngeli 3 umoja – hali – mzizi T – kiishio.

(ii) Mi-ti i-me-anguk-a.

Kb. Ngeli 4 - miti kip. Ngeli 4 wingi –hali –mzizi T – kiishio.

Ngeli 9/10 (i) Ngao i-me-tobok[a

Kb. Ngeli 9 kip. Ngeli 9- hali – mzizi T - kiishio

(ii) Ngao zi-me-tobok[a.

Kip. Ngeli 10 – hali – mzizi T – kiishio.

Tunaona kuwa ngeli ya 1 ingawa haijaandikwa kwa wingi, tayari ina vipatanishi vitatu {a-u-ni-} ambavyo vinategemea nafsi. Ngeli ya 3/4 , ina viambishi kiima viwili {u-} na {i-} na ya 9/10 ina {i-} na {zi-}.

Lugha ya Ek ina kiambishi cha kwanza ambacho ni {n-} tofauti na Ks. Mfano:

22. (i) **Omo-iseke n-a-som-et-e.**

kb. Ngeli 1 – msichana kiy. –kip nafsi 3 umoja -- mzizi T soma – wkt pita – kiishio
(Msichana alisoma)

(ii) **Aβa-iseke m-ba-som-et-e**

kb ngeli 2 – wasichana kiy. Kip. nafsi 2 wingi – mzizi T soma – wkt
pita – kiishio.

(Wasichana walisoma)

Kiambishi hiki hupatikana pia katika lugha zingine za Kibantu kama Kikikuyu, Kikamba, Kimbeere n.k. Ni muhimu kufafanua kuwoko kwa kiambishi hiki kabla ya kuendelea.

Perez (1986:17) anaita kiambishi hiki fokasi. Anasema

ingawa [ni] inatumika kama fokasi au kibainishi cha kutilia mkazo, pia hutumika katika sentensi arifu ingawa wazungumzaji hawatilii mkazo kuwako kwake (TY).

Tunapochunguza zaidi kuhusu fokasi Dik (1987:210) anasema kuwa, fokasi huwa na matumizi mbalimbali. Tunachukulia fokasi kuwa vipashio vinavyobainisha vijenzi vingine zaidi katika kishazi. Hata hivyo, kiambishi hiki katika lugha ya Ek hakionyeshi fokasi bali kinaonyesha hali ya uyaikinishi katika nyakati na hali fulani. Mbali na Perez, tumekiita kiambishi kiyakinishi (kb. kiy). Katika lugha ya Ek, huchukua nafasi ya kwanza katika vitenzi vinavyochukua upatanishi kwa wakati uliopo au hali inayoendelea, wakati ujao, wakati uliopita isipokuwa kwa hali timilifu na hali mazoea. Kiambishi kiyakinishi huchukua mabadiliko ya kimofonemiki na kuwa [m] katika kufuatwa na /β/ ya mghuno mkwaruzo. Kwa mfano.

/ N + βareme / → [mbareme] (watalima).

Sheria 2 / n / → m / - β

Mabadiliko haya ya /n/ ambayo ni konsonanti ya ufizi kubadilika na kuwa /m/ ya midomo yanatokea kwa sababu ya usilimisho wa nazali. Mabadiliko mengine ni ya /β/ ya mkwaruzo kuimarika kuwa /b/ ya mtuo.

Baada ya kiyakinishi katika Ek, kiambishi kinachofuata hutegemea na wakati wa kitenzi hicho. Inawezekana, kiyakinishi kikafuatwa na kiambishi cha kiima kwa wakati uliopita au katika hali ya kuendelea, na kwa hali timilifu, vitenzi huwa havina kiambishi kiyakinishi mwanzoni bali kiima huchukua nafasi ya kwanza, isipokuwa nafsi ya 1 umoja ambayo huchukua kiyakinishi. Tazama mifano hii ya Ek.

23. i) **Mame n-a-ch-et-e.**

Mjomba kiy- kip nafsi 3 umoja – mzizi T ja – wkt pita - kiishio

(Mjomba alikuja.)

ii) **Aβa-na m-ba-rem-et-e.**

kb. ngeli 2 – watoto kiy -kip nafsi 3 wingi- mzizi T lima – wkt pita - kiishio

(Watoto walilima.)

iii) **Omo-iβori o-rem-ir-e.**

kb. ngeli 1 mzazi kip nafsi 3 umoja – mzizi T lima – hali – kiishio.

(Mzazi amelima.)

iv) **Tata n-ko-rem-a-r-e.**

Baba kiy- hali kuendelea – mzizi T lima – kip nafsi 3 umoja – hali .

(Baba analima.)

Sentensi ya 23 (i) na (ii) ni za wakati uliopita na kama tunavyoona vitenzi vimepatanishwa kwa kuchukua kiambishi kiyakinishi na baadaye kiambishi cha kiima, ilhali sentensi ya 23 (iii) haina kiambishi kiyakinishi na kitenzi kiko katika hali timilifu. Na sentensi 23 (iv) iko katika wakati uliopo, wa hali ya kuendelea, ambapo kiambishi kiyakinishi kiko mwanzoni mwa kitenzi na kiima kinachukua nafasi ya pili toka mwisho.

Lugha ya Ks ina mpangilio mahsusi wa kiambishi cha kiima ambapo kinachukua nafasi ya kwanza katika kitenzi katika kupatanisha nomino na kitenzi. Lugha ya Ek mpangilio wake ni changamani kwani kiambishi cha kiima kinaweza kuchukua nafasi ya kwanza katika kitenzi, ya pili au ya pili toka mwisho.

24. (i) **Omo-te o-gu-er-e.**

kb. ngeli 3 – mti kip- mzizi T anguka – hali – kiishio

(Mti umcanguka.)

(ii) **Aβa-ana m-ba-gend-e.**

kb. ngeli 2 – watoto kiy. – kip. nafsi 3 wingi – wkt pita - mzizi T enda – kiishio.

(Watoto walienda .)

(iii) **Aβa-ana n-ko-gend-a-βa-r-e.**

kb. ngeli 2 watoto kiy – hali kuendelea – mzizi T enda – kiishio – kip. nafsi 3 wingi – hali- kiishio.

(Watoto wanaenda)

3.2.1.3 Viambishi vya Njeo na Hali katika Ks na Ek

(a) Njeo

Kimsingi, huwa kuna njeo tatu ambazo hurejelea wakati kitendo fulani hufanyika. Njeo hizo ni za wakati uliopo, wakati uliopita na ujao. Njeo za lugha ya Ks na Ek kimuundo huwa , ni konsonanti na vokali au vokali peke yake. Viambishi vya njeo katika lugha ya Ks, hufuata viambishi vya kiima, katika lugha ya Ek baadhi ya viambishi huchukua nafasi ya mwisho au ya pili toka mwisho, na baadhi hufuata kiambishi kinachowakilisha kiima.

(i) Njeo ya wakati uliopo

Lugha hizi viambishi vya wakati uliopo, huonyesha kuwa tendo linaendelea kutendeka wakati huo msemaji anapoongea. Lugha ya Ks ina kiambishi {na-} ambacho pia hufanya kazi kama kiambishi cha hali ya kuendelea. Kiambishi kingine ni {a-} ambacho kina mjadala mkali, ambapo wanaisimu wengine husema kuwa ni kiambishi cha kuonyesha desturi ya kutendeka kwa kitendo, na wengine husema ni kiambishi cha wakati katika lahaja za Kiswahili, ilhali wengine husema

kuwa ni kiambishi cha wakati uliopo. Sisi tunaclewa kwamba, kiambishi {a-} kinaonyesha wakati uliopo na hali ya matendo ya mazoea. Tazama mifano ifuatayo.

28. (i) Mwalimu a-na-fund-ish-a.
(ii) Mwalimu a-fund-ish-a.
(iii) Mama a-pik- a.

Sentensi hizi zinaonyesha vitendo vinatendeka, lakini tukichunguza pia tunaweza kuona desturi ya kitendo katika sentensi ya (ii) na (iii) kitendo cha kufundisha na kupika vinadumu, hufanyika kila wakati. Kiambishi {-na-} kinafuatwa na mzizi wa kitenzi na kiambishi {a-} katika (ii) na (iii) kinatangulia kitenzi, lakini kimedondosha kiambishi cha wakati ambacho kingekitangulia.

Lugha ya Ek nayo, ina viambishi viwili ambavyo vina uamilifu sawa na ule wa Ks. Gesare (1992:116) anaeleza kuwa wakati uliopo na wa kuendelea katika Ek huonyeshwa na kitenzi kikuu na kitenzi kisaidizi cha 'kuwa' ambapo kitenzi kisaidizi huja baada ya kitenzi kikuu katika sentensi yakinishi. Kwa mfano.

29. (i) **Kerubo n-go-som-a-re.**

Kerubo.kb. kiy- hali kuendelea-mzizi T soma – kip nafsi 3 umoja – Ts hali iliyopo.

(Kerubo anasoma)

- (ii) **Aba-gaka nko-rem-a βa-re.**

Kb. ngeli 2 wazee kiy – hali kuendelea – mzizi T lima – kiishio – kip nafsi 3 wingi – hali iliyopo / Ts.

(Wazee wanalima)

Mofimu {-re} inaonyesha wakati uliopo na hali ya kuendelea kwa kitenzi.

Kumbuka [-re} hii inatumika pia kama kitenzi kisaidizi kama tulivyoeleza

mwanzoni mwa sura hii. Kiambishi {-re} kikitumika kuonyesha wakati au hali

huwa kinafuata kitenzi kikuu na huchukua nafasi ya mwisho baada ya kiima.

Muundo wake ni:

Kiambishi kiyakinishi + Kiambishi cha hali ya kuendelea + mzizi wa T + Kiima + njeo

Katika kukanusha, kiambishi cha wakati {-re} hubadilisha nafasi yake kutoka mwishoni mwa kitenzi kikuu na kuingia nafasi ya tatu kwa kufuata kiambishi cha kukanusha {ti-}. Tazama ukanusho wa 30.

30. (i) **Kerubo t-a-ri go-som-a**

Kerubo kb. kukana – kip nafsi 3 umoja – hali ya kuendelea – mzizi T. soma - kiishio

(Kerubo hasomi)

(ii) **Aba-gaka ti-ba-ri ko-rem-a.**

Kb. ngeli 2 wazee kb. kukana – kip nafsi 3 wingi- hali hali kuendelea – mzizi T lima- kiishio

(Wazee hawalimi)

Kiambishi kingine ni {na-} ambacho huonyesha hali ya kuendelea wakati uliopo huku washiriki wa kitendo wakisubiri muda wa kutekeleza tendo lingine katika Ek. Kwa mfano.

31. (i) **Ko-na ko-rem-a.**

Kip. nafsi 2 – wkt uliopo – hali kuendelea – mzizi T lima – kiishio.

(endelea kulima)

(ii) **To-na-go-togi-a**

Kip. nafsi 1 wingi – hali kuendelea – mzizi T shangilia – kiishio.

(Tuendele kushangilia).

(ii) **Njeo ya wakati uliopita.**

Lugha Ks ina kiambishi {li-} cha wakati uliopita kinachoonyesha kitendo kilitendeka muda uliopita. Lugha ya Ek ina viambishi vinne vinavyotambulisha wakati uliopita. Viambishi hivyo ni {-ete-}, {a}, {ka-} na {et}.

Kiambishi {a} kisarufi huonyesha wakati uliopita si muda mrefu uliopita, kwa mfano tendo la jana au juzi kutoka wakati wa kuzungunza. {-et-} huashiria tendo la hivi majuzi au karibuni huku kiambishi hiki kikiwa na toni ya chini. Kikiwa na

toni ya juu huashiria tendo lililotendeka muda mrefu wa miaka fulani iliyopita na {ka-} huonyesha kitendo kwa wakati uliopita haujulikani lakini si mbali sana. Nyakati hizi hutofautishwa kwa kutumia toni kwa viambishi {a-} na {-ete}. Toni ipandapo huonyesha wakati uliopita zamani, ikishuka wakati uliopita karibuni. Tazama mifano ya 33.

Ks (i) Mnunuzi a-li-nunua nguo.

Ek (ii) **Omo-gori n-a-gor-et-e e-yanga.** (hivi karibuni)

Kb. ngeli 1 mnunuzi kiy. kip nafsi 3 umoja – mzizi T nunua – wkt pita – kiishio nguo.

(Mnunuzi alinunua nguo.)

(iii) **Omo-gori n-a-gor-ete e-yanga.** (zamani)

Kb. ngeli 1 mnunuzi kiy. kip nafsi 3 umoja – mzizi T nunua – wkt pita – kiishio nguo.

(Mnunuzi alinunua nguo.)

(iv) **Omo-gori n-á-gor-a e-yanga** (hivi maajuzi).

Kb. ngeli 1 mnunuzi kiy. kip nafsi 3 umoja – wkt pita – mzizi T nunua – kiishio nguo.

(Mnunuzi alinunua nguo)

(v) **Omo-gori n-á-gór-a e-yanga.** (Siku nyingi zilizopita)

Kb. ngeli 1 mnunuzi kiy. kip nafsi 3 umoja -- wkt pita – mzizi T nunua – kiishio nguo.

(Mnunuzi alinunua nguo)

(v) **Omo-gori á-ka-gor-a e-yanga.** (wakati uliopita mrefu)

Kb. ngeli 1 mnunuzi kip nafsi 3 umoja – wkt pita – mzizi T nunua –kiishio nguo.

(Mnunuzi alinunua nguo)

Sentensi moja ya wakati uliopita katika Ks inaweza kuwakilishwa kwa sentensi tano za wakati uliopita kwa lugha ya Ek kama hapo juu. Lugha ya Ek inatofautisha muda wa wakati uliopita, kwa kuzingatia urefu wa vipindi na nyakati zilizopita. Lugha zingine za kibantu, zinazo pia viambishi mbalimbali vya

kutambulisha wakati uliopita. Kama Kimbeere, Maringah (1987:82) anasema ina wakati uliopita wa aina tatu na kiambishi {ira} kwa pamoja husimamia wakati uliopita wowote ule.

Kimuundo, kiambishi cha wakati uliopita katika lugha ya Ks hufuata kiambishi cha kiima. Lugha ya Ek baadhi ya viambishi vya wakati huja mwishoni mwa kitenzi ambapo vinafuata kitenzi kama vile {etc} na kiambishi {-a} kiambishi [ka-] hufuata kiambishi kiwakilishi kiima kama Ks. Tunaweza kufupisha miundo hiyo hivi;

34. Ks. (i) Kiambishi kiwakilishi kiima + njeo + mzizi wa T + Kiishio.
 Ek (ii) Kiambishi kiyakinishi + kiima + mzizi wa T + njeo. ({ete} na {a}).
 M - ba- rem -et-e (Walilima)
 (iii) Kiambishi kiwakilishi kiima + njeo + mizizi wa T + kiishio. ({ka}).
 A- ka- rem -a. (Alilima)

Mara nyingi lugha ya Ek hutumia vielezi vya wakati ili kutofautisha wakati unaozungumziwa mbali na kutumia toni. Kwa mfano 35:

35 **N-a-ch-et-e omwaka oria.**

Kiy- kip. nafsi 3- mzizi T ja- wkt pita – kiishio ngeli 3 mwaka kip.- kionyeshi.
 (Alikuwa mwaka uliopita.)

Katika kukanusha, Ks hufutilia mbali kiambishi cha wakati uliopita badala yake kiambishi {ku-} hutumiwa. Ek kukanusha viambishi vya wakati uliopita hubakia palepale na havibadiliki isipokuwa wakati uliopita si mbali sana ambapo {-e} hubadilika na kuwa {-i}. Mfano ukanusho wa 33.

36. Ks. (i) Mnunuzi ha-ku-nunu-a nguo.
 Ek. (ii) **Omo-gori t-a-go-ret-et-e e-yanga.**
 Kb. ngeli 1 mnunuzi kb. kukana - kip. nafsi 3 umoja -- hali – mzizi T nunua – wkt pita – kiishio nguo
 (iii) **Omo-gori t-a-gor-et-e e-yanga.**
 Kb. ngeli 1 mnunuzi kb. kukana kip. nafsi 3 umoja – hali – mzizi T nunua – wkt pita – kiishio nguo

(iv) **Omo-gori t-a-gor-ete e-yanga.**

Kb. ngeli 1 mnunuzi kb. kukana kip. nafsi 3 umoja – mzizi T nunua – wkt pita – kiishio nguo

(v) **Omo-gori t-a-gor-ete e-yanga.**

Kb. ngeli 1 mnunuzi kb. kukana kip. nafsi 3 umoja – mzizi T nunua – wkt pita – kiishio nguo

Katika kukanusha, viambishi vya wakati uliopita {a} na {ka} hubadilika na kuchukua {ete}. Kwa hii, tunaweza kusema kiambishi {ete} huchukua nafasi muhimu katika wakati uliopita, kukana.

(iii) **Njeo ya wakati ujao**

Kwa Ks kiambishi kinachoashiria njeo ya wakati ujao hufuata kiambishi kiwakilishi kiima kama njeo zingine, na huwakilishwa na kiambishi {ta}. Ek njeo hii huwakilishwa na kiambishi [-e] ambacho kimuundo huja mwishoni mwa kitenzi. Tazama mifano 37.

37) Ks A-ta-lim-a juma lijalo
kip. nafsi 3 njeo – mzizi T – kiishio.

Ek N-a-rem-e echuma egocha.

Kiy. – kip nafsi 3 umoja – mzizi T lima – njeo juma lijalo.

(Atalima juma lijalo.)

Kimuundo, viambishi vya wakati ujao vinachukua nafasi zinazotofautiana. Ks hudumisha muundo 34 (i) kwa njeo zote na Ek wakati huu huchukua muundo wa 34 (ii). Kiambishi kingine ambacho mara nyingi hutumika pamoja na kiambishi cha wakati ujao ni {-ra-}, Kiambishi hiki kina uamilifu kadha wa kadha katika sarufi ya Ek. Kwanza, kikitumiwa pamoja na wakati ujao, huonyesha hali ya kukusudia kutekeleza jambo hilo, wala hakionyeshi wakati ujao. kwa mfano;

38. (i) **M-ba-ra-rem-e**

kip. nafsi 3 wingi – hali – mzizi T lima njeo / kiishio.

(Watalima.)

(ii) N-to-ra-gend-e

Kiy. –kip nafsi 1 wingi –hali mzizi T enda njeo / kiishio.

(Tutaenda.)

Sentensi hizi zinaonyesha nia ya kufanya kitendo hicho wakati ujao ambao haujulikani.

Pili, kiambishi [-ra} kikitumiwa pamoja kwa kutanguliwa na leksika ‘naβo’ (huenda) humaanisha au huonyesha mashaka ya kutenda hilo tendo linalorejelewa kwa wakati ujao. Hamna uhakikisho wa kutekeleza jambo hilo. Kwa mfano.

39) Naβo to-ra-gend-e

Huenda kip. nafsi 1 wingi – hali – mzizi T enda njeo / kiishio

(Huenda tutaenda.)

Kitendo cha ‘kwenda’ huenda kitafanyika au kisifanyike.

Tatu, huonyesha urejelezi wa vitendo kwa kufuatana. Hapa kitendo cha kwanza kutendwa hutendwa ndipo baadaye kifuatwe na kingine. Kwa mfano.

40) O-ra-rager-a o-manye kogenda.

Kip. nafsi 3 umoja – hali – mzizi T la – kiishio kip. nafsi 3 umoja – ndipo hali kuendelea – enda.

(Ule kwanza ndipo huende).

b) Hali

Katika lugha hizi hali kama njeo, ni kategoria ya kisarufi ambayo huonyesha tendo lilitendeka vipi kuambatana na wakati. Huwa kuna hali tatu; hali timilifu, hali ya kuendelea na hali ya mazoea. Hali hizi pia, huhusianishwa na njeo za wakati uliopo, uliopita na ujao. Aghalabu, hali pia huwa iliyokamilika na ile isiyokamilika.

(i) Hali timilifu

Huonyesha kuwa kitendo kimekamilika muda mfupi uliopita kwa siku hiyo inayozungumziwa. Hali hii timilifu kwa lugha ya Ks huwakilishwa na {me-} na katika lugha ya Ek ni {ir-}. Mfano.

41) Ks. A-me-end-a hosipitali.

Ek. **O-chi-ir-e nyagitari.**

Kip. nafsi 3 umoja – mzizi T enda – hali timilifu- kiishio hospitali.

(Amcenda hospitali)

Hali hii timilifu, katika vitenzi vingine matokeo ya kukamilika kwa kitendo hudumishwa na huendelea kuonekana wakati wa kuzungumza. Kwa mfano;

42) Ks Wa-me-simama.

Ek **βa-tenen-ir-e**

Kip. nafsi 3 wingi -mzizi T simama - hali timilifu – kiishio.

(Wamesimama)

Katika mifano hii, hali ya ‘kusimama’ inaendelea kuonekana kwani mhusika anasimama wakati mzungumzaji anapoongea.

Lugha ya Ek mbali na Ks, hutumia sana vielezi vya wakati kuonyesha timilifu muda uliopita. Kwa mfano;

43) **O-sok-ir-e βono iga**

kip. nafsi 3 umoja – mzizi T toka – hali timilifu – kiishio sasa hivi.

(Ametoka sasa hivi)

‘Bono iga’ (sasa hivi) ni kielezi cha kuonyesha kuwa muda uliopita si mrefu.

Katika kukanusha, Ks hutumia kiambishi {-ja-} badala ya {me-}, Ek kiambishi cha kukanusha {ti-} huja kwanza na kufuatwa na kiambishi kiima na ukanushi wa viambishi vya hali timilifu, ambavyo katika ukanushi hubadilisha nafasi yao toka mwisho kuja katika nafasi ya tatu. Vilevile, {e} ya hali hubadilika na kuwa {-a}.

Mabadiliko haya huletwa na vokali ya kiambishi cha kiima kinachofuatwa na kiambishi cha hali timilifu. Tazama mifano hii.

44) Ks (i) Lanina a-me-ku-fa.

Lanina h-a-ja-ku-f-a.

Ek (ii) **Omote o-gu-re.**

Mti kip. ngeli 3- mzizi T anguka – hali timilifu

(Mti umeanguka)

(iii) **Omo-te t-o-ra-gwa.**

Mti kb. kukana kip ngeli 3 umoja – hali – mzizi T anguka.

(mti haujaanguka)

Kimuundo, kiambishi cha hali timilifu katika Ks huchukua nafasi ya pili kama njeo ilhali katika Ek, kinachukua nafasi ya mwisho.

(iii) **Hali ya Kuendelea.**

Hali ya kuendelea katika lugha ya Ks na Ek, huonyesha kuwa kitendo hakijakamilika kutendeka. Hali hii mara nyingi huambatanishwa na njeo katika Ks na Ek. Kwa mantiki hii, hali ya kuendelea mara nyingi huonyeshwa kwa kutumia kitenzi kisaidizi (Ts) 'kuwa' (-reng) huku Ts kikifuatwa na T. Ts huchukua viambishi vya njeo ilhali T huchukua viambishi vya hali. Kwa mfano:

45) Ks (i) Mwalimu a-li-kuwa a-na-fund-ish-a.

(ii) Ahmed a-ta-kuwa a-ki-chez-a,

(iii) A-me-kuwa a-ki-lim-a tangu asubuhi.

EK (i) **Omw-ana n-ko-rer-a a-reng / a-reng.**

Kb. ngeli 1 – mtoto kiy – hali kuendelea – mzizi T lia – kiishio kip. nafsi 3 umoja- Ts kuwa

(Mtoto alikuwa akilia)

(ii) **Omo-remi n-ko-rem-a a-raße**

Kb. ngeli 1 mkulima kiy. – hali kuendelea – mzizi T lima – kiishio kip nafsi 3 umoja – Ts kuwa / hali endelea.

(Mkulima atakuwa akilima)

Sentensi (i) ya Ks, inamaanisha kuwa kitendo cha kufundisha kilikuwa kikiendelea wakati uliopita, (ii) inaonyesha hali ya kuendelea kwa kitendo katika wakati ujao, (iii) kitendo kimekuwa kikitendeka tangu asubuhi ya siku hiyo na huenda kinaendelea au kimekoma. Kunao matumizi ya kiambishi {ki-} ambacho kinaonyesha hali ya kuendelea kwa kitendo katika wakati wowote ule. Matumizi mengine ya {ki-} ni yale ya kuonyesha dhamira tegemezi kwa kutoa masharti ya kitenzi¹.

Sentensi za Ek zinaonyesha hali ya kuendelea katika wakati uliopita na unaoendelea kama inavyodhihirika kwa toni ya juu () kwa wakati uliopita (arenge) na toni ya chini kwa ‘a-renge’ za sentensi Ek (i) na (ii) inaonyesha kuendelea kwa kitendo wakati ujao ambao huonyeshwa na Ts **a-raβe** (takuwa). Hali ya kuendelea ya wakati uliopita na uliopo katika Ek hutumia **-reng** (kuwa) na ujao hutumia Ts **-raβe** (kuwa) mbali na Ks ambayo hutumia ‘kuwa’ bila kubadili maumbo yake.

(iii) Hali ya mazoea

Hali hii huonyesha kutendeka kwa kitendo mara kwa mara kama desturi. Lugha ya Ks hutumia kiambishi {hu-} ambacho huchukua nafasi ya kwanza katika T. Wakati mwingine kiambishi {a-} hutumiwa kuonyesha hali hii katika Ks. Mifano

- 46(a) (i) Mtoto huyu hu-li-a sana
 (ii) Mtoto huyu a-li-a sana ;

Lugha ya Ek hutumia kiambishi {a-} ambacho huja mwanzoni mwa T baada ya kiambishi kiima. Kiambishi hiki kikitumika katika sentensi hufuatwa na leksika **βotambe** (kila mara) kufafanua hali ya mazoea

(b) (i) Omw-ana o-yo a-rer-a βotambe .

Mtoto kip. nafsi 3 - kionyeshi kip. nafsi 3 - hali – mzizi T lia – kiishio kila mara.

(Mtoto huyu hulika kila mara.)

(ii) N-to-βe to-ko-rem-a βotambe.

Kiy. –kip nafsi 1 wingi – Ts kuwa kip. nafsi 1 wingi – hali ya kuendelea – mzizi T lima. Kiishio kila mara.

(Tutakuwa tunalima kila mara.)

Kielezi ‘**βotambe**’ hutumika katika wakati wowote kuonyesha hali ya kurudiarudia kutendeka kwa kitendo.

Maelezo yanayohusu njeo na hali tuilizozitoa hapo juu, yanaweza kufupishwa hivi katika Jedwali 10.

NJEO	Viambishi vya njeo		Viambishi vya hali na visaidizi		
	KS	EK	HALI	KS	EK
Uliopo	a-/ -na-	-re / -e	Timilifu	-me-	-re-
Uliopita	-li/-ka-	-et-/ a/-ka-	Mazoea	-hu- /a-	a-/βotambe
Ujao	-ta-	-e	Kuendelea		
			Uliopo	'kuwa/na-	-re/βotambe
			Uliopita	-likuwa/-ki-	-renge/βotambe
			Ujao	-takuwa/-ki	-raβe / βotambe

Kulingana na maelezo haya, tunaweza kuona kuwa kuna tofauti kubwa kimuundo katika ya mofimu njeo na hali ya lugha ya Ks na Ek.

3.2.1.4 Viambishi jirejee vya Ks na Ek

Kiambishi cha kujirejelea ni kimojawapo ambacho pia hupatikana katika kitenzi. Mofimu hii huwa ni kisabiki² cha kiima. Mofimu jirejee kwa Ks ni {ji-} na Ek ni {-e} kwa mfano:

47) Ks. M-zee a-na-ji-pik-i-a chakula.

Ek. **Omo-gaka n-kw-e-ruger-a endagera.**

Mzee kiy- hali kuendelea – kb jirejee – mzizi T pika – kauli tendea – kiishio kb ngeli chakula.

(Mzee anajipikia chakula.)

Mofimu ya {ji} katika Ks, hurejelea 'mzee' ambayo ni nomino yenye uamilifu wa kiima katika sentensi na [-e} katika Ek hurejelea 'Omogaka'. Mofimu hizi hukubalia kitenzi kuchukua kivumishi –enyewe katika lugha hizi zote chenye uamilifu wa yambwa. Mfano.

48) Ks. (i) Mzee a-na-ji-pik-i-a mwenyewe.

Ek. (ii) **Omo-gaka a-kw-e-rug-er-a omonyene.**

Kb. ngeli 1 – mzee kip nafsi 3 umoja – hali kuendelea – kb jirejee- mzizi T pika- kauli kutendea – kiishio mwenyewe.

Ingawa mofimu jirejee zinarejelea kiima, uamilifu wao ni wa yambwa, katika lugha hizi.

3.2.1.5 Viambishi vya urejeshi katika Ks na Ek

Katika sura ya kwanza, tulitaja kuwa kuna urejeshi wa kutumia **amba-** na ule wa **o-rejeshi**. Urejeshi huu una uhusiano mkubwa, kwa sababu **O-rejeshi** hujitokeza kama kiambishi cha upatanishi cha nomino na kitenzi, pale ambapo kinajumuishwa pamoja na **amba** – kutoa urejeshi. **O-rejeshi** na **amba-** hutawaliwa na ngeli ya nomino husika. Katika Ks huwa kirejeshi -o- hutumika kama faridi ya urejeshi. Kwa lugha ya Ks, kirejeshi hiki huchukua nafasi ya tatu, na pengine huchukua nafasi ya mwisho. Kwa mfano.

- 49) (i) Kitabu ni-li-cho-ki-som-a ni chake.
Kitabu ni-ki-soma-cho ni chake.

Ingawa mofimu ya urejeshi {cho} inachukua nafasi tofauti tofauti, urejeshi wake ni kwa kiima tu (kitabu).

Lugha ya Ek, urejeshi wake hutumia aidha viwakilishi vionyeshi vya karibu au vya mbali, kulingana na ngeli ya nomino inayopatanishwa. Kwa mfano.

- 50) (i) **Omo-te o-yo-gwa noyoye**
kb. ngeli 3 – mti kip ngeli 3 – kirejeshi – mzizi T anguka ni wake.
(Mti ulioanguka ni wake).

- (ii) **Keria gia-sir-ete gia-tok-ir-e.**
Ambacho kip. ngeli 7 – mzizi T potea – wkt pita - kiishio kip ngeli 7 –
mzizi T pata – hali timilifu - kiishio
(Ambacho kilipotea kimepatikana.)

Vionyeshi vya karibu hutumika kama O-rejeshi ya Ks katika Ek kama (i) na vile vionyeshi vya mbali hutumika kama amba- ya Ks kama (ii).

3.2.1.6 Viambishi yambwa katika Ks na Ek

Yambwa ni leksika yenye uamilifu wa kisarufi katika mofosintakisia. Mofimu ya yambwa huwa na uhusiano mkubwa na hurejelea nomino tendwa au tendewa ambazo wakati mwingi hutangulia kitenzi katika lugha Ks na Ek. Nomino yambwa inaweza kuwepo au isiwepo, ikiwa mofimu yake imeambatishwa kwa kitenzi. Mofimu ya yambwa katika lugha hizi huchukua nafasi karibu na mzizi wa kitenzi, ukiifuatia. Mofimu yambwa huwa ni kiambishi kipatanishi cha nomino katika kitenzi, isipokuwa ngeli ya 1 ambayo mofimu yambwa inaweza kuwa kiwakilishi nafsi.

Mfano:

51) (i) Ks (i) A-li-ni-pig-a.

(ii) A-li-m-pig-a.

Ek (i) **A-ka-ng-it-a.**

Kip nafsi 3 umoja –wkt pita – kip yambwa nafsi 1 umoja – mzizi T piga – kiishio.

(ii) **A-ka-mo-it-a.**

Kip. nafsi 3 umoja – wkt pita – kip yambwa nafsi 3 umoja– mzizi T piga – kiishio.

(ii) Ks Nataka u-i-ni-som-e-e barua hiyo.

Ek **0-ye-ng'a-anor-er-e.**

Kip. nafsi 3 umoja – yambwa tendwa ngeli 9 – kb yambwa tendewa –mzizi T anua- hali - kiishio

(Uinianulie.)

Sentensi 51 (i) huonyesha vile ngeli ya 1 inaweza kuchukua mofimu yambwa mbalimbali. 51 (ii) zinaonyesha vile kitenzi kimoja kinaweza kuchukua yambwa mbili huku yambwa tendwa ikitangulia yambwa tendewa. Hali ya kuwa na yambwa mbili hutokea pale vitenzi vinaruhusu.

3.2.1.7 Viambishi vya vitenzi visoukomo

Lugha ya Ks mofimu ya kuonyesha kitenzi kisoukomo ni {ku-}, na Ek ni {ko-} ambayo ina alomofu {kw-}, {go-} na {gw-}, na zote hupachikwa mwanzoni mwa kitenzi (mzizi wa kitenzi). Kwa mfano

52)	Ks:	ku - imb-a	-	kuimba,
		ku - som-a	-	kusoma
		ku - end-a	-	kwenda
	Ek:	go-tera-a	-	gotera,
		go-som-a	-	gosoma,
		ko-gend-a	-	kogenda

Kisheria mifano ya lugha hizi inakuwa hivi;

Kb. kisoukomo + mzizi T + kiishio.

Katika kukanusha, Ks huongeza (-to-) kiambishi ambacho kinafuata kiambishi kisoukomo, na Ek hutumia {ti-} kwa kufuata kiambishi kisoukomo mfano.

53) (i) Ku-fik-a kwake mapema.

Ku-to-fik-a mapema.

(i) **O-ko-rema kwaye.**

Kb. kiso-mzizi T. lima kwake.

(Kulima kwake.)

O-go-ta-rem-a kwaye.

Kb.kiso – kb kukana – mzizi T lima kwake.

(Kutolima kwake.)

3.2.1.8 Viambishi vya Mwisho

Mofimu za mwisho katika lugha za kibantu huwa ni irabu /a/ na /e/. Mofimu hizi zina majukumu ya kuonyesha dhamira mbalimbali zinazobebwa na kitenzi. Lugha ya Ks na ya Ek, zina viishio vya irabu hizi ambazo kwa jumla husimamia dhamira ya mzungumzaji ya kueleza hisia za mzungumzaji kuhusu yale anayoyasema. Kuna dhamira mbalimbali.

(i) Dhamira arifu.

Dhamira arifu huwa na sifa za kusudia kueleza juu ya jambo fulani au kujulisha zaidi kuhusu jambo hilo. Hutumiwa kueleza ukweli wa mambo unavyodhihirika. Inaweza kuwa kwa njia ya maelezo tu au kwa kuuliza. Dhamira hii wanasarufi wengine huita dhamira elezi. Kitenzi cha kuonyesha dhamira hii katika sentensi huwa kinaishia mofimu {a} kwa Ks. Mifano ya Ks.

- 54) (i) Sisi tu-na-imb-a sasa.
(ii) Utafikaje kwake Yusuf?

Lugha ya Ek, hutumia mofimu {a} na zile za wakati na hali ambazo huchukua nafasi ya mwisho katika kitenzi kutoa dhamira arifu kama {e}. Rejelea sura hii sehemu ya 3.2.1.3. Mifano.

55) (i) **Moraa o-chi-ir-e e-chiiro**

kip. nafsi 3 umoja – mzizi T enda – hali timilifu – dhamira sokoni.
(Moraa ameenda sokoni)

(ii) **Iter-a amache ayio.**

Mzizi T mwaga – kiishio / dhamira maji kip. 6 - kionyeshi
(Mwaga maji hayo)

(ii) Dhamira agizi.

Aina hii ya dhamira pia huitwa dhamira amrishi. Hutoa maana ya amri, ombi, pendekezo au taradha. Dhamira hii huelekezwa na mtu / watu katika nafsi ya pili, ingawa anayegizwa mara nyingi hatajwi. Mofimu {a}, {c} na {-eni} hutumiwa kuonyesha dhamira hii katika lugha ya Ks; Mfano.

- 56) (i) Imb-a
 (ii) Nisaidie maji ya kunywa.
 (ii) Tok-eni hapa nyote.

Sentensi hizi zinaonyesha dhamira agizi kwa kuamrisha {a} (i), kuomba (ii) mofimu {e}, na (iii) mofimu ni {eni}. Tunadokeza hapa kuwa, mofimu {a} hutumiwa kuamru mhusika mmoja na {eni} wahusika wengi na mofimu {e} hudhamiria kuagiza na kupendekeza kwa njia ya kuomba.

Lugha ya Ek, hutumia mofimu {a} kwa kuamrisha na {e} kuagiza na kuomba au kupendekeza. Kwa mfano.

- 57) (i) **Kir-a** (nyamaza)
Rug-a (pik-a)
 (ii) **N-kony-e amache yokonywa.**
 (Nisaidie maji ya kunywa)
 (iii) **Ndetere ekaramu**
 (Nilettee kalamu)

57) (i) Kitenzi kinaishia {a} ambayo huonyesha dhamira ya kuamru, (ii) mofimu {e} dhamira ya kuomba na {ii} ni kuagiza lakini mofimu zinaweza kuwa na uamilifu zaidi. Dhamira agizi katika lugha ya Ks na Ek hujitokeza katika {a} na {e}, lakini tofauti ni ile ya kiambishi {-eni} ambacho kinatumika kwa lugha ya Ks tu, wala hakipatikani kwa Ek. Mofimu {a} kwa jumla ikitumiwa kuagiza, kitenzi kinatumika katika umbo lake la msingi.

(iii) Dhamira tegemezi

Dhamira tegemezi hutumika zaidi kuonyesha uwezekano wa kutendeka kwa jambo. Dhamira hii hutazamiwa na hutoa matumaini ambayo kwa kawaida huenda hayapatikani.

Dhamira tegemezi katika Ks huonyeshwa kwa mofimu {e} mwishoni mwa kitenzi {-ngo-} na {-ngali-} ambazo huchukua nafasi kabla ya mzizi wa kitenzi.

Tazama mfano:

- 58) Ks (i) Ungalimpata ungalifurahi.
 (ii) Ningemtahadharisha ningemjua.

- (iii) Mpatie mtoto chakula.
- (iv) Mungu amsaidie apone.

Sentensi (i) na (ii) zinatoa maana ya kutumainia. Kiambishi [ngali] huonyesha zaidi kutowezekana kuliko {nge} ambayo hutoa matumaini na uwezekano.

Mofimu {e} katika (iii) na (iv) huonyesha hali ya kutegemea. Dhamira tegemezi hutumika sana kumwomba Mungu kwa matumaini. Lugha ya Ek dhamira hii huonyeshwa kwa mofimu {e}, na vielezi vingine. Mfano

59) **Ba-tebi-e ba-gend-e.**

kip nafsi 3 wingi – mzizi T ambia – kiishio kip nafsi 3 wingi – mzizi T
enda

(Wambie waende.)

O-rar-e

Kip nafsi 3 umoja – mzizi T lala – kiishio.

(Ulale.)

Dhamira tegemezi ina maana nyingine kimatilaba ambazo hujumuisha nia, kuagiza kwa upole na dhamira ulizi ya kuruhusu³. Mfano.

60) (i) **Gend-a mo-risi-e chiombe.**

enda kip – nafsi 2 wingi – mzizi T lisha- kauli ish-kiishio kb ngeli 10
ng'ombe.

(Enda mlishe ngombe.)

(ii) **Ng-i-mokie.**

Kip nafsi 1 umoja – mzizi T beba.

(Nibebe).

(iv) **Dhamira masharti.**

Dhamira hii hutumika kuelezea uwezekano wa kitenzi kutekelezwa baada ya masharti yaliyo katika mzizi wa kitenzi chenye mofimu ya kuonyesha masharti. Mofimu za masharti ni {ki-}, {ngali-}, {nge}, {japo} katika Ks. Vitambulishi {nge} na {ngali} huwa na uamilifu kuwili, hutumika kwa dhamira tegemezi na dhamira masharti. Anavyoeleza Mychina (1981:53), {ki} hutoa masharti ya

kutendeka kwa kitendo kutegemea kitendo kingine. Masharti humaanisha kuwa masharti fulani sharti yatekelezwe kabla ya kitendo kufanyika. Tazama mifano hii ya Ks.

- 61) (i) Kama angeenda mapema, angempata.
 (ii) Ujapomwita, haitiki.
 (iii) Angalipata angalinunua.
 (ii) Ukimpiga nitakupiga.

Vitendo vya pili hutegemea vitendo vya kwanza katika sentensi. Kama (i) angempata tu angeenda mapema; (ii) kuitika kunategemea kuitwa, sentensi hii ina matilaba zaidi ya ukubaliano, (iii) na (iv) huonyesha masharti ya utekelezaji.

Dhamira masharti katika Ek huwakilishwa na {-ko-} (ki) ambayo hufanya kazi kama {-ki-} ya Ks. Tazama mifano:

- 62) EK (i) **Ko-go-et-a a-ma-temwa n-in-ko-gor-er-e ekeegwa**
 kip nafsi 2 umoja – kb masharti mzizi T pita kiishio kb ngeli
 7 mtihani kiy –kip nafsi 1 umoja – hali - mzizi T nunua –
 kauli tendea – kiishio.
 (Ukipita mtihani nitakununulia zawadi.)
- (i) **Go-ko-gend-a, o-nda-nger-i-e.**
 Kip nafsi 2 umoja – masharti – mzizi T – kiishio kip nafsi 2 –
 kb yambwa – mzizi T ita – kiishio.
 (Ukienda uniite)

Kimantiki, dhamira za Ks na Ek zinafanana kwa sababu matumizi yao ni sawa, mofimu nyingi zinafanana ingawa baadhi tu zinatofautiana. Tazama ufupisho wao.

Dhamira	Mofimu za Ks	Mofim za Ek.
Arifu	a	a, / re
Agizi	a / e	a / e
Tegemezi	e / nge / ngali	e
Masharti	Ki / nge / ngali	Ko / go

Mofimu katika jedwali hii hazimaanishi kuwa zinasimamia dhamira zilizoonyeshwa pkee bali zinaweza kuwa na matumizi mengine zaidi ya kisarufi.

3.2.1.9 Uamilifu Wa Toni katika Ek

Toni ni kiwango cha kidatu pamoja na mabadiliko yake ambayo hutokea wakati mtu anapotamka silabi au maneno. (Mgullu 1999:37). Toni katika Ek ina uamilifu wa kisemantiki na ule wa kisintaksia. Kisemantiki, toni hutumiwa kutofautisha maneno kimaana (Osinde 1988) kwa mfano ri:ka (andika) rika (kwama). Hatuelezi zaidi jinsi toni inavyotumika kisemantiki kwani ni suala lililo nje ya mpaka wetu.

Kisintaksia, toni katika Ek, hutumiwa kutofautisha njeo na hali mbalimbali. Ikiwa toni inapanda, huwakilisha wakati tofauti kwa mofimu ileile, ikishuka huwakilisha wakati mwingine tofauti. Toni hutofautisha njeo za wakati uliopita katika Ek.

Tulitaja awali kuwa lugha ya Ek ina njeo za wakati uliopita mbalimbali. Mofimu {et-} huwakilisha njeo iliyopita mara mbili. Kwanza, ikiwa mofimu {ete} ina toni ya kupanda {↗} humaanisha ni wakati uliopita mrefu unaodhihirika kuwa mwaka au miaka iliyopita. Ikiwa inashuka (↘) njeo hiyo huwa ni ya wakati uliopita karibuni, si mbali sana. Tazama sentensi hizi;

(i) **Ányoreté aria.** (Alipata pale.)

(ii) **Ányoreté aria.** (Alipata pale.)

Sentensi ya (i), inaonyesha alipata muda uliopita hivi karibuni. Ilhali ya (ii), inaonyesha muda mrefu uliopita. Mara nyingine, mofimu hizi hutumiwa pamoja na vielezi vya wakati kutofautisha wakati.

Ányoreté aria igoro. (Alipata pale jana).

Ányoreté aria omwaka oria. (Alipata pale mwaka uliopita)

Pia, toni hutumiwa kutofautisha hali timilifu na wakati uliopita kwa mofimu {a}. Toni ikipanda, huonyesha wakati uliopita si mbali, kuonyesha juzi, ikishuka, huonyesha muda mfupi uliopita katika wakati wa kuzungumza, hurejelea tukio la siku hiyo lakini muda mfupi sana umepita.

(i) **Ekaramu anyora.** (Amepata kalamu)

(iii) **Ekaramu anyora.** (Alipata kalamu)

Sentensi ya (i) inaonyesha muda mfupi uliopita ndipo alipata kalamu, (ii) inaonyesha muda mrefu uliopita na si siku hiyo ya kuzungumza bali siku zimepita zaidi ya moja. Mofimu {a} ya wakati uliopita mfupi si sawa na ile ya hali timilifu ya {re} ambayo tulieleza awali. Uamilifu wa {a} ni tofauti kiwakati na ule wa {-re}. {re} huonyesha hali timilifu.

3.2.2.0 Unyambuaaji Wa Vitenzi Vya Ks Na Ek

Wataalamu mbalimbali wametoa maoni mbalimbali kuhusu unyambuaaji wa vitenzi vya lugha za Kibantu. Ashton (1947) alidokeza unyambuaaji wa vitenzi vya Kiswahili sanifu kuwa kuongezea vitenzi maumbo ya kifonetiki ambayo ni viambishi tamati kwa mzizi wa kitenzi. Viambishi tamati hivi hukipatia kitenzi maana tofauti na hivyo kukinyambua.

Habwe na Karanja (2004) wanasisitiza kuwa kuongezea vitenzi vya lugha za Kibantu viambishi tamati si unyambuzi bali uambishaji kwani kitenzi hakibadili kategoria yake.

Nasi tungependa kusema kuwa, maoni haya yanapotosha kwani, kitenzi kinapoongezewa viambishi tamati huwa maana ya kitenzi hubadilika na hivyo kupiga hatua kwa kupitia mnyambuliko. Ni sawa na vile nomino inaweza kupitia unyambuaaji na kuzaa nomino nyingine. Kwa mfano katika Ks, kutokana na nomino 'mvulana' tunaweza kuunda nomino 'uvulana' kwa kuongeza kiambishi awali {u} badala ya {m}.

Polome (1967:82) anasema kuwa, unyambuaaji katika vitenzi vya lugha za Kibantu ni changamano kwa kuwa mzizi wa kitenzi hupanuliwa kwa kuongezewa kiambishi kimoja au zaidi kwa njia maalum, kwa minajili ya kufanya kazi kama kinyambuo.

Upanuzi wa vitenzi katika lugha hizi huwa na uamilifu wa kisemantiki wa kuongeza au kupanua au kueleza zaidi maana ya kitenzi msingi⁴. Upanuzi wa vitenzi ni muundo wa kimofolojia wa neno ambao una mahusiano muhimu ya kisarufi kwa kuzalisha maana zaidi kisemantiki.

Vitenzi vikuu vya uelekezi na visivyoelekezi ndivyo huongezewa viambishi tamati katika hali ya kuvinyambua. Vitenzi vishirikishi na vile visaidizi havina uwezo wa kujiongezea viambishi tamati. Kimofolojia, vitenzi visoelekezi vikipitia mnyambuliko aghalabu hupoteza hali yao ya usoelekezi na kuwa vielekezi. Kwa mfano.

- 63) Ks (i) Mtoto a-me-lal-a.
(ii) Mama a-me-m-lal-ish-a mtoto.,
Ek (iii) βαβα o-mo-rar-ir-i-e omwana.
Mama kip nafsi 3 umoja – kip yambwa – mzizi T lala – hali –
kauli ish – kiishio mtoto.

Sentensi 62 (ii) na (iii) zimeandikwa katika hali ya kutendesha, ambapo katika (i) ni sentensi isoelekezi. Kitenzi 'lala' kisichoelekezi kimeongezewa viambishi tamati {ish-} katika Ks, na Ek kitenzi 'rara' kimeongezewa {-ir}, ambavyo ni viambishi tamati vinavyoongeza maana ya kumfanya mtoto alale badala ya kulala pekee yake kama (i)

Unyambuzi wa vitenzi huchukua kauli mbalimbali katika lugha hizi. Hata hivyo tutashughulikia kauli zifuatazo na viambishi vyao vya unyambuzi katika lugha ya Ks na Ek kiulinganishi.

1. Kauli ya kutendea.
2. Kauli ya kutendwa.
3. Kauli ya kutendesha
4. Kauli ya kutendana
5. Kauli ya kutendua.
6. Kauli ya kutendeka.
7. Kauli ya kutendatenda.

3.2.2.1 Kauli ya kutendea

Vitenzi katika kauli ya kutenda vinapogeuzwa kwa kauli ya kutendea viambishi ambavyo huongezwa kwa T huwa ni irabu ya mbele ambayo huwa aidha {e} au {i}. Irabu hizi zina alomofu [li], [le]. Viambishi hivi vyote katika Ks hutokea kutegemea muktadha wa neno. Ikiwa mzizi wa kitenzi una irabu /a/, /i/ au /u/ kiambishi {i} huongezwa kwa kitenzi hicho. Kiambishi {-e} huongezwa pale ambapo mzizi wa kitenzi una irabu /o/ au /e/ kama katika mifano hii.

<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli ya Kutendea</u>
imb-a	imb-i-a
pit-a	pit-i-a
vunj-a	vunj-i-a
som-a	som-e-a
chot-a	chot-e-a
tend-a	tend-e-a.

Alomofu {-li} na {le} huongezwa kwa vitenzi vyenye mzizi inayoishia irabu. Ikiwa mzizi wa kitenzi unaishia vokali /a/, /i/ au /u/ huongezewa alomofu {li}, na alomofu {-le-} huongezewa vitenzi vyenye mizizi yenye irabu /e/ au /o/ katika Ks. Tazama mfano.

<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli ya kutendea</u>
Twa-a	twa-li-a
Ng'o-a	ng'o-le-a
Le-a	le-le-a
Vu-a	vu-li-a.

Lugha ya Ek, mofimu {-er} huongezewa vitenzi vilivyo katika kauli ya kutenda. Mofimu hii ya {-er} ina alomofu kama Ks, ambazo huletwa na ukubaliano wa vokali katika mizizi ya vitenzi ambayo ni {-eri-} tazama mifano ifuatayo.

<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli ya kutendea.</u>	<u>Tafsiri</u>
it-a	it-er-a	piga - pigia
ier-a	rer-er-a	lia - lilia
tir-a	tir-er-a	panda - pandia
som-a	som-er-a	soma - somea
ror-a	ror-er-a	ona - onea
o-ni-a	on-eri-a	uza - uzia
ombi-a	omb-eri-a	vaa miwani - valia miwani
siβi-a	Siβ-eri-a	fua - fulia

Mifano mitatu ya mwisho mizizi inaishia kwa irabu /i/ ambayo inadondoshwa katika kauli ya kutenda na hukifanya kitenzi kuwa kama katika kauli ya kutendesha. Ndio sababu mofimu {-er-} imeongezea irabu /i/.

Vitenzi katika kauli ya kutenda hutoa maana ya kitendo kutendwa kwa faida au hasara ya mtendewa au yambwa. Zaidi, vitenzi vingine vinaweza kutoa maana ya kuelekea mahali fulani, na vingine huonyesha hali ya kuisitiza kutendeka kwa kitendo. Kwa mfano.

Kiswahili Sanifu

Ekegusii

<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli ya kutendea</u>	<u>Kitenzi</u>	<u>Kutendea.</u>
kimbi-a	kimbi-li-a	et-a	et-er-a
tembe-a	tembe-le-a	gor-a	gor-er-a
pit-a	pit-i-a	tar-a	tar-cr-a.

Vitenzi vingine katika lugha ya Ks na Ek vikiwa katika kauli ya kutendea hutoa maana iliyo kinyume kimaana na kitenzi katika kauli ya kutenda.

Mfano:

64) Ks: nuk-a - nuk-i-a, Ek: ror-a - ror-er-a. (ona – onea)

Tofauti na Ek, Ks ina vitenzi vingine vinavyoweza kunyambuliwa zaidi baada ya kauli ya kutendea na kutoa maana ya kuisitiza vikiwa katika kauli ya kutendea.

Kwa mfano:

<u>Kitenzi</u>	<u>Kutendea</u>	<u>Kutendea.</u>
ach-a	ach-i-a	ach-i-li-a
shinda	shind-i-a	shind-i-li-a
kat-a	kat-i-a	kati-li-a.

3.2.2.2 Kauli ya Kutendwa

Kauli hii hutambulika kwa njia mbili katika Ks na Ek. Kwanza, pale ambapo yambwa ya sentensi katika kauli ya kutenda, hugeuka na kuwa kiima cha sentensi tendwa.

Pili, huwa kuna matumizi ya kihusishi 'na' kinachohusisha kiima na yambwa kupitia kwa kitenzi tendwa. Tazama mifano ya sentensi

65) Ks. (i) Juma a-me-m-pig-a maria.

(ii) Maria a-me-pig-w-a na Juma.

Ek. (i) **Makori o-som-ir-e ege-taβu.**

Kip nafsi 3 umoja – mzizi T – hali kb ngeli 7 kitabu.

(Makori amesoma kitabu)

(ii) **Ege-taβu gi-a-som-ir-w-e na Makori.**

Kb ngeli 7 kitabu kip – mzizi T – hali timilifu – kauli tendwa

– kiishio makori.

Kitabu kimesomwa na Makori.

Mofimu {-w-} huongezwa kwa mizizi ya vitenzi katika lugha hizi mbili ili

kukifanya kitenzi katika kauli tenda kuwa katika kauli tendwa. Kwa mfano.

Kiswahili sanifu

Ekegusii.

<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli ya kutendwa</u>	<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli ya kutendwa.</u>
pig-a	pig-w-a	rem-a	rem-w-a (lima)
som a	som w-a	ter-a	tar-w-a (imba)
chom-a	chom-w-a	siβ-a	siβ-w-a (funga)
lim-a	lim-w-a	ror-a	ror-w-a (ona)

Tungependa kuongeza kwamba, kauli ya kutendwa ina kauli mwenza inayokaribiana nayo ambayo ni kauli tendewa. Kauli tendewa ni tofauti na kauli tendwa kwa sababu kauli tendewa hufanyiwa vitenzi ambavyo tayari vimepitia mnyambuliko. Kwa mfano vitendo vilivyopitia mnyambuliko wa kutendea, kutendesha, n.k. huweza vilevile kunyambuliwa kutumia kauli tendewa. Kwa mfano.

1. **Kiswahili sanifu.**

<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli ya kutendea</u>	<u>Kauli ya kutendewa</u>
pig-a	pig-i-a	pig-i-w-a
za-a	za-li-a	za-li-w-a
twa-a	twa-li-a	twa-li-w-a
imb-a	imb-i-a	imb-i-w-a.

<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli ya kutendesha</u>	<u>Kauli ya kutendewa.</u>
som-a	som-esh-a	som-esh-w-a
lim-a	lim-ish-a	lim-ish-w-a
imb-a	imb-ish-a	imb-ish-w-a.

Ekegusii

<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli ya kutendea</u>	<u>Kauli ya kutendewa.</u>
rem-a	rem-er-a	rem-er-w-a
ter-a	ter-er-a	ter-er-w-a
som-a	som-er-a	som-er-w-a
rug-a	rug-er-a	rug-er-w-a

Kutokana na mifano hii, tunaweza kuona kuwa katika kauli ya kutendewa, vitenzi au mizizi ya vitenzi huongezwa mofimu {-w-} baada ya viambishi tamati vingine ambavyo hufuata mzizi wa kitenzi, kisha mofimu {-w-} ya kutendewa hupachikwa, ilhali kauli ya kutendwa, mofimu {-w-} huongezwa kwa mzizi wa kitenzi punde tu baada ya mzizi na wala hakifuati viambishi vingine tamati. Tunadhani, data hii

itamsaidia Omusula (1998:24) ambaye amemtia Maringah (1987:108) lawamani kwa kutoa kauli kama hii.

3.2.2.3. Kauli ya kutendesha

Kauli hii hutoa dhana ya kiima kusababisha yambwa kutenda tendo. Yaani, hali ya kitendo fulani husababishwa kufanyika na mtu au kitu fulani. Hali hii si lazima iwe ya kulazimisha tu bali ya hiari pia kwa mfano.

66) Ks Mwalimu a-na-fund-ish-a watoto.

Ek **Omw-arimu n-ko-som-i-a-re aβana.** (Tafsiri ya Ks)

Kb.ngeli 1 mwalimu kiy – hali – mzizi T soma – kauli ish – kiishio – kip nafsi 3 umoja – hali.watoto.

Hali ya mwalimu kufundisha haimaanishi kuwa amelazimika kufanya hivyo, bali ni wajibu wake. Kwa mantiki hii, aghalabu kauli hii hutoa maana ya kulazimishwa.

Mofimu ya kutendesha kwa Ks ni {-iʃ-} ambayo ina alomofu {-eʃ-}, {eʃ}, {z}, {iz-}, {ez}, {s} {-fj-} na {-vj}. Kwa lugha ya Ks, hii ndio kauli yenye alomofu nyingi zaidi ya kauli zote. Mnyambuliko huu pia huchukua ile sheria ya ukubaliano wa irabu. Kwa mfano, katika Ks, ikiwa mzizi wa kitenzi una irabu /a/ /i/ au /u/ vitenzi hivyo vitachukua kiambishi {iz} au {iʃ}. Kwa mfano.

<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli ya kutendesha</u>
uz-a	uz-ish-a
fung-a	fung-ish-a
ig-a	ig-iz-a
fany-a	fany-iz-a

Vilevile, mofimu {ez} {eʃ} huongezwa kwa mizizi ya kitenzi yenye irabu /e/, /o/ au /ɔ/ mfano.

<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli ya kutendesha</u>
chez-a	chez-esh-a
mez-a	mez-esh-a
pend-a	pend-ez-a
end-a	end-esh-a
tok-a	tok-ez-a.

Kiambishi [z-] huambatishwa pale ambapo vitenzi vina mizizi inayoishia vokali.

Mifano.

<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli ya kutendesha</u>
ja-a	ja-z-a
pa-a	pa-z-a.
li-a	li-z-a.

Baadhi ya vitenzi vinavyoishia /t/ katika mzizi wa kitenzi, huchukua mofimu {s} ambayo hutokea kwa sababu ya athari ya kiyeyushi /j/ kilichotumika sana katika lugha za Mamebantu katika kauli ya kutendesha⁵. Kwa mfano takata –takasa.

Kiyeyushi hiki /j/ pia kinapoongezewa kwenye vitenzi vinavyoishia konsonanti /p/ au nusu irabu /w/, matokeo yake huwa ni /fj/ na /vj/ mtawalia. Tazama mifano.

<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli ya kutendesha</u>
ogop-a	ogofya
ongop-a	ongofya
pap-a	pafya
lew-a	levya
low-a	lovyo.

Ks ikiwa inapitia mabadiliko mbalimbali kwa kuzingatia ukubaliano wa irabu, Ek huwa ni tofauti. Mofimu ya Ek ya kutendesha ni moja tu nayo ni {i} ambayo huongezwa kwa mzizi wa kitenzi. Mifano ni kama;

<u>Kitenzi</u>	Tafsiri	<u>Kauli ya kutendesha.</u>	
siek-a	(funga)	siek-i-a	(fungisha)
ter-a	(imba)	ter-i-a	(Imbisha)
eβ-a	(sahau)	eβ-i-a	(sahaulisha)

rug-a (pika) rug-i-a (pikisha)

tig-a (acha) tig-i-a (achisha)

Kutokana na utafiti wetu, tuligundua ya kwamba, mofimu {lish}, {lesh} {liz} za Ks ambazo wanasarufi wengi huzitaja kuwa ni za kutendesha huwa si moja kwa moja hivyo. Tungependa kusema kwamba, hizi mofimu hutokea baada ya mzizi wa kitenzi kupitia mnyambuliko wa kwanza hasa ule wa hali ya kutendea.

Tazama mifano hii.

<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli ya kutendea</u>	<u>Kauli ya kutendesha</u>
za-a	za-li-a	za-li-ish-a
zo-a	zo-le-a	zo-le-esh-a
va-a	va-li-a	va-li-ish-a
to-a	to-le-a	to-l-ez-a
tu-a	tu-li-a	tu-l-iz-a
li-a	li-li-a	li-l-iz-a ⁱ

Kutokana na mifano hii, irabu za kauli ya kutendea, zikiwa katika kauli ya kutendesha huwa zinadondoshwa kisheria kwa sababu ya kufuatana.

/Za + li + ish + a/ → [zalisha] i + i = i

3.2.2.4 Kauli Ya Kutendana

Kauli ya kutendana hutoa maana kimatilaba, kwamba mhusika wa kwanza hutenda jambo na tendo lilo hilo hufanyiwa yeye na yule wa pili. Kauli hii huhusishwa wahusika wawili au zaidi, ambao pia wakati mwingine wanaweza kuwa wanatenda kitendo hicho kwa mwingine wakati mmoja bila kungoja mwingine amalize. Kwa mfano.

67) Ks. Watoto wa-na-pig-an-a

Ek. $\alpha\beta$ ana n-ko-it-an-a β a-re.

Watoto kiy. – hali kuendelea – mzizi T piga – kauli an – kiishio kip nafsi 3 wingi – hali.

Sentensi hizi zimetoa maana kuwa, watoto wanafanya kitendo kwa wakati mmoja, kwa mwingine. Mofimu ya kutendana ni {-an-} katika lugha ya Ks na Ek, na hii huonyesha kuwa zote ni lugha za Mame Bantu. Mofimu hii haina alomofu.

Tazama mifano.

Kiswahili Sanifu

<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli va kutendana</u>
ju-a	ju-an-a
pig-a	pig-an-a
pend-a	pend-an-a
som-a	som-an-a

Ekegusii

<u>Kitenzi</u>	<u>Tafsiri</u>	<u>Kauli ya kutendana</u>	<u>Tafsiri</u>
tar-a	(tembea)	tar-an-a	(tembeleana)
anch-a	(penda)	anch-an-a	(pendana)
ror-a	(ona)	ror-an-a	(onana)
a-k-a	(piga)	a-k-an-a	(pigana)

Minyambuliko mingine katika lugha hizi, inaweza pia kunyambuliwa zaidi katika kauli ya kutendana, kwa mfano, kauli ya kutendwa inaweza kuwa kauli ya kutendana.

Katika lugha ya Ks na Ek. Tazama mifano.

Kiswahili

<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli ya kutendea</u>	<u>Kauli ya kutendana</u>
pik-a	pik-i-a	pik-i-an-a
fung-a	fung-i-a	fung-i-an-a
tembe-a	tembe-le-a	tembe-le-an-a
ondo-a	ondo-le-a	ondo-le-an-a

Ekegusii

it-a	it-cr-a	it-cr-an-a	(pigiana)
tar-a	tar-er-a	tar-er-an-a	(tembeleana)
rug-a	rug-er-a	rug-er-an-a	(pikiana)
rem-a	rem-er-a	rem-er-an-a.	(limiana)

3.2.2.5 Kauli ya Kutendua

Vitenzi katika kauli hii, hutoa maana yaliyo kinyume cha mzizi wa kitenzi katika kauli ya kutenda. Lugha ya Ks, mofimu za kutendua ni {o} na {u}. Kiambishi {o} hupachikwa kwenye mzizi wa kitenzi wenye irabu / o / au / ɔ / na kiambishi {u} huongezwa kwa mzizi wenye irabu /a/, /e/, /i/ au/u/.

Kwa mfano

Kitenzi Kauli ya kutendua

teg-a	teg-u-a
zib-a	zib-u-a.
fumb-a	fumb-u-a
chom-a	chom-o-a
shon-a	shon-o-a.

Kiambishi cha kutendua kwa Ek ni kimoja tu nacho ni {or-}. Mifano ni kama.

Kitenzi Kauli ya kutendua

ring-a	ring-or-a	(kunjua)
siβ-a	siβ-or-a	(fungua)
om-a	om-or-a	(bomoa)
teg-a	teg-or-a	(tegua)

Mbali na Ks, Ek huwa na vinyume vingine ambavyo vinapingana kimaana moja kwa moja na mizizi ya vitenzi haifanani, ingawaje mofimu {or} inatumika. Kwa mfano.

<u>Kitendo</u>	<u>Kutendua.</u>	
kunek-a	kun-or-a	(funika- funua)
siek-a	ig-or-a	(funga –fungua)
aneke-a	an-or-a.	(anika – anua)

Ni muhimu kugundua pia kuwa, vitenzi katika kauli ya kutendua, vinaweza kunyambuliwa zaidi kwa kauli zingine katika lugha hizi. Kwa mfano, vinaweza kunyambuliwa kwa kauli ya kutendea, kutendesha au kutendeka. Kwa mfano, Ks; Teg-u-a –teg-u-li-a, teg-u-li-k-a n.k.

Ek; Anora - an -or-er-a, an-or-ek-a, an-or-er-an-a (anu-a - anulia -anulika – anuliana).

3.2.2.6 Kauli ya kutendeka

Mofimu za kauli hii katika Ks ni {ik-} na {ek}, na Ek ni {-ek-}. Mychina (1981:48) anaeleza kauli hii kuwa na maana mbili. Moja ni kuwa, vitendo katika kauli hii hutendeka bila kuonyesha mtendaji au aliyesababisha kitendo kutendeka. Kwa mfano.

68) Ks. Bilauri i-me-vunj-ik-a.

Ek. **Ege-kombe gia-tek-ir-e.**

Kb. ngeli 7 kikombe kip ngeli 7 – mzizi T vunja -hali timilifu – kiishio.

(Kikombe kimevunjika.)

Kitendo cha kuvunjika kwa bilauri na kikombe, hakionyeshwi kuwa ni nani aliyevunja. Pili, huonyesha kuwa kitendo kina uwezo wa kufanyika au kufanywa.

Kwa mfano.

69) Ks. Chakula hiki ki-na-l-ik-a.

Ek **Omo-gondo o-yo o-ko-rem-ek-a.**

Kb. ngeli 3 shamba kip. ngeli 3 – kionyeshi kip ngeli 3 umoja – hali
– mzizi T lima – kauli tendeka – kiishio.

(Shamba hili linalimika.)

Hebu tazama mifano ya vitenzi hivi sasa:

Kiswahili sanifu

<u>Kitenzi</u>	<u>Kauli ya kutendeka</u>
l-a	I-ik-a
nyw-a	nyw-ek-a
lim-a	lim-ik-a
fung-a	fung-ik-a

Ekegusii

<u>Kitenzi</u>		<u>Kauli ya kutendeka</u>	
ter-a	(imba)	ter-ek-a	(imbika)
rem-a	(lima)	rem-ek-a	(limika)
rug-a	(pika)	rug-ek-a	(pikika)
at-a	(vunja)	at-ek-a	(vunjika).

Vitenzi vilivyonyambuliwa kwa kauli zingine vinaweza kunyambuliwa zaidi kwa kauli ya kutendeka. Kwa mfano:

Ks. End-a -end-esh-a –end-esh-e-a –end-esh-e-k-a.

Ek **teg-a teg-or-a teg-or-ek-a.**
(tega tegua tegulika)

3.2.2.7 Kauli ya kutendatenda

Kauli hiji katika lugha ya Ks na Ek, hutoa maana ya kutendeka kwa kitendo kwa muda au hali ya kusisitiza uzito wa tendo hilo. Aghalabu, mzizi au konsonanti za mwanzo au mwisho hurudiwarudiwa. Tazama mfano.

- 70) Ks. Gogota, pepeta, ombaomba, imbaimba n.k.
 Ek. Sunasuna, mogamogia, kenakena, sisikia n.k
 (Kuchunachuna, pepesa macho, kutotulia, kusukua).

3.2.2.8. Kauli ya kudumisha

Kauli hii haipo katika lugha ya Ek lakini hupatikana katika Ks. Kauli hii humaanisha kuwa kitendo hudumishwa katika hali fulani bila kubadilika. Kwa mfano: Kwa- kwama, ganda -gand-am-a, n.k. Wanasurufi wengi, kama Polome (1967) husema mofimu ya kudumisha ni {am}.

Viambishi vya unyambuzi katika lugha ya Ks na Ek. vinaweza kuungana kupitia kwa uambishaji kuongezea maana zaidi kimatilaba kwa mzizi wa kitenzi.

Kuungana huku tumekushughulikia kwa kila lugha. Tumeonyesha jinsi ambavyo mnyambambuliko mmoja unaweza kufungua njia kwa minyambuliko mingine. Kwa mfano.

71)	Ks.	Kutenda	kauli ya kutendea + kutendean
		Ona	on-e-a on-e-an-a
	Ek	Tera	Ter-er-a ter-er-an-a
			(imba + imb-ia + imb-i-an-a)

Kwa jumla tumeangalia katika sura hii, muundo wa kitenzi cha lugha ya Ks na Ek. Muundo huu tumetazama kwa kuzingatia viambishi vya kimofolojia kupitia uambishaji na unyambuaji. Jedwali ifuatayo inatoa ufupisho wa viambishi vya unyambuaji.

Viambishi Vya Kauli

Mnyambuliko	Kiswahili sanifu	Ekegusii
Kutendea	e, e, -li, le-	-er-, eri-
Kutendwa	-w-	-w-
Kutendesha	i, e, ez, iz, z, s, vj, fj,	-i-
Kutendeana	-an-	-an-
Kutendua	u, o,	-or-
Kutendeka	-ik-, -ek-,	-ek-
Kudumisha	-am,	-

3.2.3.0 Kitenzi Na Uminimalisti


Kama tumeona, kitenzi katika lugha hizi kina mofimu nyingi ambazo zinaweza kuwakilishwa kwa vifundo mbalimbali katika kanuni ya kujenga miundo kwa kutumia uminimalisti. Hali ya kunyambua na kuambisha vitenzi katika lugha hizi ni hatua ambayo inakifanya kitenzi kuwa kikamilifu chenye maana sanifu. Kitenzi kilichoambishwa kwa hiyo ni sentensi sahili katika lugha ya Ks na Ek. Kwa mfano;

Ks Tu-li-ki-nunu-a

Ek To-ga-ke-gor-a

Kip nafsi 1 wingi -- kb wkt pita – kip. yambwa ngeli 7 mzizi T nunua – kiishio.

Kutokana na kitenzi hiki, ambacho unakiona kuwa KT, tunaweza kukagua sifa zake za upatanishi na kiima, yambwa na sifa ya njeo kwa sababu zinawakilishwa kimofolojia. Mfano katika kielelezo matawi.



Kitenzi hiki kinasogezwa kutoka kwa T hadi kwa UPy na kwa NJ na mwisho kwa UPk. Katika UPy kinakaguliwa sifa ya upatanishi wa yambwa ambavyo inawakilishwa na kiambishi {ki} kinachosimamia nomino kutoka ngeli ya 7. Kwa NJ kinakaguliwa njeo ya wakati uliopita inayowakilishwa na mofimu {li} na {ga} katika lugha ya Ks na Ek. Katika UPk kinakuguliwa sifa ya upatanishi kiima kwa sababu ya mofimu {Tu} na {To} zinazosimamia kiima. Lakini sifa hizi zote zinamotishwa kimofolojia tu, na kwa sababu hatuna uhusika wa kiima na yambwa hatuwezi kuukagua.

3.2.4.0 Hitimisho

Viambishi vya kitenzi katika lugha ya Ks na Ek katika uambishaji, vyote vinapatikana katika vitenzi vya lugha hizi. Tofauti ni kwamba, vinachukua nafasi tofauti, kama tulivyoonyesha. Viambishi vinyambuzi, vinachukua nafasi sawa katika vitenzi katika lugha hizi. Tofauti kuu katika unyambuaji kati ya Ks na Ek ni kwamba, lugha ya Ks ina viambishi vingi na alomofu nyingi zinazosimamia baadhi ya kauli zake. Kufanana kupo pale ambapo viambishi vya kauli kutendwa, kutendeka na kutendana.

Sura hii sasa itaweza kutufungulia sura ya 4 ambayo ndio mada yetu. ambayo ni KT, baada ya kuelewa muundo wa kitenzi. ambacho ni kwasi sana kimofolojia, kiasi cha kuweza kuwa KT chenye maana kamilifu kama sentensi sahili au kishazi.

TANBIHI

1. Tulirejelea Mohamed, M:A (2001) *Modern Swahili Grammar* Uk. 1
2. Maelezo ya TUKI (1990) tafsiri ya 'antecedent' kuwa kisabiki cha kiima.
3. Tumemnuuu Gesare (1992). The Morphology of nouns and verbs in Ekegusii (M.A. Thesis) Uk. 99.
4. Maelezo yake Prof. Abdulaziz, M (1996) *Transitivity in Swahili* Uk. 47.
5. Rejelea Ileri Mbaabu (1982) kwa maelezo zaidi kuhusu muundo wa mzizi wa kitenzi cha Kiswahili. Uk. 136.

SURA YA NNE

4.0.0 Utangulizi

Tumechambua vipashio mbalimbali katika sura ya pili na ya tatu, ambavyo vimetupatia mwangaza kuhusu mada yetu. Katika sura hii, tunatazamia kuchunguza muundo wa KT. Kisha tutazame matumizi ya nadharia ya uminimalisti katika KT cha lugha ya Ks na Ek. Kwa kutumia nadharia ya uminimalisti, tunaonyesha jinsi kanuni ya kukagua sifa inavyojitokeza katika KT cha lugha hizi, katika uundaji wa miundo.

4.1.0 Muundo Wa KT Sahili Cha Ks Na Ek

Katika sura ya kwanza, tulifanikiwa kueleza faslu ya KT kwa kuzingatia nadharia za mwanzo za Chomsky hadi nadharia ya Uminimalisti. Pia tuliona kuwa, katika kategoria ya virai, kuna KT ambacho kimuundo kinaweza kuchukua vipashio vifuatavyo:

1. Kitenzi (T) peke yake
2. Kitenzi kisaidizi (Ts) na kitenzi kikuu.
3. Kitenzi na kielezi (E)
4. Kitenzi na nomino au KN.
5. Kitenzi, nomino na kitenzi.
6. Kitenzi kisaidizi na kitenzi kisoukomo
7. Kitenzi, nomino (N) na kivumishi.
8. Kitenzi na kihusishi (H) au kitenzi kihusishi na nomino.
9. Kitenzi cha kuwa (kuwa na) na kijalizo.

Kutokana na mpangilio huu tunaweza kuhakikishiwa kuwa leksika kuu katika vipashio vya KT, ni T. Hakuna kirai tenzi bila kitenzi (T). Vipashio vingine vya KT ni nomino (N), kielezi (E), kitenzi kisaidizi (Ts), Kivumishi (V), kihusishi (H) na kijalizo (KJ).

Vipashio vya KT vinaweza kuzidi hivi, hasa ikiwa mtu anashughulikia muundo ambatani na changamani. Lakini, muundo huu tulioutoa ni sahili.

Vipashio vingine kati ya hivyo tulivyovitaja vya KT, tumevipitia tulipokuwa tunatazama muundo wa KN, kama vivumishi na nomino; Pia vitenzi visaidizi tumeviangalia katika sura iliyopita, sasa tuangalie vipashio vya vielezi na vihusishi kabla ya kuingilia ruwaza ya muundo wa KT kindani.

4.1.1.0 Muundo Wa KT Na Vielezi Katika Ks Na Ek

Vielezi ni maneno ambayo huongeza maana kwa kitenzi kwa kueleza jinsi kitendo kilivyotendeka, lini kilitendeka, wapi na mara ngapi. Vielezi katika lugha hizi ni vya aina nne;

- (i) Vielezi vya wakati.
- (ii) Vielezi vya mahali.
- (iii) Vielezi vya kiasi.
- (iv) Vielezi vya namna.

4.1.1.1 Vielezi Vya Wakati

Vielezi vya wakati huonyesha wakati kitendo kilipotendeka, kitakapotendeka hutendeka au hutarajiwa kufanyika. Vielezi vya wakati katika lugha ya Ek na Ks vinaweza kuwa nomino za majina ya miaka, miezi, siku au sehemu za nyakati fulani. Kwa mfano majina ya siku za juma na sehemu za nyakati zao katika Ks na Ek ni; Ijumaa (Enyongesa), Jumapili (Omokuβio), Jumatatu (Tichirimo), Jumanne, (Tichi kaβere), asubuhi (mambia), kesho (ankio), jioni (mogoroβa), juzi (moisonde), jana (igoro), usiku (βotuko), n.k. Tazama mifano katika sentensi.

1. Ks (i) Mgeni ameingia sasa hivi.

(ii) Mti ulikatwa Jumapili

Ek (i) **Omo-geni o-so-ir-e βono iga**.

Kb. ngeli 1 – mgeni kip. nafsi 3 umoja ingia – hali sasa hivi.

(Mgeni ameingia sasa hivi)

(ii) **Omo-te o-βutor-et-w-e omokuβio**.

Kb. ngeli 3 – mti kip ngeli 3 mzizi T kata – wkt pita – kauli tendwa – kiishio Jumapili.

(Mti ulikatwa jumapili)

Vielezi vya wakati husimamia matukio katika njeo na hali zote yanapotukia.

Vielezi vingi huwa ni mofimu huru katika lugha ya Ks na Ek. Tofauti tu, ni kwamba, Ks ina baadhi ya vielezi ambavyo ni funge vya kuashiria wakati kama **po- na – takapo-**.

2. Ks (i) Alipomwona alifurahi sana.

(ii) Utakapofika umjulishe mjomba.

Mofimu {-po-} huwa na matumizi mawili kisintaksia. Yale ya kuonyesha mahali na yale ya kuashiria wakati, kama katika mfano wa 2(i) ambapo wakati unaorejelewa ni uliopita kilipotendeka kitendo. Mofimu {-po} inaweza vilevile kurejelca wakati ujao inapotumika pamoja na {ta} na {ka} kama mfano wa 2 (ii).

4.1.1.2 Vielezi Vya Mahali

Vipashio hivi vya mahali huonyesha mahali ambapo kitendo kilitendeka, kitatendeka, kinatendeka au hutendeka. Huwa na nomino ya mahali au viashiria vya mahali majina ya pande za dira, n.k. Mfano.

3. Ks (i) Wageni walitoka Magharibi.

(ii) Nyoka anakaa humu.

Ek (i) **Aβa-geni βa-rw-et-e βosongo.**

Kb. ngeli 2 wageni kip.nafsi 3 wingi – mzizi T toka – wkt pita –
Kiishio Magharibi.

(Wageni walitoka Magharibi.)

(ii) **E-ng'iti n-emeny-et-e imaa.**

Kb. ngeli 9 nyoka kiy - kip – mzizi T ishi – wkt pita – kiishio ndani.

(Nyoka anakaa humu.)

Lugha ya Ks ina mofimu {ni} ambayo huashiria mahali inapoongezwa mwishoni mwa jina la mahali. Nomino ya mahali ikiwa na mofimu {-ni} mwishoni huwa na uamilifu wa kielezi cha mahali. Lugha ya Ek, haina mofimu {-ni} au yoyote inayoiwakilisha katika nomino. Mfano wa:

4. Ks: Mwalimu yumo darasani.

Ek **Omw-arimu n-ao a-re e-kerasi ime.**

Kb. ngeli 1- mwalimu kiy. kip. nafsi 3 umoja-kb mahali kip nafsi 3 umoja

Tsh.kuwa kb. ngeli 7 darasa ndani.

Mofimu zingine za vielezi vya mahali katika Ks ni kama {po, ko na mo}, ambazo mara nyingi huchukua nafasi zao katika vitenzi mfano:

5. (i) Alimwendea alipokuwa akilima.

(ii) Hafahamu aendako wala atokako.

(iii) Mle ndimo alimoishi kwa miaka kumi.

4.1.1.3. Vielezi Vya Kiasi

Kuambatana na Kapinga (1983) anaeleza kuwa vielezi vya kiasi hueleza tendo fulani limetukia mara ngapi. Vielezi hivi hugawika kwa makundi mawili, kwanza, vielezi vya kiasi, ambavyo hueleza idadi halisi ya kutendeka kwa kitendo. Vielezi vya idadi halisi hutoa idadi inayotoa orodha ya hesabu au maneno yanayofafanua idadi hiyo. Kwa mfano Ks (Ek); mara moja (mararimo), mara tatu (mara gatato), mara ya mwisho (mara yomoerio) n.k.

6. Ks Daktari humtembelea mara tatu kwa mwezi.

Ek **Omo-nyagitari a-ko-mo-tar-er-a mara gatato ase omo-tienyi.**

Kb. ngeli 1 – daktari kip. nafsi 3 umoja – hali mazoea + hali
kuendelea – kip yambwa – mzizi T tembea – hali – kiishio mara tatu
kwa mwezi

(Daktari humtembelea mara tatu kwa mwezi.)

Aina ya pili ya vielezi vya kiasi, ni vielezi vya jumla, ambavyo hutoa idadi kwa jumla tu kwa kujumuisha. Kwa mfano, Ks (Ek); mara nyingi (mara aange), kidogo kidogo (akeake) daima (rioka), kila (kera)n.k.

4.1.1.3 Vielezi Vya Namna

Kama neno lenyewe linavyodokeza, vielezi namna hueleza jinsi tendo lilivyotendeka. Vielezi vya namna huwa vya aina nyingi kuliko vielezi vingine vyote. Kuna (i) vielezi vya kufananisha, ambavyo mara nyingi hutumia mofimu {ki} kama kiambishi awali kinachooongezwa kwenye mzizi wa nomino au vivumishi vya Ks, na Ek hutumia {ge} au {ke}. Tazama mfano:

7. Ks anatembea kiume.

Ek **a-go-tar-a ge-sacha.**

Kip. nafsi ya 3 umoja - hali kuendelea – mzizi T tembea – kiishio kb-ngeli
7 – kiume.

(Anatembea kiume.)

Kielezi kiume (gesacha) hutokana na nomino mume (omosacha) ambayo mzizi wake ni {ume} {sacha} ambao umeongezewa awali viambishi vya kufanana ambavyo ni {ki-} na {ge} katika Ks na Ek. (ki + ume - kiume) (ge + sacha – gesacha).

Pia, vielezi vya namna vingine ni vile vya kueleza hali ambayo uhusiana na tabia ya kitu au mtu au mnyama. Vielezi vya hali huwa ni nomino dhahania. Kwa mfano; Ks (Ek) upesi (βwango), ubaya (οβοβc), utu (οβomwanyaβanto), wema (οβuya) n.k.

8. Ks Mlikimbia upesi

Ek **Mo-ka-minyok-a chimbero /βwango.**

Kip. nafsi 2 wingi – wkt pita – mzizi T kimbia – kiishio upesi.

(Mlikimbia upesi)

Vielezi vingine ni vya kuonyesha hali halisi ya kutendeka kwa jambo, hivi ndivyo hutumika sana. Vielezi hivi ni kama; sana (mono), bure (βosa), zaidi (βoire), polepole (ngo'ra) n.k.

9. Ks Mwizi alikamatwa akapigwa sana.

Ek **Omo-iβi a-ka-βwat-w-a a-ga-it-w-a mono.**

Kb. ngeli 1 iba kip nafsi 3 umoja – wkt pita – mzizi T shika – kauli tendwa – kiishio kip. nafsi 3 umoja – wkt pita – piga – kauli tendwa – kiishio mno.

(Mwizi alikamatwa akapigwa sana.)

Vielezi vingine vya namna hueleza kwa kurudiarudia kile kielezi mara mbili kwa njia ya kufululiza kwa kutoa maana jinsi kitendo kilivyotendeka. Lugha ya Ks ina mifano ya aina hii mingi kuliko Ek. Ek haitumii sana mtindo wa kurudiarudia kielezi, ingawa kuna mifano michache.

10. (i) Ks Walimbeba kijuujuu.

EK βakamoβogoria igorogoro.

Ks. Mlevi alianguka kifudifudi.

Ek. **Omotindu akagwa maumama.**

Vielezi vya sauti navyo huiga sauti ya kitendo kilivyofanyika chenyewe. Pia huitwa vielezi viigizi. Mifano yake hupatikana katika lugha ya Ks na Ek. Kwa mfano.

(i) Kuanguka mchangani tifu (kogwa cha)

(ii) Kuanguka majini chupwi (kogwa timbu)

(iii) Kupiga pa (goaka pa au mo)

Kapinga (1983) ameeleza kuhusu vielezi vitumizi ambavyo ni vyombo au vitu vinavyoweza kufanyika kwa kitendo fulani. Vielezi vitumizi huwa vya mguso na dhahania. Vya mguso ni vile vielezi vinavyoweza kushikika au kutoshikika na

matokco yanonekana kama vile, kisu (omoyio), upanga (eβeti), upepo (cmbeo), mikono (omokono), miguu (okogoro) n.k. Vielezi dhahania ni kama; makusudi, akili, siri, bidii n.k. Vielezi hivi huwa si vielezi bila usaidizi wa maneno; 'kwa' na 'na' katika Ks na 'no' katika Ek. Mifano.

11. (i) Ks Majambazi waliwakatakata kwa panga.

Ek Eβi-βago βi-ka-βa-βutoratorana ne-βeti.

Kb. ngeli 2 – majambazi kip. ngeli 7 – wkt pita – kip yambwa – katakata kiy – kip ngeli 9 panga.

(Majambazi waliwakatakata kwa panga.)

(ii) Ks Adui a-li-m-nyemele-a kwa siri.

Ek Omo-βisa a-ka-mo-choβer-a βoβosi.

Kb. ngeli 1 – adui kip. nafsi 3 umoja – wkt pita – kip yambwa – nyemelea kwa siri.

(Adui alimnyemelea kwa siri.)

Vielezi katika Ks vinaweza kuwa mofimu huru au mofimu funge ilhali kwa Ek huwa ni mofimu huru tu. Vielezi pia havitumiki kwa kuelezea vitenzi, bali vinaweza kueleza zaidi juu ya vivumishi na vielezi vingine. Tazama mifano:

12. (i) Msichana mrefu sana.

Omo-seko omo-tambe mono.

(ii) Ks. A-na-tembea polepole sana.

Ek. **A-go-tara ng'orang'ora mono.**

Kip. nafsi 3 umoja – hali kuendelea – mzizi T tembea polele mno.

(Anatembea pole pole sana.)

Mfano wa 12(i) ni mfano wa vielezi vinavyoeleza zaidi kuhusu kivumishi 'mrefu' (omotambe). Na 12(ii) ni mifano ya vielezi vinavyoelezea vielezi vingine zaidi, ambapo 'polepole' ni kielezi cha jinsi na 'sana' ni kielezi halisi.

4.1.2.0 Vihusishi vya Ks na Ek

Hivi ni vipashio vinavyotumiwa kuonyesha uhusiano fulani kati ya vitu viwili au zaidi, vitenzi viwili au baina ya fungu moja la maneno na lingine au neno na neno. Vihusishi asili katika lugha ya Ks huwa ni vichache navyo huwa vinajihusisha na irabu /a/ ya kutoa uhusiano wa kuunganisha. A-unganifu katika Ks kama kihusishi huambatanishwa viambishi vya ngeli za nomino, ndipo hutokea kuwa kwa mfano: ya , cha, za , wa, vya, pa, kwa n.k. Vipashio hivi hutumika pamoja na nomino zingine kama zile za wakati dhahania na mafungu mengine ya viwakilishi au maneno na kutoa vihusishi. Kwa mfano nyuma ya, upande wa, kwa fulani, mahali pa, nyumbani mwa n.k.

Lugha ya Ek ina vihusishi vya a-unganifu pia ambavyo vilevile huambishwa nomino za ngeli, na baadaye hutumika vikiwa vinaandamana na maneno mengine. Kwa mfano: inse ya (chini ya), nyomba mwa (nyumbani mwa), igoro ya (juu ya) n.k. Ek pia huwa na kihusishi 'o' ambacho hufanya kazi kama 'kwa' ya Ks'.

Mifano ya sentensi

13. (i) Ks Mtoto analala chini ya mti.
Ek **Omwana araire inse yomote.**
- (ii) Ks Anaishi kwa dadake.
Ek. **Amenyete omoiseke omwaβo.**
- (iii) Ks. Walienda kwa miguu.
Ek. **βachiete na magoro.**

Vihusishi 'kwa' na 'na' vina matumizi katika lugha ya Ks na Ek, kama tunavyoona kutokana na mifano. Kihusishi "kwa" cha Ks kimetokana na {ku- }ya mahali ya kitenzi kisoukomo kwa kuongezewa a-unganifu (ku + a) kisha irabu /u/ inabadilika na kuwa /w/ kwa sababu ya kufuatwa na irabu. Kihusishi 'kwa' katika Ek, kina maneno tofauti yanayotumika sawa nacho: Tazama sentensi za 13 (ii) na (iii) kuna 'o' na 'na' katika Ek, ambazo ni sawa na 'kwa' ya Ks kwa sababu Ek

hutumia vihusishi hivi kulingana na kile kinachoambatanishwa kimaana. Katika

Ks 'kwa' ina matumizi mengi kama:

- a) Kuishi au kukaa mahali .
Anaishi **kwa** mjomba wake.
- b) Kwenda mahali
Ameenda **kwa** Hamisi.
- c) Sababu za kutenda jambo.
Juma ameoa **kwa** kulazimishwa na wazazi.
- d) Kuonyesha vifaa au vyombo vya matumizi
Ninaandika **kwa** kalamu ya wino.
- e) Hukusudia kuonyesha bei.
Nilinunua nguo hii **kwa** bei ghali.

Ek kwa matumizi ya kihusishi 'kwa' huweza kufanya kazi kwa neno 'na' ambayo huambishwa kulingana na nomino inayohusishwa. Matumizi huwa sawa na yale 'kwa' Mfano:

14. (i) **Akamoita nomoyio**. (Alimwua kwa kisu)
- (ii) **Nigo twatarete namagoro**. (Tulitembea kwa miguu).

Aghalabu, Ek hutumia maneno mengine ya kuhusisha kama 'ase' (kwa) badala ya 'kwa' ya Ks kwa mfano

- (ii) **Anywomete ase okoβetereiwa**.
(Alioa kwa kulazimishwa)
- (ii) **Nagorete egetaβu ase rigori rinene**
(Nilinunua kitabu kwa bei ghali)

Lugha ya Ks ina vihusishi vya mkopo ambavyo lugha ya Ek haina. Vihusishi hivyo ni kama: **Katika, tangu, walau, hadi, bali, labda, kama, ila, kuzidi ama, lakini, n.k.** Kati ya vihusishi hivi, tungependa kutoa maelezo mafupi kuhusu kihusishi '**katika**' kwa sababu ni changamani kidogo kuliko vingine. 'katika' hutumika kutoa wakati, mahali na kufafanua hali fulani ambayo huhusishwa na kitenzi.

Tazama mifano hii ya 15.

15. (i) **Katika** mwezi uliopita, tulimwona.
(ii) Panya ameingia **katika** sanduku hii.
(iii) Tulijaribu kumfariji, lakini alikuwa **katika** majonzi mengi.

Sentensi ya (i) inaonyesha wakati, (ii) inaonyesha mahali na ya (iii) huashiria hali alimo mtu ambayo ni ya majonzi. Kuhusiana na mahali, kiambishi {-ni} kinaweza kutumika badala ya katika, au 'ndani ya' sentensi ya 15 (ii) inaweza kuandikwa hivi.

- (i) Panya ameingia ndani ya sanduku.
(ii) Panya ameingia sandukuni.

Lugha ya Ek haina mpangilio huu wa kuongeza 'ni' wala haina vihusishi vilivyokopwa kutoka lugha zingine kama Ks.

4.1.3.0 Muundo wa KT

Sehemu ya 4.1.0 tuliweza kutaja muundo wa KT. Kwa sasa, tunakusudia kutoa maelezo kwa ufupi ambayo yanaweza kutufungulia sehemu inayofuata.

- (i) KT kinaweza kuwa kitenzi (T) peke yake.

KT - T

Kitenzi ambacho kinaweza kusimama kama KT ni kitenzi chenye uwezo wa kuambishwa viambishi awali na tamati. Huwa katika Ek na Ks ni vitenzi vielekezi au visoelekezi (vikuu). Mfano:

16. Ks. Tu – ta-m-pig-a

Ek. **N- to-mo-it-e** (Tafsiri ya Ks)

Kiy-kip nafsi 1 wingi – kip yambwa – mzizi T piga – kiishio.

(Tutampiga.)

Kwa kuonyesha michoro inaweza kuwa hivi

T'

|

T

|

Tutampiga (Ntomoite)

- (ii) KT kinaweza vilevile kuwa kitenzi (T) na nomino au kiwakilishi nomino katika lugha ya Ks na Ek.

KT – T + N.

17. Ks (i) Tu-li-m-pig-a m-toto.

Ek (ii) **To-ka-mo-it-a omw-ana**

Kip nafsi 1 wingi – wkt pita – kip yambwa – mzizi T piga kb ngeli
- mtoto

(iii) Ni-ta-ku-pig-a wewe.

N-ko-go-it-a-n-de aye. (Tafsiri ya K)

Kiy – hali kip yambwa –mzizi T piga – kiishio – kip nafsi 1
umoja – hali – kiishio / njeo wewe.

(Nitakupiga wewe.)

Mchoro wake utakuwa.

KT

|

T'

|

T

|

N/W

Tulimpiga mtoto

Nkamoita omwana

Nitakupiga wewe

Nkogoitande aye.

- (iii) KT kinaweza kubeba nomino na kivumishi katika lugha hizi mbili. Nomino inayofuata kitenzi, huwa na uamilifu wa yambwa kisarufi. Kivumishi baada ya nomino huvumisha nomino. Hebu angalia mifano huu.

18. Ks. Tu-li-m-pig-a m-toto huyo.


Ek. To-ka-mo-it-a omw-ana o-yio.

Kip. nafsi 1 wingi – wkt pita – kip yambwa – mzizi T piga – kiishio kb.

ngeli 1 – mtoto kip. nafsi 3 umoja – kionyeshi.

(Tulimpiga mtoto huyo.)

Mifano hii inaweza kuchukua mchoro mmoja kama.



Kutokana na mchoro huu tunaweza kuona kuwa KT kinamiliki 1, N, na V katika lugha hizi kimuundo.

(iv) KT Kimuundo kinaweza vilevile kuchukua au kubeba kitenzi, na nomino mbili au tusema KN.

KT - T + KN (TNN).

19. Ks. M-pat-i-e mw-alimu ki-tabu.

Ek. Ka-e omw-arimu ege-taβu.

Kip. yambwa – mzizi T patia – kiishio kb. ngeli 1 – mwalimu kb ngeli 7 kitabu.


(Mpatie mwalimu kitabu.)

Nomino zikiwa mbili huwa zimekubaliwa na kitenzi katika kirai au sentensi.

Kisarufi, uamilifu wa nomino hizo kama 'mwalimu' (omwalimu) na 'kitabu'

(ege-taβu) ni yambwa. Nomino 'mwalimu' (omwalimu) ni yambwa tendewa ilhali nomino inayoandama nayo 'kitabu' ni yambwa tendwa. KT hiki kimejengwa kwa

kuunganisha kitenzi nomino na nomino nyingine. Tazama vipashio hivi vinavyounda KT katika mchoro huu.



- (v) KT kinaweza kujengwa na vipashio vya kitenzi kisaidizi, kitenzi kikuu na nomino.

$$KT = Ts + T + N.$$

Mfano wa KT katika lugha ya Ks na Ek ni kama hapa chini.


20. Ks. Tu-na-taka ku-imba wimbo.

Ek. **N-to-ganati-e go-tera ogo-tera**

Kiy. kip nafsi 1 wingi – mzizi Ts taka – kiishio hali ya kuendelea – imba kb ngeli 5 wimbo .

(Tunataka kuimba wimbo.)

Mfano huu umetumia kitenzi kisaidizi 'taka' (gania), ambacho kimeungana na kitenzi kikuu 'imba' (tera) kikiwa kitenzi kisoukomo, na nomino nayo imeungana na vipashio Ts na T ili kuunda KT. Katika muungano huu, neno kuu ni kitenzi leksika. Tazama Mchoro.



- (vi) KT cha Ks na Ek kinaweza kujengeka kutokana na kitenzi na kielezi (E) au kirai kielezi (KE).

KT – T + E / KE

Mifano katika sentensi ni.

21. (i) Ks A-na-m-pend-a sana.

Ek **A-mw-anch-et-e mono.**

Kip. nafsi 3 umoja – kip yambwa – mzizi T penda – wkt pita – kiishio sana.

(Anampenda sana.)



- (ii) Ks A-me-lim-a sana tangu asubuhi.

Ek **O-rem-ir-e mono korwa mambia**

Kip. nafsi 3 umoja -mzizi T lima – hali timilifu – kiishio sana tangu asubuhi.

(Amelima sana tangu asubuhi.)

Sentensi 21 (i) zinaonyesha muundo wa kirai ambacho kina kitenzi na kielezi, na (ii) ni mifano ya sentensi au virai, vyenye kitenzi na kirai elezi (KE). Michoro ya muundo huu ni kama ifuatavyo.



(vii) KT – T Kishirikishi cha kuwa + V/U/N/E.

Massamba nw (1999:103) wanapendekeza kuwa KT kinaweza kuundwa na kitenzi kishirikishi pamoja na vipashio vingine kama kivumishi kiunganishi(u), nomino au kielezi. Kama tulivyotaja hapo awali, vitenzi vishirikishi hufuatwa na viajalizo ambavyo huwa uamilifu wao ni kufafanua zaidi juu ya nomino iliyotajwa. Hata hivyo, vipashio vya KT vinaweza pia kuwa vipashio vya kileksika vinavyomilikiwa na KT. Tazama na kuchunguza mifano ifuatayo:

22. (i) KT – kuwa + V/KV.

Ks A-me-kuwa m-rembo sana.

Ek **O-βe-ir-e omo-nyakieni mono.**

Kip. nafsi 3 umoja – Ts kuwa – hali timilifu – kiishio kb ngeli 1 – mrembo mno.

(Amekuwa mrembo sana.)



(ii) KT – kuwa + kielezi (E) + T

Ks I-li-kuwa vema ku-mzuru.

Ek **Ya-renge βuya ko-mo-tarera.**

Kip. nafsi ya 3 umoja – Ts kuwa vizuri kb ngeli 15 – yambwa – tembelea.

(Ilikuwa vema kumzuru.)



KT ni muungano wa vipashio mbalimbali vikiwa vinaongozwa na leksika kuu ambayo ni kitenzi. Maelezo haya ni fasiri ya Sarufi Miundo Virai, (SMV) ambayo ilizingatia kuwa sintaksia ina miundo ya virai mbalimbaili kama; NK, KT, KV, KE, KH na KU. Wanasarufi miundo walizingatia kuwa sentensi sahili, ina virai viwili ambavyo ni KN na KT. Sentensi hiyo sahili, walisema ilipatanishwa na kiima ambacho ni KN chake. Tumetumia maelezo ya KT sahili kama SMV, ambapo KT ni kirai kilicho na uamilifu wa kuarifu. Tukiangalia nadharia ya uminimalisti, inadai kuwa sentensi sahili ni KT. Rejelea maelezo yetu katika kazi hii sura ya I.

Kwa sababu ya mipaka ya nadharia yetu na kanuni zake, tumeweza kushughulikia KT kama sentensi sahili vilevile ili kukagua sifa za uhusika katika kuchunguza spesifaya katika kichwa cha upatanishi wake. Kutokana na wazo hili la KT kuwa ni sentensi sahili, tunaweza kuwa na mfano ufuatao, katika lugha hizi mbili tunazochunguza.

23. Ek Aβa-na n-go-som-a-βa-re ege-taβu.

kb. ngeli 2 – watoto kiy- hali kuendelea – mzizi T soma – kiishio –
kip nafsi 3 wingi – hali kitabu.


(Watoto wanasoma kitabu)

Ks Wa-toto wa-na-soma ki-tabu.

Vipashio vya KT hiki ambavyo vimeunganishwa ni watoto(aβana) + wanasoma (ngosomaβare) + kitabu (egetaβu)

KT – N + T + N.

Kielelezo.



Kutokana na mchoro huu, tunaweza kuona kuwa kuna tofauti kati yake na mchoro ya ile ya kwanza ya KT. Tofauti hii imetokana na kutumia nomino (kiima) ambayo imepelekea kuunda kwa kichwa cha spesifaya ambacho hakikuwa katika KT za awali. Nomino watoto (aβana) ina uamilifu wa kiima na hupatanishwa na KT chenye uamilifu wa kuarifu kupitia kwa kiambishi awali kinachowakilisha nomino 'mtoto (omwana)' ambacho ni {a-} katika Ks na {-a-} katika Ek inayochukua nafasi ya pili toka mwisho. Kwa maelezo zaidi rejelea sura ya 2 na 3 ili kuelewa zaidi kuhusu nomino na viambishi. Nomino (kiima)


zote zinapatishwa na vitenzi katika lugha hizi. Iwapo KT katika uminimalisti kina nomino zenye uamilifu wa yambwa mbili, muundo wake utakuwa hivi kama hapa chini kimchoro.

24. Ks Baba a-me-nunu-li-a m-toto ki-tabu.

Ek Tata o-mo-gor-e-ir-e omw-ana ege-taβu.

Baba kip. nafsi 3 umoja – yambwa – mzizi T nunua – kauli tendea – hali – kiishio kb. ngeli 1 umoja mtoto kb. ngeli 7 kitabu.

(Baba amemnunulia mtoto kitabu.)



Katika sehemu hii, tumejaribu kuonyesha jinsi leksika zinazopatikana katika leksikoni zinavyoweza kuungana kuunda miundo ya KT, baada ya kupitia numerali hatua ya kuchagua leksika kutoka leksikoni. Vipashio vya kilekiska na vya kisarufi hutolewa kwenye leksikoni vikiwa vimeambishwa tayari. Katika hatua ya muungano, leksika hizo zinaungana na kuunda muundo wa kisintakisia uwe virai, vishazi au sentensi.

4.2.0 Mtazamo wa uminimalisti na KT cha Ks na Ek

Nadharia ya uminimalisti inadai kuwa lugha asilia huwa na vitengo viwili muhimu ambavyo husaidia kuzalisha miundo mbalimbali katika lugha yoyote ile.

Chomsky (1995b:168) anasema kuwa

“lugha ina vitengo viwili: leksikoni na mifanyiko ya kimkokotoo”. (TY)

Kitengo cha leksikoni hufafanua faridi zinazolingia katika mifanyiko ya *kimkokotoo* na sifa zao. Uchanganuzi wa faridi hizo (ambazo huwa ni leksika zote na sifa zote za kisarufi) hufanywa kupitia kwa michakato ya numerali. Faridi za kimofosinstaksia na zile za kileksika *huungana*. *Mifanyiko ya kimkokotoo* huanza pindi tu *numerali* imekamilisha jukumu lake la kuchagua faridi zinazounganishwa. Muundo huu mwishoni hujitokeza katika *mjumuiiko* ambao huwakilisha maumbo mawili: *Umbo la kifonetiki na umbo la kimantiki*.

Katika kitengo cha mifanyiko ya *kimkokotoo*, tunapata kanuni na nadharia mbalimbali hujitokeza kwa kazi mbalimbali ili kuhakikisha kuwa muundo ulioundwa unafikia kiwango cha *kuungana na kuingiana* kabla ya *mdhihiriko wazi*. *Mifanyiko ya kimkokotoo* hujuimuisha hali na hatua zote za kujenga miundo hadi kwa *mjumuiiko*. Vilevile huonyesha ujenzi wa miundo katika vilelezo matawi kwa mujibu wa *kanuni ya ukaguzi wa sifa na usogezi wa leksika mbalimbali*.

Kwa mfano, ikiwa kuna muundo ulioundwa tayari wa KT kama.

(a) Ks. A-li-som-a ki-tabu.

Ek. N-a-som-et-e ege-taβu

Kiy-kip. nafsi 3 umoja – mzizi T – wkt pita – kiishio kb. ngeli 7-
kitabu.

(Alisoma kitabu.)

Kisha katika kuendelea kuunda miundo, tunaweza kuunganisha kiima, ambacho *kitaunganishwa* katika kifundo cha KUPk katika kichwa cha SPE. Mfano sasa itakuwa.


(b) Ks. Maria a-li-soma ki-tabu

Ek **Maria n-a-som-et-e ege-taβu.**


Maria kiy. – kip nafsi 3 umoja – mzizi T soma – wkt pita – kiishio kb. 7 kitabu.

(Maria alisoma kitabu).

Kielelezo cha (a)



Sasa kielelezo matawi hiki kinaonyesha KT bila nomino ya kiima. Tukiwa na muundo wa kujenga kielelezo kingine, ambacho kitaongezewa kiima 'Maria' muundo utakuwa hivi.




Jinsi miundo inavyojengwa katika uminimalisti kupitia kuunganisha vipashio, ndivyo vielelezo matawi vinvavyokuwa, kwani ni sharti kanuni ya *iktisadi* itimizwe kwa kupitia KUK. Kwa jumla, *mifanyiko ya kimkokotoo* huanzia *numerali* ambapo leksika huchaguliwa za kuunda miundo, *kuungana* kwa leksika na vipashio vingine vya kisarufi na kimofolojia, usogezi ambao hushurutishwa na kanuni ya *'usogezi wa mwisho'* na mdogo zaidi, kanuni ya *kucheleweshwa* na ile ya *ubinafsi*, *kukagua* sifa kwa masharti ya KUK, na mwisho kwa *mdhihiriko* wazi ambao hutoa uwakilishi wa kifonetiki na ule wa kimantiki.

Haja yetu kuu, ilikuwa kuchunguza jinsi nadharia ya *kukagua sifa* inavyoweza kutumika katika KT cha lugha hizi mbili. Kwa sababu tulikuwa tunashughulikia muundo na upatanishi wa KT, cha lugha ya Ks na Ek, tuliweza kuangalia

matumizi ya nadharia hii katika ujengaji wa miundo na usogezi wa vipashio vya T na N.

Chomsky ametoa muundo wa kimsingi wa sentensi sahili au KT kuwa kama hapa chini. Muundo huu unaweza kufanyiwa marekebisho na upangaji wa vifundo na vichwa hufanywa kwa kutegemea muundo unaoundwa.



4.2.1 Nadharia ya kukagua sifa

Je, ni sifa gani zinazokaguliwa katika KT? Kwa nini sifa zikaguliwe? Haja kuu ya kukagua sifa katika miundo fulani ni kuhakikisha kuwa sifa au faridi zisizoeleweka na ambazo zinaweza kupotosha maana ya muundo katika mdhihiriko wazi zinatolewa katika harakati za kuzalisha miundo. Nadharia ya kukagua sifa ni muhimu katika uminimalisti kwa sababu, nadharia ya uminimalisti haina lile umbo la nje lilokuwa katika Sarufi Zalishi Geuza Maumbo (SZGM). Kwa hiyo kukagua sifa ni kanuni iliyochukua nafasi ya maumbo nje na ndani katika sintaksia ya uminimalisti.

Nadharia ya uminimalisti, inahitaji sifa za kimofolojia. Sifa hizi za kimofolojia, huwakilishwa katika sifa za kisarufi kisintaksia ambazo hujumuisha njeo, uhusika na upatanishi. Sifa hizi huwa zimeambishwa kategoria leksika kutoka kwa *leksikoni*. Uamilifu wa sifa hizi huwa ni katika hatua ya *mifanyiko ya kimkokotoo*, na wala hazina maana yoyote katika maumbo ya kifonetiki na kimantiki. Kwa hivyo, sifa hizo hazitakiwi kutokea katika mjumuiko kwani zitasababisha kugongana katika kuzalisha muundo.

Katika lugha hizi (Ks na Ek) kategoria amilifu za njeo, upatanishi na yambwa huambishwa T na hukaguliwa katika T kinaposogezwa juu ili kuepukana na sifa za mgongano. Vifundo vya Up (upatanishi) na Nj (njeo) hubeba sifa za kimofolojia zinazoambishwa T na N. Up pia hubeba sifa zingine zenye uamilifu wa kisarufi kama vile idadi, nafsi na kundi la nomino. Kwa sababu ya sifa hizi, Chomsky (1995b) anadai kuwa vichwa amilifu¹ hutawala jozi ya sifa kuliko mofimu halisi ambazo hupatikana katika leksika kimofolojia. Kwa mfano:

26. Ks. A-li-imb-a

Ek. A-ga-ter-a

Kip. nafsi 3 umoja wkt pita mzizi T imba – kiishio.

(Aliimba)

Kiambishi cha upatanishi wa kiima {a} kinakaguliwa katika UPk na kile cha njeo {li} / {ga} kinakaguliwa kwa NJ badala ya kukaguliwa kwa T.

Nadharia ya kukagua sifa, hukubalia uundaji wa maneno kileksika na kisintaksia kukaguliwa ikiwa tu sifa hizo za kukaguliwa zinajitokeza waziwazi katika T au N. Kwa mfano, sifa za spesifaya hukaguliwa kwa kichwa cha SPE yenyewe kwa nia ya kukagua uhusika wao.

27. Ks M-toto a-na-som-a.

Ek **Omw-ana n-go-som-a-re.**

Kb. ngeli 1 mtoto kiy – hali kuendelea - mzizi T soma – kiishio –kip nafsi 3 umoja - hali.

(Mtoto anasoma.)

Sifa za uhusika wa 'mtoto (omwana)' zitakaguliwa kwa SPE ya KUPk. Kwa sababu uamilifu wa nomino mtoto (omwana) kisintaksia ni ule wa kiima kwa hiyo sharti ukaguliwe kwa spesifaya ya kirai kipatanishi kiima (KUPk).

Nadharia ya uminimalisti hudai kuwa, muundo wa virai au sentensi zilizounganishwa huwakilishwa katika umbo la kifonetiki (UF) na umbo kimantiki (UM). Kwa hiyo, sentensi au kirai kilicho sahihi kisarufi, sharti kiwakilishe viwango viwili vya kisarufi, umbo kifonetiki na umbo kimantiki. Ni kupitia kwa maumbo haya wanasarufi wanaweza kufafanua miundo kiisimu katika kiwango cha mjumuiko. Umbo la kifonetiki huwakilisha sifa zinazoweza kufafanuliwa au kuelezwa kifonetiki na umbo la kimantiki huwakilisha sifa zinazoweza kufafanuliwa kimantiki. Sifa hizi zikifafanuliwa katika viwango hivi huwa basi masharti ya *kanuni ya ufafanuzi wa kina* (KUK) yametimizwa.

Kanuni ya ufafanuzi wa kina (KUK) hudai kuwa,

Uwakilisho wa umbo sharti uwe na sifa pekee ambazo zinaweza kuchangia ufafanuzi wa umbo hilo tu kistahiki. Kwa hiyo, sifa pekee ambazo zinawakilisha umbo kifonetiki sharti ziwe zile za kudhihirisha ufafanuzi wa umbo kifonetiki, na vilevile, sifa pekee za kuwakilisha umbo kimantiki huwa tu ni sifa zinazojidhihirisha tu katika umbo mantiki. Radford (1997:171) (Ty).

Ikiwa uzalishaji wa umbo fonetiki unatimiza masharti za KUK basi muundo ulioundwa unasemekana kuwa *umekutana* (converge) katika UF, na ikiwa uzalishaji wa muundo unatimiza masharti ya KUK katika UM, husemwa kuwa *umekutana*, na hivyo kufikia mahitaji ya KUK.

Kwa kuwa sifa zinazoweza kufafanuliwa kifonetiki hujumuishwa tu katika UF, na za kisemantiki hufafanuliwa katika UM. basi tunajiuliza, je sifa za kisarufi zina hadhi gani? Sifa za kisarufi huwa ni zile ambazo zinafanyakazi katika michakato ya kisarufi (kimofolojia na kisintaksia) nazo ni:

- (a) Idadi: Sifa ya idadi husaidia katika sarufi ya upatanishi. Idadi huonyesha umoja au wingi wa vipashio kisintaksia. Kwa mfano ngeli ya 3/4 katika lugha ya Ks na Ek tuna.

Ks: Mti - miti (umoja na wingi)

Ek: Omote – emete (umoja na wingi).

- (b) Jinsia: Sifa hii hupatikana katika lugha zile ambazo zinatofautisha jinsi ya kiume na kike kama Kiingereza. Sifa hizi huwa na jukumu katika sintaksia kuelezea anafora ya kujirejea. Kwa mfano katika Kiingereza 'she' pronomino ya jinsia ya kike sharti iende sambamba na hali ya kujirejea ya 'herself'.

Katika lugha za kibantu tunaweza kupendekeza kuwa, jinsia ni sifa inayotofautisha makundi ya nomino katika ngeli, kiasi kwamba nomino ya kundi la ngeli moja haiwezi kuwakilisha nomino ya kundi la ngeli nyingine. Kwa mfano, tukisema 'mti umekatwa' nomino 'mti' haiwezi kuwakilishwa na nomino kutoka ngeli nyingine, kama vile 'nyumba' ya ngeli 9/10. *nyumba umekatwa. Sentensi hii si sahihi katika sarufi ya Ks. Suala hili la jinsia huwa lina uwakilishi wa UF na UM hasa katika lugha za Kibantu.

- (c) Nafsi: Sifa za nafsi kama tulivyozishughulikia katika sura ya pili, zina majukumu ya kisintaksia katika kupatanisha kiima na T.

- (d) Sifa za kimofolojia: Hujumuisha zile sifa zinazoambishwa vitenzi kama sifa za pronomino (viwakilishi) katika vitenzi, njeo n.k.

kutokana na mfano ufuatao, tunaweza sasa kuona jinsi sifa hizi zinavyojitokeza.

Ks. Msichana a-na-som-a.

Ek. **Omo-iseke n-go-som-a-r-e.**

Kb. ngeli 1 msichana kiy – hali kuendelea – mzizi T soma – kip
nafsi 3 umoja – hali – kiishio.

Kwa kuzingatia kuwa huwa mpaka dhahiri upo kati ya sifa za kisarufi na zile za kisemantiki kwa sababu sifa za kisarufi za nomino ‘msichana’ ‘(omoiseke)’ huonyesha kuwa ni katika ngeli ya 1 umoja na ni nomino yenye uamilifu wa kiima, ‘anasoma (ngosomare)’ ni T kilicho na upatanishi wa kiima nafsi ya tatu kwa wakati uliopo. Sifa hizi za kisarufi, baadhi zinaweza kufafanuliwa na zingine haziwezi kufafanuliwa kisemantiki. Kama upatanishi wa kiima katika nafsi ya tatu ($\{a\}$) haifafanuliwi kisemantiki kwa sababu ujumbe huo unaelezewa na nomino (kiima) yenyewe ambayo ni ‘Msichana’ (Omoiseke). Pia hairejelei tu ‘msichana’ peke yake bali pia nomino yoyote katika kundi hilo la ngeli umoja. Kwa hiyo vipengee muhimu vya kisemantiki ni vile vinaweza kufafanuliwa kisemantiki ili kufikia lengo la KUK. Vipengee visivyoweza kufafanuliwa huondoshwa na kufutwa. Ikiwa sifa hizo zisizofafanuliwa kisemantiki huondolewa, zinaondolewa vipi? Na ni kwa jinsi gani neno kuu (kichwa) linaweza kuchukua ili kuchagua kijalizo na spesifaya iliyo na sifa zinazohitajika? Kwa kujibu, ni muhimu kukumbuka kuwa nadharia ya uminimalisti inatumia kanuni ya *kukagua sifa na usogezi wa leksika*.

Nadharia hii pia inachukulia kuwa kategoria ya maneno inabeba seti za sifa za kisarufi ambazo ni:

- (1) Sifa za spesifaya ambazo huamua ni spesifaya gani ya kategoria za kileksika zinachukua.
- (2) Sifa za neno kuu (kichwa) ambazo hutambulisha sifa zinazochukuliwa na kategoria leksika.
- (3) Sifa za kijalizo, pia hutambulisha aina ya kijalizo ambacho leksika itachukua (Radford 1997a:174 –175)

kutokana na mfano ufuatao, tunaweza sasa kuona jinsi sifa hizi zinavyojitokeza.

Ks. Msichana a-na-som-a.

Ek. **Omo-iseke n-go-som-a-r-e.**

Kb. ngeli 1 msichana kiy – hali kuendelea – mzizi T soma – kip
nafsi 3 umoja – hali – kiishio.

Kwa kuzingatia kuwa huwa mpaka dhahiri upo kati ya sifa za kisarufi na zile za kisemantiki kwa sababu sifa za kisarufi za nomino ‘msichana’ ‘(omoiseke)’ huonyesha kuwa ni katika ngeli ya 1 umoja na ni nomino yenye uamilifu wa kiima, ‘anasoma (ngosomare)’ ni T kilicho na upatanishi wa kiima nafsi ya tatu kwa wakati uliopo. Sifa hizi za kisarufi, baadhi zinaweza kufafanuliwa na zingine haziwezi kufafanuliwa kisemantiki. Kama upatanishi wa kiima katika nafsi ya tatu ({a}) haifafanuliwi kisemantiki kwa sababu ujumbe huo unaelezewa na nomino (kiima) yenyewe ambayo ni ‘Msichana’ (Omoiseke). Pia hairejelei tu ‘msichana’ peke yake bali pia nomino yoyote katika kundi hilo la ngeli umoja. Kwa hiyo vipengee muhimu vya kisemantiki ni vile vinaweza kufafanuliwa kisemantiki ili kufikia lengo la KUK. Vipengee visivyoweza kufafanuliwa huondoshwa na kufutwa. Ikiwa sifa hizo zisizofafanuliwa kisemantiki huondolewa, zinaondolewa vipi? Na ni kwa jinsi gani neno kuu (kichwa) linaweza kuchukua ili kuchagua kijalizo na spesifaya iliyo na sifa zinazohitajika? Kwa kujibu, ni muhimu kukumbuka kuwa nadharia ya uminimalisti inatumia kanuni ya *kukagua sifa na usogezi* wa leksika.

Nadharia hii pia inachukulia kuwa kategoria ya maneno inabeba seti za sifa za kisarufi ambazo ni:

- (1) Sifa za spesifaya ambazo huamua ni spesifaya gani ya kategoria za kileksika zinachukua.
- (2) Sifa za neno kuu (kichwa) ambazo hutambulisha sifa zinazochukuliwa na kategoria leksika.
- (3) Sifa za kijalizo, pia hutambulisha aina ya kijalizo ambacho leksika itachukua (Radford 1997a:174 –175)

Kulingana na sifa hizi, neno kuu (kichwa) hukagua sifa za spesifaya na kijalizo. Sifa za spesifaya ya neno kuu hutumiwa kukagulia sifa za neno kuu la spesifaya hiyo. Vilevile sifa za kijalizo cha neno kuu, hukagua sifa za neno kuu za kijalizo. Hivyo ndivyo sifa hukaguliwa na sifa zisizoweza kufafanuliwa hufutwa. Tazama mfano huu.


28. Ks. M-sichana a-na-pik-a ndizi.

Ek. **Omo-iseke n-ko-rug-a-re ritoke.**

Kb. ngeli 1 msichana kiy – hali kuendelea – mzizi T pika – kiishio-
kip nafsi 3 – hali ndizi

(Msichana anapika ndizi.)


Tulitaja awali kwamba, lugha za Kibantu, ambapo Ek na Ks hujumuishwa, zina upatanishi imara kuliko lugha ya Kiingereza, ambayo ina upatanishi dhaifu. Kwa sababu lugha ya Ks na Ek zina upatanifu imara, kategoria leksika ambazo ni T na N, zitasogezwa juu ili kukagua sifa zao za kisarufi. Tazama kielelezo hiki cha Ks.



Kutokana na mchoro huu wa Ks, tunaona vifundo vinatokana na vichwa amilifu kisarufi. Kitenzi 'anapika' kinachochukua nafasi ya T inayotokana na KT na kichwa T' kinazogezwa hadi kwa UPk ya UPk'. Kitenzi hiki kinapitia nafasi UPy ya UPy' kwa ajili ya kukagua sifa za upatanishi yambwa na kinaacha athari zake (at) kwa kusogezwa hadi kwa NJ ya NJ' kwa sababu ya kukagua sifa za njeo (hali). Kitenzi hiki kiko katika njeo iliopo au hali inayoendelea {na} ambayo imeambishwa kwa mzizi 'pika'. Kitenzi hiki, kina sifa za njeo iliyoopo ambayo inakaguliwa kwa kichwa cha NJ. Pia kuna sifa za kundi la ngeli ya 1 umoja kuonyesha kuwa spesifikaya ya kitenzi hiki inayohitajika ni ile ya uhusika kiima au

bila kiima, kwa sababu lugha hizi zinadondosha nomino kiima na kitenzi kikawa ni kirai au sentensi inayojisimamia kikamilifu kimaana.

Nomino kiima 'msichana' inasogezwa hadi kwa SPE ya KUPk kwa minajili ya kukagua sifa za uhusika kiima ambazo ni idadi, kundi la ngeli na upatanishi na kitenzi. Kwa kuwa sifa hizi za neno kuu zinafanana na sifa za spesifaya, hatuna haja ya kukagua sifa za kundi la ngeli, idadi na nafsi kwa hiyo zinafutwa. Sifa hizi zinazofutwa hazina maana yanayofafanuliwa kisemantiki. Hebu tutazame vile nomino yambwa inavyobadilisha nafasi yake kwa kusogezwa toka kwa kichwa cha KN hadi kwa SPE ya KUPy kwa mintarafu ya kukagua sifa za uhusika yambwa. Tazama mfano wa muundo wa Ek.



Miundo ya kielelezo hiki inaonyesha tofauti iliyo kati ya lugha hizi mbili kimuundo. Ingawa sentensi au KT ni sawa kimaana na jinsi vipashio vya kisintakisia vilivyounganishwa. kielelezo hiki cha Ek kinatofautiana na kile cha Ks. Tumeunda vifundo vingine zaidi ambavyo havikuwa katika Ks. Kifundo cha KIY ya KIY' hakikuwa katika Ks. Kichwa cha KIY kimeundwa kwa kusudi la *kukagua sifa* ya upatanishi wa kiuyakinishi kwa kutumia spesifaya ya T. T cha Ek kina sifa za idadi, kundi la ngeli, njeo na nafsi ambayo ni ya tatu umoja na uyakinishi. T kinasogezwa toka T ya T' hadi kwa UPy kwa mintarafu ya kukagua sifa za upatanishi yambwa, kisha kwa HAL kwa kukagua sifa za hali ambayo ni ya wakati uliopo. Kutoka kwa HAL, T kinasogezwa hadi kwa kichwa cha UPk cha UPk' kwa kukagua sifa za upatanishi na kiima kisha kwa KIY kwa ajili ya ukaguzi wa sifa ya hali yakinishi. Sifa za spesifaya ya T katika Ek zinafanana na zile za nomino kiima na kwa hivyo zinafutwa ili kutimiza masharti ya *kanuni ya ufafanuzi wa kina* (KUK) ambayo inadai kuwa sifa zisizofafanuliwa kisemantiki zifutwe.

Kwa sababu ya kukagua uhusika, Nomino kiima ya 'Omoiseke (msichana)' inasogezwa hadi kwa nafasi ya SPE ya KUPk, ili kuhakikisha uhusika kiima wa nomino. T huhitaji kijalizo ambacho ni nomino katika ngeli yoyote lakini kisiwe kiwakilishi (pronomino). Nomino yambwa inasongezwa juu hadi kwa SPE ya KUPy ili kukagua sifa za upatanishi yambwa na uhusika yambwa.

Kufikia hapa tumeonyesha jinsi nadharia ya *ukaguzi* wa sifa inavyofanya kazi katika lugha ya Ks na Ek. Hebu sasa tutazame *usogezi na ukaguzi* wa sifa katika KT.

4.2.2 Usogezi na ukaguzi wa KT

Nadharia ya uminimalisti inadai kuwa usogezi katika KT hufanywa ikiwa tu kitenzi hicho (au leksika yoyote ile), ina sifa thabiti za upatanishi zinazokiwezesha (T) kusogezwa ili kuzikagua sifa hizo. Marantz (1995) anaelezea dhana za upatanishi thabiti na upatanishi dhaifu. Upatanishi dhaifu haukubalii kusogezwa

kwa kategoria leksika kwa sababu hakuna sifa za kukaguliwa. Lugha ya Kiingereza upatanishi wake ni dhaifu. Upatanishi wa lugha ya Ks na Ek, tunauona kuwa thabiti na ndio sababu ya kusogeza leksika ili kukagua sifa kabla ya kufikia mdhihiriko wazi.

Kanuni ya *iktisadi* chini ya uminimalisti inadai kuwa kusiwe na nafasi tupu au elementi zaidi, bali miundo ya kisintaksia iwe na elementi zinazowakilisha sintaksia. Viambajengo vidogo zaidi vitumike kutoa maelezo na nadharia za sintaksia katika virai na sentensi kikamilifu. Hii ni mojawapo ya sababu za kujumuisha mofolojia katika sintaksia.

Usogezi na kanuni ya *iktisadi* ni sehemu kuu za ujengaji miundo kisintaksia Chomsky (1995b) anasema mifanyiko ya kimkokotoo ya kuunganisha leksika na miundo midogo ili kuunda miundo mikubwa kuliko ile ya awali huitwa *muungano*. *Mifanyiko ya kimkokotoo* hujumuisha numerali, kuungana, kujenga miundo, usogezi na ukaguzi wa sifa, mdhihiriko wazi na mjumuiko ulio na uwakilishaji wa kifonetiki na wa kimantiki.

Lugha ya Ks na Ek, KT kinaweza kuundwa kwa leksika moja ya kitenzi ambayo aghalabu uambishwa kwa kipatanishi cha kiima, njeo, idadi, na mara nyingine T kinachukua yambwa. Tazama mfano huu.


29. Ks. Wa-li-zi-chom-a

Ek. **Ba-ga-chi-samba-a.**

Kip. nafsi 3 wingi – wkt pita – kip yambwa – mzizi T choma – kiishio.

(Walizichoma)

Kt hiki, kina sifa zote zinazohitajika katika kuunda virai. KT hiki kina kipatanishi kiima {wa (β a)} cha ngeli ya wingi, njeo ya wakati uliopita {li(ga)}, kipatanishi yambwa {zi(chi)} shina la kitenzi {chom} (samba) na kiishio {a} cha lugha za kibantu kuonyesha dhamira ya kutenda. Kielelezo matawi kwa ajili ya kusogeza na kukagua sifa ni kama ifuatavyo.



T kimesogezwa toka T ya T' hadi kwa UPy ya UPy' ili kukagua sifa za upatanishi yambwa, hadi kwa NJ ya NJ' ili kukagua sifa za njeo na mwisho kwa UPk ya UPk' kwa kukagua sifa za upatanishi kiima. Kupitia kwa mfano huu, tunasema na kusisitiza kuwa, lugha ya Ks na Ek zina ukwasi mkubwa wa kimofolojia ambao hukifanya kitenzi kuwa KT au kishazi kinachojisimamia kisarufi. Mifano mingine ya virai tenzi itagusia kauli mbalimbali za kitenzi katika KT, huku tukionyesha usogezi na ukaguzi kwa kutumia vichwa amilifu kimofosintaksia.

4.2.3.0 Uchanganuzi Wa KT Kwa Kutumia Kanuni Ya Kukagua Sifa

Uchanganuzi huu unaelekea kuonyesha jinsi sifa za kimofolojia na kileksika zinavyoweza kukaguliwa katika KT cha Ks na Ek. Tumechunguza sifa za kisarufi ambazo hukaguliwa kwa nia ya kuonyesha upatanishi kimofosintaksia na jinsi vipashio hivyo vinaunda muundo fulani wa kisintaksia. Kwa mujibu wa mada yetu, tumechunguza KT katika kauli mbalimbali.

4.2.3.1 Ukaguzi wa sifa katika KT cha Ks na Ek

4.2.3.2 KT katika kauli ya kutenda

KT katika kauli ya kutenda huonyesha nomino kiima ambayo hutenda kitendo. Katika lugha ya Ks na Ek, KT kinaweza kuwa na nomino kiima au iwe nomino imedondoshwa na maana ibakie kuwa kamilifu.

Kwa mfano.


30. Ks M-toto a-li-chez-a m-pira.

Ek Omw-ana a-ka-gosori-a omo-bira.

Kb. ngeli 1 mtoto kip. nafsi 3 umoja – wkt pita – mzizi T cheza –
kiishio kb ngeli 3 mpira.

(Mtoto alicheza mpira.)

KT hiki kina leksika tatu ambazo ni nomino, kitenzi na nomino. Leksika hizi zina uamilifu wa kiima, kiarifu na yambwa. Nadharia ya uminimalisti inapendekeza zaidi matumizi ya faridi kiuamilifu. Katika kukagua sifa, tutakagua sifa za upatanishi, njeo na uhusika. Kukagua sifa, hufanya vipashio mbalimbali kusogezwa ikiwa zinakubaliwa kimofolojia na kileksika. Kimofolojia vipashio husogezwa kwa kukagua sifa za upatanishi na njeo, na kileksika vipashio husogezwa kwa kukagua uhusika wa kiima au yambwa katika lugha ya Ks na Ek. Tazama kielelezo matawi kifuatacho cha KT hapa juu.



Kutokana na kielelezo matawi hiki tunaweza kuona kuwa N yenye uamilifu wa yambwa katika N ya T' imesogezwa hadi kwa SPE ya KUPy kwa nia ya kukagua sifa za uhusika. Kitenzi kimesogezwa juu kutoka kwa T ya T' ya KT kwa hatua ya kwanza ambapo inatua kwa UPy ya UPy' ili kukagua sifa zake za upatanishi yambwa, kisha kinasonga hadi kwa NJ ya NJ' kwa nia ya kukagua njeo ambayo ni ya wakati uliopita, mwisho hadi kwa UPk ya UPk' kukagua sifa za upatanishi kiima. Kiima kinasogezwa mara moja tu kutoka SPE ya KT hadi kwa SPE ya KUPk ili kukagua sifa za uhusika kiima na upatanishi.

4.2.3.3 KT katika kauli ya kutendwa.

Kauli ya kutendwa hugeza yambwa katika kauli tenda kuwa kiima kwa kuongezewa mofimu {w} katika lugha hizi. Kwa mfano:

31. Ks (i) **Yohana a-me-kat-a m-ti.**

(ii) M-ti u-me-kat-w-a na Yohana.

Ek (i) **Yohana o-nach-ir-e omo-te.**

Kip. nafsi 3 – mzizi T kata – hali timilifu kiishio kb ngeli 3 mti.

(Yohana amekata mti.)


(ii) **Omo-te o-nach-ir-w-e na Yohana.**

Kb. ngeli 3 mti kip - mzizi T hali timilifu kata – kauli tendwa – kiishio na Yohana.

(Mti umekatwa na Yohana.)

KT za (i) ziko katika kauli ya kutenda zile za (ii) ni katika kauli ya kutendwa.

Tazama kielelezo.



Kutokana na kielelezo hiki tunaona kuwa vipashio ambavyo haviwakilishwi kimofolojia au kukubaliwa kimofolojia na kileksika kukagua sifa zao, havisogezwi. Kirai kihusishi katika KN hakiruhusiwi kusonga kwani hakina kibali hicho kimofosintaksia. Kitenzi katika T (umekatwa) kinasogezwa hadi kwa kifundo cha W ya W' ambacho huonyesha kauli ya kutendwa au kutendewa kwa nia ya kukagua sifa za kutendwa, tena kinasogezwa hadi kwa NJ ili kukagua njeo ambayo ni hali timilifu, mwisho kinasogezwa hadi kwa UPk ya UPk' kwa mintarafu ya kukagua sifa za upatanishi. SPE ya KT inasogezwa hadi kwa SPE ya KUPk kwa nia ya kukagua sifa za upatanishi na uhusika kiima. Kauli hii inaweza kubadili vitenzi katika kauli ya kutendea na kuwa katika kauli ya kutendewa. Kauli ya kutendea na kutendewa zinaweza vilevile kuchukua KN tatu katika lugha hizi. ambapo mfano ni:

32. KS (i) Rukia a-li-m-piki-a mama ch-akula
(ii) Mama a-li-pik-i-w-a ch-akula na Rukia.
- Ek (i) **Rukia a-ka-mo-rug-er-a βaβa e-ndagera.**
Kip. nafsi 3 umoja – wkt pita – kip yambwa- mzizi T pika –
kauli tendea – kiishio mama kb ngeli -chakula.
- (ii) **βaβa a-ka-rug-er-w-a e-ndagera na Rukia.**
Kip. nafsi 3 umoja – wkt pita - mzizi T pika – kauli tendea –
kauli tendewa - kiishio kb ngeli 9-chakula na Rukia.

Katika sentensi za (i) Rukia ndiye kiima, na zile za (ii) mama ndiye kiima.
‘chakula’ ni yambwa tendwa na mama ni yambwa tendewa. Sasa swali ni
kwamba mama tena anawezaje kuwa kiima katika kauli tendewa? Rukia ana
uamilifu upi? Tazama kielelezo matawi kifuatacho, ndipo tupate majibu ya
maswali haya.

33. Ks (ii) Mama a-li-pik-i-w-a ch-akula na Rukia
- Ek (ii) **βaβa a-ka-rug-er-w-a e-ndagera na Rukia.**
Mama kip nafsi 3 umoja wkt pita – mzizi T pika – kauli
tendea – kauli tendewa kiishio kb. ngeli 9 – chakula na Rukia
(Mama alipikiwa chakula na Rukia)

'mama(βaβa)' tunaitambua kuwa kiima kwa sababu kiupatanishi inachukua mofimu {a} ambayo inapatanisha viima katika kundi la nomino la ngeli ya 1. Ni muhimu tukumbuke kwamba, vipashio vinavyosogezwa, huacha athari zao nyuma (a) ambazo zinaweza kufuatiliwa kama nyayo zao⁷.

4.2.3.4 KT katika kauli ya kutendea kiulinganishi.

Kauli hii katika lugha ya Ks na Ek, humaanisha tendo linafanywa kumfaidi mwingine au kumsadia na hata kumduru. Ks hutumia mofimu {i} na Ek kauli hii huonyeshwa kwa mofimu {er-}. Mfano:


34. Ks. Wa-me-m-pik-i-a m-gonjwa ch-akula.

Ek. βa-mo-rug-e-ir-e omo- rwaïr-e e-ndagera.

Kip nafsi 3 wingi – kip yambwa – mzizi T pika – hali – kauli tendea – kiishio kb. ngeli mgonjwa kb ngeli chakula.

(Wamempikia mgonjwa chakula.)

Ukitazama kielelezo matawi hiki kinachofuata, utaona kuwa vifundo vinabadilisha nafasi kuambatana na mpangilio wa maundo uliozalishwa kupitia mifanyiko ya kuungana. KT hiki kimeongeza kifundo cha nomino inayofaidi kutokana na kifundo ambacho tumekiita IA kwa kuonyesha upatanishi kati ya T na N. Lugha ya Ks na Ek zimeafiki kielelezo hiki kutokana na mfano hapo juu.



Katika kielelezo hiki, leksika ya T na yambwa zimepata kibali cha kusogezwa kupitia kwa mchakato wa kuunda miundo, ili kukagua sifa za upatanishi na hali, kwa kutimiza malengo ya KUK. Mtendewa ambaye ni 'mgonjwa (omorwaire)' amepewa kichwa cha SPE kwa nia ya kukagua sifa za uhusika kwa agiumentu ya 'chakula (endagera)' katika uwakilishi wa kuunda muundo, mtendewa (mtendewa) anapewa SPE kwa KEA (kirai tendewa) ili kujiepusha na nomino kukaguliwa sifa za uhusika maradufu kwa KT.


Pia katika kielezo hiki, hatuna kifundo cha SPE ya kiima, kwa sababu muundo msingi wa sentensi au KT, katika uminimalisti unaruhusu tu vifundo na vichwa vilivyojengwa katika mchakato wa uzalishaji wa sentensi. na *kanuni ya iktusadi* haikubalii nafasi tupu, kwa sababu KT hiki hakikuwa na SPE ya kiima' haionyeshwi katika kielelezo vilevile

4.3.3.5 KT Katika kauli ya kutendesha.

Vitenzi katika kauli ya kutendesha huonyesha hali ya kusababisha. Hali hii hufanya yambwa kutenda tendo kwa kusababishwa na kiima na mofimu yake ni {ish} kwa Ks (kumbuka kauli hii kwa Ks huwa na alomofu zaidi ya mofimu hii {ish}) Lugha ya Ek hutumia mofimu {i} kuonyesha kauli hii kwa mfano.

35. Ks. A-li-m-l-ish-a m-toto ch-akula
 Ek A-ka-mo-rager-i-a omw-ana e-ndagera.

Kip. nafsi 3 umoja- wkt pita – kip yambwa – mzizi T kula - kauli ish
 – kiishio kb. ngeli mtoto kb ngeli 9 chakula.
 (Alimlisha mtoto chakula.)



Tazama vile T kinavyosogezwa kutoka kwa T ya T' hadi kwa UPy ya UPy' kwa sababu ya kukagua sifa za upatanishi na yambwa. Tena hakitulii katika nafasi hii kinasonga tena juu hadi kwa ISH ya ISH' ili kukagua sifa za kauli ya kutendesha. T kinasogezwa tena juu kwa NJ ya NJ' ili kukagua sifa za njeo, ambayo imeonyeshwa kuwa ni ya wakati uliopita katika sentensi hizi. Mwisho T kinatulia kwa UPk ya UPk' ambapo kinachekeki sifa za upatanishi kiima. Ingawa kiima kimedondoshwa, katika lugha hizi, KT huwa kamilifu hata bila kiima (nomino kiima) na kiambishi awali {A (o)} kinaashiria nomino inayotendesha ambayo ni kiima.

Kuambatana na nadharia ya uminimalisti, sentensi au KT hukaguliwa kwa kusogezwa juu kutoka chini. Ndivyo, nomino yambwa inasogezwa juu kupitia kwa hali ya kujenga miundo hadi kwa SPE ya KUPy ili kukagua sifa za uhusika yambwa; nomino yambwa tendewa ambayo inasababishwa kutenda tendo inasogezwa toka kwa N ya T', hadi kwa SPE ya KEsh ili kukagua sifa za spesifaya katika T kwa kauli ya kutendesha. T' inatawala T, N na N.

4.3.4.0 KT Jirejee (anafora)

Sifa za KT jirejee cha Ks na Ek zinafanana. Mofimu zao huwa ni {ji} kwa Ks na {e} kwa Ek Schroeder (2002 : 47-48) anaeleza kuwa katika uundaji wa miundo, KUK hulazimisha sifa za kimofolojia kukaguliwa na kichwa kikaguzi³ katika kichwa chake. Kwa hiyo, KT cha kujirejea kinahitaji kukaguliwa kwa kichwa fulani. Anasema kwamba

“ inapendekezwa sifa za kujirejea zikaguliwe katika kichwa cha UPy kwa sababu mofimu ya kujirejelea inawakilisha yambwa ya KT au sentensi. (TY).

Mfano:


36. Ks. Baba a-li-ji-pik-i-a.

Ek **Tata a-ka-e-rug-er-a.**

Baba kip. nafsi 3 umoja - wkt pita –kip jirejee – mzizi T pika – kauli tendea – kiishio

(Baba alijipikia)

Hebu sasa tugeukie kielelezo tuone jinsi miundo inavyoundwa katika KT cha kujirejea ambacho ni:



Sifa za kimofolojia za T zinazokaguliwa katika mfano huu ni zile za viwakilishi vinavyoashiria njeo, kwa NJ, jirejee katika UPy ya UPy' na upatanishi katika UPk ya UPk'. Kiambishi cha kujirejelea {ji, e} kinafanya kazi kama yambwa; ndio sababu ya kukikagua kwa kichwa cha UPy.

Radford (1997:114-6) anaeleza jinsi anafora katika uminimalisti zinavyochukua kibainishi kiima kinachohusiana nacho.

4.2.5 KT katika hali yakinishi na ya kukanusha.

Ukanusho katika nadharia ya uminimalisti huundiwa kifundo chake ambacho hutangulia kile cha upatanishi UPk, kwa sababu katika lugha ya Ks na Ek, mofimu za ukanusho hutangulia mofimu za kiima cha upatanishi. Mfano:

38. (i) Ks. A-li-m-pig-a m-toto vibaya

Ek. **A-ka-mo-it-a omw-ana** βoβe.

Kip. nafsi 3 umoja-wkt pita – kip yambwa – mzizi T piga –
kiishio kb. ngeli 1 mtoto vibaya.

(Alimpiga mtoto vibaya)


(ii) Ks. Ha-ku-m-pig-a m-toto vibaya.

Ek. **T-a-mo-it-et-i mwana** βoβe.

Kb. kukana –kip nafsi 3 umoja – kip yambwa – mzizi T piga
– wkt pita – kiishio. Kb. ngeli 1 mtoto vibaya.

(Hakumpiga mtoto vibaya.)

Kielelezo matawi katika hali ya ukanushi huwa hivi:



T Katika muundo huu wa Ks na Ek, kimesogezwa hatua nyingi juu kwa kukagua sifa mbalimbali kama ilivyoonyeshwa. Mwisho kinafikia, KAN (hali ya kukanusha) ya KAN' kwa kukagua sifa za ukanusho kiupatanishi. Kwa kuwa KT hiki hakina SPE ya kiima, pia haionyeshwi katika kukagua sifa. Kielezi (E) hakina sifa ya kukaguliwa, kinabakia bila kusogea popote.

4.2.6 Njeo Na Hali

Tulilazimika kueleza mambo muhimu ya kimuundo kuhusu njeo na hali katika lugha ya Ks na Ek kwa sababu ya tofauti zinazojitokeza (Rejelea sura ya 3) Njeo na hali katika lugha ya Ks, hazibadilibadili nafasi zao katika KT, bali lugha ya Ek inabadilii sana. Niivile mofimu ya hali ya uya kinishi katika lugha ya Ek, ambayo huchukua nafasi ya kwanza katika KT kwa wakati fulani, hutoa muundo unaotofautiana na wa Ks. Kwa mfano, tulieleza kuwa KT katika Ek kilicho katika njeo iliyopo, iliyopita, na hali inayoendelea, hutumia kiambishi cha hali ya



uyakinishi tofauti na Ks. Katika kujenga miundo kupitia kuunganisha vipashio, tunapata kuwa KT cha Ks na Ek huchukua muundo tofauti. Ek hujenga kifundo cha KIY juu hatua zaidi kuliko Ks ambayo humalizia UPk. Tazama mfano huu:

39. Ks. Wa-li-lim-a

Ek. M-ba-rem-et-e.

Kiy-kip nafsi 3 wingi-mzizi T lima – wkt pita – kiishio.

Ks



Kwa kuchunguza vielelezo matawi hivi, tunaona kifundo cha juu katika Ks ni UPk' ambayo kichwa chake ni UPk inayotumiwa kukagua sifa za upatanishi wa T. Ek imemalizia kifundo cha KIY ya KIY' ambapo hali ya uyakinishi inaweza kukagulia sifa zake za upatanishi na T. Sifa za njeo za T zinakaguliwa katika NJ ya NJ'.

Tumetumia wakati huu kuonyesha tofauti kati ya Ks na Ek kwa kujenga miundo na kukagua sifa kwa wakati uliopita. Njeo zingine katika Ks na Ek zinafanana wakati wa kutumia moJimu za njeo hizo zingine kwa kuzikagua.

Kufikia hapa tumekuwa tukitumia vitenzi vikuu (vitenzi vielekezi na visoeiekezi) kwa kueleza ukaguzi wa sifa na uundaji wa miundo. Hebu tuone mfano wa vitenzi vingine.

4.2.7 KT kinachotumia vitenzi visaidizi.


Ukaguzi wa sifa za kimofolojia katika KT chenye vitenzi visaidizi, hufanywa kwa kukagua sifa za kisarufi ambazo ni njeo, upatanishi na uhusika. Mfano wa KT kilicho na vitenzi visaidizi ni:

40. Ks Makori a-li-tak-a ku-nywa maji.

Ek **Makori a-tag-et-e ko-nywa amache.**

Makori kip. nafsi 3 umoja – Ts taka – wkt pita – kiishio – kb. kiso – kunywa maji.

T na Ts vinavyotokana na KT vimekaguliwa pamoja kwa UPY kwa kuangalia sifa za upatanishi yambwa. Njeo hukaguliwa kwa NJ na Upatanishi wa kiima unakaguliwa kwa UPk ya UPk'. Sifa za spesifaya ya yambwa inayotokana na N ya T', zinakaguliwa kwa SPE ya KUPy, na sifa za spesifaya ya kiima katika SPE ya KUPk.




Kutokana na kielelezo matawi hiki, kitenzi kisoukomo 'kunywa (konywa)' kinakaguliwa katika kichwa cha KISO ya KISO' na kitenzi kisaidizi taka kinakaguliwa sifa za upatanishi yambwa kwanza katika UPy ya UPy' kisha njeo katika Nj ya NJ' na kutulia kwa UPk ya UPK' kwa sifa za upatanishi kiima. Spesifaya ya maji (amache)' inakaguliwa uhusika katika SPE ya KUPy' na Spesifaya ya Makori inasogezwa hadi SPE ya KUPk kwa kukaguliwa uhusika kiima.

4.2.8 KT kinachotumia vitenzi vishirikishi

KT chenye kitenzi kishirikishi hakina yambwa, badala yake huchukua kijalizo. Kwa hiyo, sifa za spesifaya za yambwa hazikaguliwi. Tazama mfano.

41. Ks. Moraa ni mwalimu.
Ek. **Moraa no mwalimu.**

Kielelezo matawi.




T kinaonyesha njeo ya wakati uliopo, kwa hiyo kinasogezwa juu kwa NJ kukagua sifa za njeo na sifa za upatanishi katika UPk ya UPk'. Sifa hizi za njeo na upatanishi zinakaguliwa katika kifundo kimoja kwa sababu zimechanganyikana. Spesifaya 'Moraa' inatoka kwa SPE ya KT na kusogezwa hadi kwa SPE ya KNJ kwa lengo la kukagua sifa za uhusika wake kama kiima. Upatanishi wa kiima hauna ushahidi wa kimofolojia kwa hivyo haukaguliwi.

Vitenzi vishirikishi vya 'kuwa na' vyenye nomino yenye uamilifu wa yambwa hukaguliwa uhusika wake kama spesifaya ya N. Tazama mfano.

42. Ks Maria a-na ki-tabu.
Ek **Maria n-a-bwate ege-taβu.**

Maria kiy. kip nafsi 3 umoja – kitenzi kuwa na kb ngeli 7 – kitabu.

(Maria ana kitabu.)



Si vishirikishi vyote vyenye yambwa, vingine huwa na uamilifu wa kujaliza tu na havisogezwi wala havikaguliwi sifa. Kwa mfano vishirikishi vya 'kuwa' vinavyochukua kijalizo cha kuvumisha, kama.

43. Ks. Maria ni mkali.

Ek. **Maria nomotindi.**

Kijalizo 'mkali' ni kivumishi kwa hiyo hakisogezwi juu kwa sababu hakina sifa za uhusika za kukaguliwa. Hata hivyo, kivumishi 'mkali (omotindi)' kina sifa za upatanishi wa kiima kimofolojia lakini nadharia hii haitoi sababu za kutoweza kukagua sifa hizo, na wapi zitakaguliwa. Tungependekeza kuwa sifa za upatanishi wa kiima na kivumishi hiki zikaguiwe katika UPk kwa sababu upatanishi wake ni ule wa kiima.


4.2.9 KT Cha Swali

KT kilicho katika umbo la swali huweza kukaguliwa sifa kuambatana na mpangilio wa viwakilishi vya maswali nafasi vinavyochukua. Kwa mfano kiulizi 'nani' katika KT kifuatacho kinachukua nafasi ya kwanza ambapo kina uamilifu wa kiima. Kama kiima, kiulizi hiki kitakaguliwa sifa za spesifaya katika SPE ya KUPk. Mfano.

44. Ks. Nani a-li-iba kalamu?

Ek. Ng'o o-ib-et-e e-kalamu?

Kiulizi – kip nafsi 3 umoja- mzizi T iba – wkt pita – kiishio kalamu
(Nani aliimba kalamu.)



Kiulizi 'nani' kinasimamia nomino kiima kiuamilifu, kwa sababu inayouliziwa ndiye mtenda wa kitendo cha kuiba. Kwa hiyo 'nani {ngo}' inachukua nafasi ya SPE baada ya kusogezwa toka kwa SPE ya KT, kwa nia ya kukagua sifa za uhusika kiima. T 'aliiba (oibete)' kinakaguliwa sifa zake katika UPy, NJ na UPk. Yambwa inasogezwa hadi kwa SPE ya KUPy.

Lakini, kiulizi kama 'vipi na wapi' vifuatavyo vinachukua nafasi ya vielezi katika kujenga miundo hivyo hakuna kukagua sifa zao kwa sababu hazikubaliwi kukaguliwa kimofolojia au kileksika. Kiulizi nini (nki) katika sentensi (iii) kinawakilisha na kuashiria yambwa, na kwa hiyo huweza kukaguliwa sifa za spesifaya ya yambwa.

45.

- (i) Ks Maria a-li-chez-a vipi?
Ek. **Maria nanki a-gosor-eti-e?**
Maria vipi kip. nafsi 3 umoja – mzizi T cheza – wkt pita – kiishio
(Maria alicheza vipi?)
- (ii) Ks Maria a-me-end-a wapi?
Ek. **Maria ng'ai a-ge-end-a?**
Maria wapi kip. nafsi 3 umoja – hali – mzizi T enda – kiishio.
(Maria ameenda wapi.)
- (iii) Ks Maria a-li-ib-a nini?
Ek. **Maria inki a-iβ-et-e?**
Maria nini kip. nafsi 3 umoja – mzizi T iba – wkt pita - kiishio
(Maria aliiba nini)

4.3.0 Hitimisho

Kufikia hapa tumejaribu kuonyesha jinsi kanuni ya kukagua sifa inavyoweza kutumiwa. Tumconyesha jinsi ya kukagua sifa za KT chenye vipashio mbalimbali vya kimofo-sintaksia. Lengo kuu la kufanya ukaguzi wa sifa kabla ya kufikia mdhihiriko wazi na mjumuiko ni kujiepusha na sifa ambazo haziwezi kufafanuliwa kuambatana na masharti ya kanuni ya ufafanuzi wa kina. Sifa za spesifaya na kijalizo za T haziwezi kufafanuliwa katika kiwango cha UM, kwa hiyo zinafutwa, na kubakia sifa zile tu zinazoweza kufafanuliwa katika UM (umbo mantiki).

TANBIHI

1. Vichwa amilifu ni tafsiri ya 'functional heads.'
2. Nyayo ni tafsiri ya 'Foot steps' katika maelezo ya Trace.
3. Kichwa kikaguzi ni tafsiri ya Head checker.

5.0 HITIMISHO

Utafiti wetu ulikuwa unashughulikia KT cha lugha ya Ks na Ek, kwa kutumia nadharia ya uminimalisti katika kulinganisha KT cha lugha ya Ks na Ek, tuliweza kugundua mambo kadha wa kadha ambayo yanaling'ana na mengine kutofautiana. Kwa kufanana, KT cha lugha hizi huchukua vipashio vinavyofanana ambavyo ni T, (kama neno kuu) N,V,E,Ts na H. Kwa hiyo viambajengo vya KT cha lugha hizi mbili vinafanana.

KT katika lugha hizi, kinaweza kuchukua tu T ambacho huambishwa viambishi awali na viambishi tamati mbalimbali. T kinaweza pia kuwa sentensi sahili katika lugha hizi. Kwa hiyo tulifikia kwamba, nadharia ya uminimalisti inayoona sentensi kama KT, ina mashiko makubwa katika lugha hizi kwa sababu KT kinaweza kubeba ujumbe unaoweza kubebwa na sentensi sahili. Kwa hiyo, KT ni sentensi sahili (kishazi).

Katika kuangalia muundo wa KT, tuliweza kuona tofauti kubwa ya mpangilio wa viambajengo vya njeo na hali, na viambishi vinavyoashiria kiima, katika Ek na Ks. Pia, tulifikia kuwa lugha ya Ek inatumia toni kwa kutofautisha njeo mbalimbali kinsintaksia. Kwa hivyo tulifikia nadharia tete yetu kuhusu toni kuwa ina uamilifu wa kimofo-sintaksia.

Kuhusu upatanishi wa KT, tuliweza kufikia kuwa KT cha Ks na Ek, kina upatanisho wa kiima, yambwa tendwa na yambwa tendewa. KT katika lugha hizi pia kina mofolojia kwasi ambayo hukifanya KT kujisimamia kama sentensi sahili. Usogezi wa viambajengo katika KT hufanywa kwa nia ya kukagua sifa za kisarufi za viambajengo hivyo. Ukaguzi wa sifa hufanyiwa sifa kimofolojia, na vichwa na vifundo huundwa kwa kutumia sifa amilifu za kimofolojia ambazo hukaguliwa. Sifa zisizofasiriwa au fafanuliwa kisemantiki zinafutwa na kubakia sifa zinazofasiriwa kisemantiki katika kiwango cha mjumuiko cha ujengaji miundo.

Nadharia ya uminimalisti kwa kukagua sifa, inaongozwa zaidi na sifa za kimofolojia na kilekska. Kwa hiyo, uchanganuzi wowote wa kutumia nadharia hii sharti ushughulikiwe kimofosintakisa. Mofolojia kama kitengo cha uundaji wa maneno kina nafasi kubwa katika sintaksia ya lugha hizi mbili.

5.1 MAPENDEKEZO

Kwa sababu lugha hukua na kuendelea, tunapendekeza kwa wanaisimu wengine kuweza kushughulikia ulinganishi wa lugha zingine kwa kutumia nadharia hii ya uminimalisti. Utafiti wetu ni mwanzo tu wa jaribio la kuangalia KT katika uminimalisti kwa hiyo hatukushughulikia vipengele vyote vya nadharia hii. Pia tungependekeza kuwa, wanafunzi wanaoweza kufanya utafiti wa lugha, waweze kushughulikia KN cha lugha hizi mbili kiulinganishi, kwa kutumia nadharia ya uminimalisti ijapokuwa tumegusia KN, hatukukiangalia kindani inavyostahili utafiti.

Kwa kuwa tulikuwa tunashughulikia KT, maswala mengi kama njeo, hali, dhamira na toni katika lugha ya Ek, hatukuyachunguza kwa kina. Kwa hiyo, ni vema kwa mwanafunzi yeyote wa isimu anayetaka kufanya utafiti kindani, afanye kwa kutumia nadharia ya uminimalisti.

MAREJELEO

- Abdulaziz, M.H. (1996) *Transitivity in Swahili*. Rudigen Kopper Verlag; Koln
- Bakari M. (1982) The Morphophonology of the Kenyan Swahili Dialects. PhD Thesis, University of Nairobi. (Haijachapishwa)
- Baya, F.M. (1993) Kitenzi Kisaidizi cha Kiswahili Sanifu Mtazamo wa Sarufi Geuza Maumbo Zalishi. Tasnifu ya M. A. chuo kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)
- Chomsky, N (1957) *Syntactic Structures*. The Hague Monton .
- _____ (1965) *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge. Massachusetts.
- _____ (1993) Aminimalist Program for Linguistic Theory in K. Hale and S.J Keyser (eds) *The view from Building 20 Essays in Linguistics in Honor of Syirain Bromberger*. MIT Press: Cambridge, mass.
- _____ (1995) *The minimalist program*. The MIT press Cambridge, mass
- Cook, V. na Newson, (1996). *Chomsky's Universal Grammar: An Introduction*. Blackwell: Oxford.
- Crystal, D. (1999) *A Dictionary of Linguistics and Phonetics 5th ed*. Blackwel Publishers Oxford.
- Der,Houssikian, H. (1969) Noun Class and Concords in Kimombasa. PhD Thesis University of Texas; Austin (Haijachapishwa).

- Gesare, H.L. (1992) A Morphological Typology of Ekegusii in a Structural Framework. M.A. thesis University of Nairobi (Haijachapishwa).
- Gicheru, D.K. (1999) Ulinganishi wa Muundo Wa Kikundi Nomino cha Kiswahili Sanifu na Kikuyu cha Kabete. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi (Hakijachapishwa)
- Guthrie, M (1948) *Comparative Bantu*. (v2) Oxford University Press London.
- Haegeman, L (1994) *Introduction to Government and Binding Theory – 2nd Ed.* Blackwell: Oxford.
- Horrocks, G. (1987) *Generative Grammar*. Longman Ltd: UK.
- Johnston, H.W. (1919) *A Comparative study of the Bantu and Semi-Bantu Languages*. Oxford University Press: London.
- Kawa, A. (2003) The Syntax of Noun Phrase Movement in Kiswahili. M.A. Thesis Kenyatta University. (Haijachapishwa).
- Manyora, H B. (1992) Intra-sentential Relationships of Logooli NPS; A Government and Binding Approach. M.A. Thesis University of Nairobi; (Haijachapishwa).
- Marantz, A. (1995) The Minimalist Program katika G Webelhuth *Government and Binding Theory and the Minimalist Program: Principles and Parameter in Syntactic Theory*. Blackwell. Oxford.
- Massamba, D et al (1999) *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*. Tuki: Dar es Salaam
- Massamba D.B (2004) *Kamusi Ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Tuki: Dar es salaam.

- Mayaka, B.A. (2000) *The Structure of Ekegusii Sentences. A Transformational Generative Approach.* B.A. Thesis University of Nairobi (Haijachapishwa).
- Mdee, J.S (1986) *Kiswahili Muundo na Matumizi yake* Intercontinental Publishers Ltd: Nairobi.
- Mgullu, R.S. (1990) *The Structure of Swahili Sentences. A Transformational Approach.* M.A. thesis University of Nairobi (Haijachapishwa)
- Mogambi, H.M. (1998) *Upatanisho wa Kisarufi Katika Sintaksia ya Kiswahili: Mtazamo wa Umilikifu na Masharti.* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).
- Myachina, E.N. (1981) *The Swahili Language- A Descriptive Grammer.* OUP: London.
- Olali, T.M. (1997) *Kikundi Nomino Cha Kiswahili. Mtazamo wa Sintaksia ya X-Bar.* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa)
- Omusula, F.B (1998) *Ulinganishi wa Mifanyiko ya Kimofonolojia Baina ya Mnyambuliko wa Kitenzi cha Kiswahili na cha Kikabarasi.* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)
- Osinde, K.N. (1998) *Ekegusii Morphophonology: An Analysis of the Major Consonantal Process.* M.A. Thesis University of Nairobi (Haijachapishwa).
- Polome, E (1967) *Swahili Language Handbook.* Centre for Applied Linguistics: Washington D.C.
- Radford, A. (1997) *Syntactic Theory And The Structure of English Aminimalist Approach.* Cambridge University Press; Cambridge.


- _____ (1997_b) *Syntax, Minimalist Introduction*. Cambridge University Press: Cambridge.
- _____ et,al (1999) *Linguistics. An Introduction*. Cambridge University Press. Cambridge.
- Schroeder, H (2002) *Word Order in Toposa. An Aspect of Multiple Feature-checking*. PhD Thesis University of Nairobi (Haijachapishwa).
- TUKI (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Tuki: Dar es -salaam.
- TUKI (2000) *English – Swahili Dicctionary 2nd edition – University of Dar – es – salaam*.
- Vitale, A. (1981) *Swahili Syntax*. Foris Publications Holland.
- Yule, G. (1996) *The Study of Language 2nd ed*. Cambridge University Press. United Kingdom.



Tafsiri za dhana zilizotumiwa

1. Athari - trace
2. Gongana - crash
3. Kanuni iktisadi - Economy principle
4. Kanuni ya kuchelewesha - Principle of procrastinate
5. Kanuni ya usogezi mfupi – Principle of shortest move.
6. Kanuni ya ubinafsi – Principle of greed
7. Kanuni ya ufafanuzi wa kina – Principle of full interpretation
8. Kifundo - Node
9. Kijalizo (Kij) – Complement
10. Kishazi kikuu - Main clause
11. Kitambulishi leksika – Lexical marker
12. Kitambulishi husika –Case marker
13. Kitendeshi - Causative marker
14. Kitita cha sifa dhahania – Bundles of abstract features.
15. Kukutana - converge
16. Kuungana – Merge
17. Kirai kipatanishi yambwa (KUPy) – Phrasal agreement object
18. Kirai kipatanishi kiima (KUPk) –Phrasal agreement subject
19. Leksikoni - Lexicon
20. Lugha asilia - Natural language
21. Mdhihiriko wazi – Spell-out
22. Mifanyiko ya ukaguzi – Checking processes.
23. Mifanyiko ya kimkokotoo – Computational processes
24. Mjumuiko – Interface
25. Nadharia ya ukaguzi – Checking theory
26. Nadharia ya ukaguzi wa uhusika - Case checking theory
27. Njeo (Nj) – Tense

28. Numerali – Numeration
29. Sarufi Bia (SB) – Universal Grammar
30. Sifa – Features
31. Spesifaya – Specifier
32. Uambishaji – Inflection
33. Usogezi – Movement
34. Umbo kifonetiki (UF) –Phonetic form.
35. Umbo mantiki (UM) – Logical form.
36. Unyambuzi – Derivation
37. Upatanishi yambwa (UPy) -Agreement object
38. Upatanishi kiima (UPk) – Agreement subject
39. Upatanisho dhaifu – Weak agreement
40. Upatanisho imara – Strong agreement
41. Uundaji miundo – Structure building
42. Uvurumishaji - Projection.
43. Uzalishaji – Derivations.
44. Visabiki vya viambishi – Pre-prefixes.
45. Yambwa na kiima kinachoonekana na kujisimamia – Overt object and subject.

Wilaya Za Kisii



-  Wilaya tatu za Kisii ambapo Ek huzungumzwa
-  Wilaya zinazopakana na Kisii

Kaskazini

